Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA NNE

**Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 17 Julai, 2006**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Samuel J. Sitta) Alisoma* Dua

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2006/2007.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA:**

Maoni ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI:**

Maoni ya Kambi ya Upinzani Kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha Uliopita, pamoja na Maoni Kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2006/2007.

**SPIKA:** Waheshimiwa kabla sijamwita Katibu kwa hatua inayofuata, inanibidi kutambulisha baadhi ya wageni. Kwanza, ninayo furaha kumtambulisha mke wa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Bibi Zainabu akiwa na wanawe pale. Nadhani ni utaratibu mzuri Waheshimiwa Mawaziri wa jinsia zote mbili, wenzi wao wawe wanakuwa hapa siku ya kuwasilisha hoja. *(Kicheko)*

Wageni wetu wale wa Jimbo la Lulindi waliokesha njiani, Madiwani 14, wamekwisha wasili. Mheshimiwa Suleman Kumchaya nadhani ndio wageni wake, nadhani watakuwa mkono wangu wa kulia pale. Wale wanatupungia mkono. Ahsante

Wapo wageni ambao ni viongozi wa Vyama vya Watu wenye Ulemavu (Leo mashine yetu inayowasaidia Walemavu kupanda juu kwenye *Public Gallery* haifanyi kazi) kwa hiyo niliomba wawe kwenye hii *Gallery* hii hapa kushoto, sijui kama wameweza kufika. Basi tutambue kuwepo kwao. Wapo pia wageni kutoka Jimbo la Kilindi, Wawakilishi wa Wachimbaji Wadogowadogo wa madini kutoka Wilaya hiyo.

Mwisho kabisa wapo wageni kutoka kwa Mheshimiwa Ezekiel M. Maige na Mheshimiwa James D. Lembeli, wako Madiwani 10 kutoka Halmashauri ya Kahama wakiongozwa na Mwenyekiti wao ambaye ni Mama Martina Sazia. Ahsante sana. *(Makofi)*

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 214

### Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bukombe

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA** Aliuliza:-

Kwa kuwa Wilaya ya Bukombe ni moja kati ya Wilaya ambazo hazina muda mrefu tangu kuanzishwa na inategemea huduma za afya hasa kwenye Hospitali ya Kahama iliyo umbali wa km 100 x 2 = 200 na hospitali ya Biharamulo na kuwa kuwa Bukombe imejitahidi sana kuanzisha ujenzi wa hospitali ya Wilaya kwa nguvu za wananchi, wadau mbalimbali ikiwemo Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

(a) Je, Serikali inaweza kulieleza Bunge mikakati iliyoandaliwa ya kuhakikisha ukamilishaji wa *OPD's*, Wodi na kwamba, sehemu nyingine za ujenzi zitakamilika katika Bajeti ili wananchi waanze kupata huduma kwa karibu zaidi na kuokoa maisha ya wananchi wa maeneo hayo?

(b) Kwa kuwa, hospitali hiyo iko mbioni kukamilika kama Serikali ikitenga fungu la kufanya hivyo haraka. Je, Serikali inaweza kutanga fedha za ununuzi wa vifaa hivyo vikiwemo vifaa vya *theatre*, *X-ray*, *OPD's*, *Dental Eye* na *MCH Departments*?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Emmanuel Jumanne Luhahula, Mbunge wa Bukombe lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Bukombe ulianza mwaka 2002 na umechangiwa kama ifuatavyo:-

(i) Nguvu za wananchi – Shilingi milioni 20.7; na

(iii) Serikali Kuu - Shilingi milioni 133.9.

Aidha Serikali kupitia *Local Government Capital Development Grant*, mwaka 2005/2006 imepeleka jumla ya Shilingi milioni 191.0 kwa awamu ya kwanza. Kati ya fedha hizi Shilingi milioni 44.0 zimeelekezwa katika ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, hali ya utekelezaji wa ujenzi wa Hospitali ni kama ifuatavyo:-

(i) Jengo la huduma za akina mama na watoto limekamilika.

(ii) Wodi tatu za wazazi, wanawake na wanaume zimekamilika.

(iii) *OPD* iko katika hatua za mwisho za umaliziaji.
(iv) *X-ray unit* iko hatua za mwisho za umaliziaji.

(v) *Minor- theatre* iko hatua za mwisho za umaliziaji.

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe itapelekewa jumla ya Shilingi milioni 313.1 kama awamu ya pili ya *Local Government Capital Development Grant*. Asilimia 50 ya fedha hizo zitaelekezwa katika miradi ya ngazi ya Wilaya ikiwa ni pamoja na hospitali ya Wilaya.

Ukamilishaji wa ujenzi wa Hospitali utategemea jinsi Halmashauri yenyewe itavyolipatia suala la ujenzi wa Hospitali umuhimu. Ikumbukwe kwamba Halmashauri yenyewe ndiyo inayoweka vipaumbele katika shughuli za maendeleo.

(b) Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali (a) jukumu la kupanga shughuli za maendeleo ni la Halmashauri yenyewe.

Idara mbalimbali zitakapoanza kufanyakazi vitendea kazi kama *X-ray* na vifaa vingine katika Idara za utalaam wa meno na macho na *MCH* vitanunuliwa kutoka bohari ya vifaa vya hospitali. Serikali Kuu na Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe zitashirikiana kuhakikisha kuwa vifaa hivyo vinapatikana.

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri; naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza:

Kwa kuwa ukamilishaji wa Hospitali hii ya kisasa uko mbioni na ambapo wakati wowote mwezi huu inaweza ikafunguliwa rasmi ili iweze kuanza kutumika kwa sehemu iliyokamilika:-

(a) Je, Serikali iko tayari kutoa vibali vya ajira tutakazozihitaji kwa ajili ya Hospitali hiyo na pamoja na hilo, Wizara itutumie Wataalam wengine kutoka Vyuoni kama ilivyokwisha ahidi?

(b) Je, Serikali inaweza kuwahakikishia wananchi wa Bukombe na Bunge hili Tukufu kwamba itawaunga mkono wananchi hawa kwa kuwapatia *Ambulance* haraka iwezekanavyo kwa juhudi walizozifanya na hapo hapo Waziri atakuwa tayari kupokea orodha ya *technical equipment* tutakazozihitaji ili nimkabidhi wazinunue?

**SPIKA:** Mheshimiwa, nimegundua baadaye kwamba unaonekana ulikuwa kama unasoma hilo swali. Ila nilichelewa tu kwa sababu nilikuwa napewa karatasi moja hapa. Kwa hiyo, ni bahati tu nimekuachia.

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba Nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa na vile vile nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kama alivyosema, hiyo Hospitali imefikia hatua ya kuizindua na nimekuwa na bahati ya kuizindua hiyo Hospitali kwa Niaba ya Serikali siku ya Ijumaa inayofuata. Ningependa kusema kwamba hiyo itanipa fursa ya kwenda kuikagua na kuelekeza na kuangalia mapungufu yako wapi ili tujue Serikali itafanyaje ili kuikamilisha kama Hospitali zingine.

**MHE. FUYA G. KIMBITA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza. Swali langu ni kwamba naulizia. Je, Serikali kwa kupitia Serikali za Mitaa labda, ina mpango gani wa kuimarisha Hospitali zilizopo kwenye njia kuu *(high way)* kutokana na hii hali ya ajali zinazotokea mara kwa mara hata ile ya Wilaya ya Hai ikiwa mojawapo?

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani hilo ni swali jipya. Tunaendelea. Swali linalofuata!

Na. 215

**Matengenezo ya Barabara Wilayani Sengerema**

**MHE. ERENEST G. MABINA** aliuliza:-

Kwa kuwa, mkakati wa kitaifa wa kupunguza umaskini na kukuza uchumi (MKUKUTA) unatambua umuhimu wa kuwepo Benki ya Kitaifa ya Maendeleo ya Wanawake, Tanzania kama nyenzo mojawapo ya kupambana na adha ya umaskini na kwa kuwa Serikali imekwishaamua benki hiyo ianzishwe:-

(a) Je, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inachukua hatua gani za vitendo kuanzisha benki hiyo?

(b) Je, Wizara haioni kwamba, kuendelea kuchelewesha uanzishwaji wa benki hiyo, kunawakatisha tamaa wanawake wa nchi yetu na kupunguza ari na kasi ya maendeleo yao?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Naomba kujibu swali la Mbunge kwamba barabara ya Nzera – Sungusira ni barabara ya Mkoa na iko kwenye kiwango cha changarawe. Aidha, barabara ya Sungusira – Idoselo – Misri – Mkolani – Lubanga hadi Busilasoga ni barabara ya Wilaya na ina urefu wa km. 53. Barabara hii imekuwa ikifanyiwa matengenezo mara kwa mara kama ifuatavyo:-

- Kwa Mwaka wa fedha 2003/2004, barabara ya Sungusira – Idosela yenye urefu wa km. 6 ilifanyiwa matengenezo katika maeneo korofi ya Sungusira hadi Nyakibanga kwa gharama ya shilingi milioni 4.2.

- Mwaka wa fedha 2004/2005, barabara hiyo kutoka Misri hadi Mkolani, yenye urefu wa km. 8 ilifanyiwa matengenezo kwenye maeneo korofi kwa gharama ya Shilingi milioni 7.8. Na kutoka Sungusira – Idoselo yenye urefu wa km 6 ilifanyiwa matengenezo kwenye maeneo korofi ya Sungusira hadi Nyakibanga kwa gharama ya Shilingi milioni. 4.1. Pia katika mwaka huo huo wa fedha, barabara ya Lubanga – Nyakaduha, yenye urefu wa km. 14 ilifanyiwa matengenezo katika maeneo korofi ya Luganga hadi Nyakaduha kwa gharama ya Shilingi milioni 18.2.
- Mwaka wa fedha 2005/2006, barabara ya Misri – Mkolani – Lubanga imefanyiwa matengenezo ya muda maalum kwa gharama ya Shilingi milioni 37.6. hasa katika sehemu za Misri – Ibisobageni, Misri – Mkolani hadi Ibisobageni.

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2006/2007 Serikali kupitia Halmashauri ya imetenga jumla ya Shilingi milioni 10. kwa ajili ya matengenezo ya kawaida Fedha hizo zitatumika kufanya matengenezo katika sehemu ya Mkoani – Nzela yenye urefu wa km. 3 kwa gharama ya Shilingi milioni1.5 na Kabanwa – Nyakaduha, yenye urefu wa km 12

kwa gharama ya Shilingi milioni 9. Kutokana na ufinyu wa bajeti, Serikali itaifanyia matengenezo kwa kiwango cha changarawe katika barabara hiyo wakati hali ya kifedha itakapokuwa ya kuridhisha. Kwa sasa Serikali itaendelea na jitihada zake za kuifanyia matengenezo katika maeneo korofi. Aidha, kutokana na urefu wa barabara hiyo, ambayo ni zaidi ya km. 50, Halmashauri ya Wilaya ya Geita itaangalia uwezekano wa kuweka katika programu ya Halmashauri ya mradi wa kitaifa wa usafiri vijijini kulingana na vipaumbele vya Halmashauri hiyo.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika jibu lake la msingi, amejibu kwamba barabara hii ilikuwa inatengenezwa kutoka Nzera – Idoselo – Misri – Mkolani – Liswageni – Kubanga II. Lakini kuna kipande ambacho sasa hivi hakijafanyiwa matengenezo kabisa cha kuanzia Lubanga – Mabagalu – Ikono – Bugilasoga, hiki kipande kimekuwa ni kisiwa na barabara ni moja hiyo hiyo. Je, Serikali inasemaje kutengeneza kipande hicho au kukipa pesa ili kiweze kutengenezeka na watu wakaweza kupita njia hiyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Katika Bajeti ya Wilaya ya Nzega na kwa fedha ambazo tutawapaia kutokana na Mfuko wa barabara, barabara zote ndogo ndogo zimeanishwa katika Bajeti ya Halmashauri ya Wilaya ya Geita. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge baada ya hapo, uje tuziangalie barabara hizo kama barabara hiyo haitakuwepo, tutaangalia utaratibu wa kufanya. Lakini, barabara zote zipo na zimeainishwa.

**MHE. KABUZI F. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza. Barabara za Wilaya ya Geita zimekuwa na matatizo makubwa sana kulingana na ukubwa wa Wilaya na mara nyingi fedha zimekuwa zikitolewa, vinatengenezwa vipande, matokeo ni kwamba Barabara karibu zote za Mkoa na za Wilaya hazipitiki. Je, Mheshimiwa Waziri sasa unaweza kuifikiria Geita kwasababu ina ukubwa sawa na Mkoa, kuifikiria kuipa fedha zaidi ili angalau barabara zianze kupitika?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu langu la msingi kwamba katika fedha za *Road Fund* ambazo zinagawiwa kwa kila Wilaya, barabara zitatengenezwa kwa awamu kulingana na fedha zilizotengwa na Mfuko huo. Iwapo fedha hizo zitaongezeka katia Mfuko wa *Road Fund*, nafikiri kila Wilaya itatengenezewa barabara zake ipasavyo. Lakini sasa hivi kutokana na Bajeti na ufinyu wa Bajeti za fedha za *Road Fund*, naomba Waheshimiwa Wabunge tuvumiliane, tupokee hicho kilichopo, tutengeneze barabara zetu kwa awamu na vipaumbele kulingana na uharibifu wa barabara zetu.

Na. 216

**Benki ya Taifa ya Maendeleo ya Wanawake**

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA (K.n.y. MHE. JENETH B. KAHAMA** aliuliza:-

Kuwa kuwa, mkakati wa kitaifa wa kupunguza umaskini na kukuza uchumi MKUKUTA unatambua umuhimu wa kuwepo benki ya Kitaifa ya Maendeleo ya Wanawake Tanzania kama nyenzo mojawapo ya kupambana na adha ya umaskini na kwa kuwa Serikali imekwishamua Benki hiyo, ianzishwe.

(a) Je, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto inachukua hatua gani za vitendo kuanzisha benki hiyo?

(b) Je, Wizara haioni kwamba kuendelea kucheleweshа uanzishwaji wa benki hiyo kunawakatisha tamaa wanawake wan chi yetu na kupunguza ari na kasi ya maendeleo yao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Janeth Kahama, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 Serikali iliruhusu kuwa Benki ya Kitaifa ya Maendeleo ya Wanawake Tanzania ianzishwe. Katika kutekeleza hii Wizara yangu imechukua hatua kadhaa za kuanzisha Benki hiyo. Hatua hizo za vitendo ni pamoja na kufanya utafiti wa kina wa kubainisha aina ya benki na uendelevu wake. Matokeo ya utafiti huo yameshawasilishwa na kukubaliwa na wadau mbalimbali. Aidha kamati ya watalaam iliundwa na imeweka mikakati ya uanzishaji wa benki hiyo. Mikakati hiyo ni kama vile utayarishaji wa mwelekeo wa benki *(road map),* mtaalam mwelekezaji aliteuliwa aliandaa na kupeleka nyaraka za usajili benki Kuu. Hatua zingine zinaendelea kuchukuliwa ili usajili ukamilike na hatimaye Benki iweze kuanza.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa uanzishaji wa Benki hiyo unaenda taratibu, hali hii inatokana na taratibu ndefu za maandalizi, upatikanaji wa fedha za kutosha na utalaam sahihi unaohitajika kabla ya kuanzisha Benki hiyo.

(c) Hata hivyo kutokana na mchakato mzuri ulioafikiwa hadi sasa, yapo matumaini makubwa kwamba benki hiyo itaanzishwa mapema.

**MHE. ESTHER K. NYAWAZWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba utaratibu unakwenda taratibu wa uanzishwaji wa benki hii ya Wanawake.

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuzipa *SACCOS* ambazo ziko mahali pote kuwasaidia wanawake kuongeza mtaji katika *SACCOS* hizo? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa utaratibu bado unakwenda taratibu wa kuanzisha benki ya wanawake. Je, Serikali sasa haioni umuhimu wa kutafuta angalau mbia wa kushirikiana naye katika kuanzisha benki ya wanawake? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Wizara inatambua umuhimu wa *SACCOS* na Wizara ina jukumu kubwa kushirikana na Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, kuhamasisha wananchi kuanzisha *SACCOS*. Kwa hiyo, sisi tumeshashauriana Wizarani na kupitia Maafisa Maendeleo walioko katika Halmashauri kuona kwamba zile *SACCOS* ambazo zitafanya vizuri basi tutaweka utaratibu wa kuzipitisha fedha ambazo tunazipeleka kwenye Halmashauri ili *SACCOS* ziweze zikakopesha akina mama.

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwamba je, Wizara ina utaratibu gani wa kumtafuta mbia kwa ajili ya kuweza kuharakisha taratibu hizi za kuanzisha benki. Napenda niseme kwamba katika kikao kilichofanywa na Mheshimiwa Waziri Mkuu na Rais wa Benki ya Dunia, sisi tulitoa hoja yetu hiyo kwa Rais wa Benki ya Dunia na ameonyesha kwamba anaweza akatusaidia katika suala hili. Kwa hiyo, bado majadiliano yanaendelea lakini hakuna *commitment* yoyote mpaka sasa hivi. (*Makofi*)

**MHE. AMINA C. MPAKANJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nilikuwa na swali moja kama ifuatavyo:-

Je, benki hii Mheshimiwa Naibu Waziri unaweza ukahakikishia labda ni lini itakuwa imeanza rasmi na itaanza labda katika baadhi ya Mikoa au itasambaa moja kwa moja nchi nzima na wenzetu wanaume ambao ni akina baba tunasaidiana nao wataruhusiwa kuingia katika benki hii au ni wanawake peke yao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, kwanza kama nilivyokwishasema kwamba benki hii tunataka ingeanza hata jana au leo. Lakini ndiyo hivyo taratibu zinaendelea. Benki hii ipo katika Ilani ya Uchaguzi kwa hiyo, ni ahadi ambayo tunaisimamia na tunataka ifanywe mapema ili tuweze tukapata imani ya wananchi kama walivyochagua. Kwa hiyo, tunafanya jitihada mwaka inshallh ianze.

Kuhusu wanaume kuwa wabia katika benki hiyo, hili linaongeleka wacha tuanze kwanza *inshallah* tutaweza kuongea baadaye. (*Makofi*)

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sambamba na kuanzisha benki hii ya wanawake na kuwapatia mikopo lakini ni vema kuwapatia elimu wanawake hao ya kuendesha miradi mbalimbali ili waweze kulipa vizuri. Je, Serikali imefanya utafiti gani kuona kwamba elimu ya biashara inawafikia wananchi hasa kule vijijini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, suala la elimu ya ujasiliamali na elimu ya biashara tunalipa

umuhimu wa pekee. Katika *component* ya kuanzisha benki tunalo suala hili la elimu. Kwa hiyo, tutahakikisha kwamba elimu inafika. Lakini kikubwa zaidi tunachokusudia ni kuona kwamba benki hii inawafaidisha akinamama wengi walioko vijijini na ndio maana utaratibu unachelewa kwa sababu tunataka tupate mfumo ambao utaweza kuwafikia akina mama vijijini na hasa maeneo yaliyoko pembezoni. Nashukuru. (*Makofi*)

Na. 217

**Uwezeshaji wa Wakulima Wadogo Wadogo**

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imepania kuwawezesha wakulima wadogo wadogo ili wajijengee uwezo wa kupunguza umaskini kwa mfano wakulima wadogo wa Milima ya Usambara Magharibi ambao wameanzisha umoja wao uitwao *Usambaa Tea Growers Association (UTEGA)* na hivyo kuuziwa Kiwanda cha Serikali cha Mponde:-

(a) Je, Serikali inafahamu kuwa kuna juhudi za wazi zinazofanywa na wakulima wakubwa wa chai katika maeneo hayo za kuuwa juhudi za wakulima?

(b) Je, kuwaruhusu wakulima wakubwa kuwa na juhudi za kuwakandamiza wakulima wadogo, sio uonevu na hivyo wahusika kustahili kushtakiwa katika Tume ya Haki za Binadamu kwa uonevu huo?

(c) Je, ni chombo gani kimewapa wakulima wakubwa leseni za kununua chai katika maeneo yenye vyama vya wakulima wadogo wanaohangaika kuondoa umaskini na watachukuliwa hatua gani?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa William Hezekia Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, napenda kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kihistoria zao la chai kama ilivyo Mkonge lilikuwa zao la mashamba makubwa (*estate Farms*) tofauti na mazao mengine ya biashara kama vile pamba, kahawa, korosho na tumbaku. Katika mwaka 1961, kabla ya uhuru wakulima wadogo wa chai chini ya Sheria ya Chai ya Mwaka 1954 *(The Tea Ordinance of 1954)* hawakuruhusiwa kulima zao la chai kwa sababu wakoloni waliwahitaji kuwa vibarua kwa ajili ya mashamba yao.

Mheshimiwa Spika, baada ya uhuru kuendelea kuzuia kilimo cha chai miongoni mwa wakulima wadogo kulionekana kupingana na dhamira ya kuleta maendeleo kwa wananchi. Kwa hiyo, mwaka 1968 Serikali ilifuta Bodi ya Chai Tanganyika na kuanzisha

iliyokuwa Mamlaka ya Chai Tanzania. Mamlaka hii ilipewa madaraka na mtazamo wa kuwahusisha wananchi katika kilimo cha chai pamoja na kufanya shughuli za usimamizi na udhibiti wa sekta ya chai nchini.

Kufuatia Sera ya Serikali ya kujitoa katika shughuli za biashara na uzalishaji, Mamlaka ya Chai, ilivunjwa mwaka 1997 na vyombo viwili vilianzishwa yaani Bodi ya Chai na Wakala wa wakulima wadogo wa chai. Wakala wa wakulima wadogo wa chai walipewa jukumu la kuendeleza zao la chai kwa wakulima wa nje ya viwanda *(outgrowers).*

Aidha, Bodi ilitoa kipaumbele kwa wakulima wadogo wa chai kwa kuwauzia hisa wakati wa kubinafsisha mashamba na viwanda vya chai vilivyokuwa chini ya mamlaka ya chai. Hivi sasa umoja wa wakulima wadogo wa chai Rungwe wana hisa asilimia 25, Lupembe asilimia 30 na Usambara asilimia 100. Hizi zote ni jitihada za makusudi za Serikali za kuhakikisha wakulima wa nje wa viwanda vya chai wanashirikishwa katika umilikaji wa kampuni yenye kiwanda.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo yangu hayo sasa najibu kwa ufupi swali la Mheshimiwa William Shellukindo lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Wizara haina taarifa kuhusu juhudi za wazi zinazofanywa na wakulima wakubwa wa chai katika maeneo hayo za kuua juhudi za wakulima wadogo.

(b) Mheshimiwa Spika, Sera ya Serikali ni ya kukuza ushirikiano baina ya wenye viwanda na wakulima wa nje ya viwanda (*outgrowers*) kwa mtindo wa kilimo cha mkataba (*contract growing*) kwa sababu watu hawa wanahitajiana. Kila upande unamhitaji wa upande mwingine.

(c) Ununuaji wa chai unatakiwa ufanywe kwa makubaliano ya wadau wote katika eneo husika chini ya uongozi wa bodi ya chai.

**MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa imeonekana wazi kwamba kuna upotoshaji wa dhana hii ya utandawazi na uchumi wa soko. Je, Waziri atakubaliana na mimi kwamba kuna haja ya kuendelea kuwaelimisha wafanyabiashara pamoja na wakulima wakubwa kwamba uchumi wa soko na utandawazi haina maana ya kufanya mambo kiholela? (*Makofi*)

(b) Kwa kuwa wakala wa chai wakulima wadogo umefanya kazi nzuri sana chini ya uongozi wa Wizara ya Kilimo. Je, Waziri haoni kama sasa ni wakati muafaka kwa wakala hiyo, sasa iwe na ofisi za kanda Kagera, Usambara Tanga, Rungwe na Njombe ili kuwa karibu zaidi na wakulima hawa wadogo ambao wameonyesha juhudi kubwa za kuondoa umaskini? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, suala la kuelimisha wakulima kuhusu mfumo wa soko ni suala linakubalika kabisa

na wakati Waziri anawasilisha Hotuba ya Bajeti, alielezea hata utaratibu tulionao wa kuwafahamisha wakulima katika Tanzania hali ya soko inavyoendelea. Kwa hiyo, suala hili halina mjadala nadhani ni suala zuri sana na linaendelea kufanywa. Labda kinachotakiwa tu ni kupanua wigo wa kuwapa taarifa.

Kuhusu wakala kuwa na ofisi ya kanda, mimi nadhani hili ni suala ambalo wadau wenyewe wa chai wanaweza wakalileta. Kama itaonekana kuwa na ofisi ya kanda itaongeza ufanisi wa utendaji au ukuzaji wa zao hili, mimi sioni kama Serikali itakataa.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa zao la mkonge linaipatia Serikali faida asilimia 99 katika mti mmoja wa mkonge na kwa kuwa wakulima wengi wameonyesha kuchoshwa na kuyaacha mashamba yao kutokana na kushuka bei ya zao hilo pamoja na kupanda gharama za uendeshaji hadi kufikia mavuno. Je, Serikali ina mpango gani katika kuongeza bei ya zao kwa mkulima?

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge, usiendelee ni swali jipya tunazungumzia zao la chai. Pole sana. (*Makofi*)

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mojawapo ya dhuluma zinazoendeshwa dhidi ya wakulima wadogo wadogo ni utaratibu wa kununua mazao yao kwa kutumia lumbesa. Je, Serikali itakubaliana sasa kwamba ni wakati muafaka kupiga mafuruku ununuzi wa mazao ya wakulima kwa kutumia lumbesa na badala yake watumie kilo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, sikusikia kwa kutumia nini, samahani.

**SPIKA:** Ufafanuzi wa swali Mheshimiwa Ngwilizi.

**MHE. BRIG. GEN. HASSAN A. NGWILIZI:** Mheshimiwa Spika, narudia tena. Kwa kuwa mojawapo ya dhuluma zinazoendeshwa dhidi ya wakulima wadogo wadogo ni kununua mazao yao kwa kutumia lumbesa badala ya kilo. Je, Serikali itakubaliana nami kwamba sasa ni wakati mufaka wa kupiga mafuruku ununuzi wa mazao ya wakulima kwa kutumia lumbesa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Wanatumia lumbesa linajazwa kupita kiasi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Spika, nimeelewa swali. Lakini mimi ni mara yangu ya kwanza kusikia chai inapimwa kwa lumbesa kwa hiyo, sina jibu la kumpa Mheshimiwa Mbunge, kuhusu hilo. Mimi sijaona chai inapimwa kwa lumbesa, lumbesa naona kwenye mpunga, mahinda na vitu vingine. Lakini kama hilo lipo basi naomba Mheshimiwa Mbunge, alilete tuzungumze

tuone kama kweli linatokea. Lakini jitihada ya Serikali kwa kweli ninavyojua ni kukazana kuhakikisha kwamba wakulima wadogo hawadhulumiwi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Hairuhusiwi usimame tena Mheshimiwa Brigedia. Ila Spika anaruhusiwa kutoa ushauri mdogo tu. Tuma watu huko badala ya kusema lete tena, swali ndiyo limekwishaulizwa Bungeni, Wizara itume mtu ili kuona ufumbuzi. (*Makofi/Kicheko*)

Na. 218

**Tatizo la Maji ya Bomba Geita**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, inaeleza wazi kuwa kufikia mwaka 2010 itatatua tatizo la maji kwa asilimia 90 (90%) mijini na asilimia 65 (65%) vijijini na kwa kuwa Mji wa Geita ulioko umbali wa kilometa 25 tu kutoka chanzo cha maji ambacho ni Ziwa Victoria una zaidi ya wakazi 100,000 na unaendelea kukua haraka kufuatia kuwepo kwa mgodi wa dhahabu Wilayani humo:-

(a) Je, Serikali inasemaje sasa kuhusu kilio cha wananchi wa Geita cha kuwapatia maji ya bomba ambapo kwa sasa hulazimika kununua maji yasiyo salama kutoka visima vifupi na ambayo hupatikana kwa shida?

(b) Je, Serikali inajisikiaje kuona wananchi wa Geita walioko jirani sana na Ziwa Victoria hawana maji wakati wale wa Shinyanga na Kahama walioko mbali sana na Ziwa hili wanapata maji?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa James Musalika, Mbunge wa Jimbo la Nyang’hwale, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua tatizo la maji katika Mji wa Geita hasa baada ya chanzo cha maji cha Bwawa la Namalembo kufungiwa maji yake yasitumike kwa matumizi ya binadamu tangu mwezi Agosti, 2003. Kuanzia wakati huo Serikali ilianza juhudi za kutatua tatizo hilo la maji kwa kufanya utafiti, upimaji na usanifu wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria.

Mapendekezo ya awali ni kujenga chanzo cha maji eneo la Senga Mchangani, umbali wa km 52 kutoka Geita Mjini na gharama ya mradi huo inakisiwa kuwa shilingi bilioni 18.5.

Mheshimiwa Spika, wakati tunasubiri utekelezaji wa mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria, Serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuboresha

upatikanaji wa huduma ya maji katika Mji wa Geita kwa kuchimba visima virefu na vifupi. Kati ya mwaka 2004/2005 hadi hivi sasa Serikali imechimba visima virefu kumi (10) na kufunga pampu za mkono kwa kushirikiana na Shirika la *Plan International* na visima hivyo vinatoa huduma. Wilaya inaendelea na uchimbaji wa visima zaidi kwa msaada wa Shirika hilo la *Plan International.*

Hatua zingine zilizochukuliwa ni kuchimba visima virefu viwili kwa msaada wa Kampuni ya *Geita Gold Mine.* Kisima kimoja kimefungwa pampu ya kutumia umeme *(Submersible pump)* na kinaendelea kutoa huduma. Wilaya pia imenunua pampu mbili kusukuma na kusambaza maji kutoka visima viwili vilivyopo eneo la Bomani na Mtaa wa 14 Kambarage. Kazi ya ujenzi wa mtandao kutoka kwenye visima hivyo viwili inaendelea.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kwamba jumla ya visima virefu na vifupi 21 vinafanya kazi Mjini Geita hadi sasa. Juhudi zote hizi zimesaidia upatikanaji wa maji mjini Geita kufikia asilimia 29 kutoka asilimia 16 ya mwaka 2002/2003. Aidha, Serikali bado inaendelea na juhudi za kutafuta fedha shilingi bilioni 18.5 kwa ajili ya kujenga mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali haijisikii vizuri kuona wananchi wake popote walipo wakiwemo wale wa Geita, Kahama na Shinyanga hawana maji. Ndiyo maana, inachukua hatua za kupeleka maji Kahama na Shinyanga na kuendelea kutafuta fedha kwa ajili ya mradi wa Geita. Suala la kusambaza maji ni la gharama na lazima utekelezaji wake uwe kwa mipango, inayotekelezwa hatua kwa hatua. Ndiyo maana yako maeneo mengine ambayo yako karibu na ziwa hata kuliko Geita, lakini pia hayana maji kutokana na kutokuwepo uwezo wa kuwahudumia wananchi wote kwa mara moja.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la msingi hapa ni uhaba wa maji na usalama wake na kwamba Serikali imesema imeshafunga chanzo kimoja kwa sababu kule kuna shughuli za madini, kuna zebaki na kwa kuwa takwimu alizotoa ni takwimu tu lakini hali halisi maji hakuna kule.

(a) Je, Serikali itushauri wakati wanasubiri wananchi wa Geita mipango hiyo, wanywe nini mbadala kwa sababu maji haya yaliyopo siyo salama na wewe umekiri? (*Makofi*)

(b) Je, Mheshimiwa Waziri, atakuwa tayari kuja Geita na kufanya mikutano kwa wananchi wa Geita na asije na maji ya chupa na afanye mkutano pia Nyang'hwale na Busanda kuhusu maji? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali yote mawili yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la awali nimeonyesha kiasi gani kwamba Serikali inajitahidi kwa kila hali ili kuhakikisha wananchi wa Geita wapate maji. Pia kwa juhudi za Serikali, imewaomba wafadhili ambao kwa sasa na wenyewe wanahangaikia pia Geita Mjini na Geita Vijijini, kuweza kuweka maji.

Mfano mmoja ni kwamba kwa hivi sasa Wafadhili *JAICA*, kutoka Japan pamoja na Serikali chini ya Wizara ya Maji tumekazana na miradi mingine ikiwemo miradi 10 zaidi ya Wilaya ya Geita ya Maji vijijini na pia *JAICA* wakiwa na miradi 11 ya maji hivi sasa iko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

**MHE. ERNEST G. MABINA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa katika jibu lake la msingi amesema kwamba wananchi wa Geita wanaopata maji ni asilimia 29 tu na waliobaki wote asilimia 69 hawana maji salama. Je, Serikali, inasemaje kuwanusuru hawa wananchi asilimia 71 ili waweze kupata maji salama katika maisha yao? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, narudia tena kama jibu la awali lilivyosema kwamba Serikali, kwa sasa hivi tunashughulika kutafuta shilingi bilioni 18.5 kwa ajili ya mradi mkubwa wa kudumu kwa ajili ya Mji wa Geita ambao mradi huu utatoka kwenye Ziwa Victoria na nina uhakika kabisa huu utakuwa wa kutosheleza hizo asilimia zilizobaki. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Dr. Mzindakaya kwanza karibu na hongera sana kwa kushinda kesi ya uchaguzi. (*Makofi*)

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri katika majibu yake amesema kuwa wanazungumza na wahisani ametaja Japan na wengine. Je, kama hao wahisani ambao ni wa nje hawatatoa misaada maana yake hawa wananchi hawatapata maji? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, wafadhili hao kama niliowataja wakiwepo *JAICA* ni kwamba wameshaanza hiyo kazi na kuna hatua mbalimbali za miradi hiyo, iliyofikiwa kwa hivi sasa.

Kwa hiyo, ni kwamba tuna uhakika na miradi hiyo ya kutoka Japan na pia tuna uhakika wa miradi kumi ile ambayo iko chini ya Program yetu ya maji safi na usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, miradi hiyo nayo ni ya uhakika kwamba watapata. Pia kwa sasa hivi huo mradi wa Geita tayari tumeanza kuongea na wafadhili mbalimbali na mfadhili mkubwa ambaye tunamtegemea na ameonyesha nia kabisa kwamba atasaidia ni hawa *Millenimu Goal Mine* ambao tayari wenyewe wamekubali watasaidia kuleta maji ya Geita. *(Makofi)*

Na. 219

### Msongamano wa Magari Katika Jiji la Dar es Salaam

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU** aliuliza:-

Kwa kuwa Jiji la Dar es Salaam lina mchango mkubwa sana kwenye pato la Taifa na kwa kuwa, msongamano wa magari unasababisha hasara kubwa ya muda, mafuta ya magari na kuathiri afya za wananchi kwa kupumua hewa yenye sumu inayotokana na moshi wa magari.

Je, Serikali ina mipango gani ya haraka ya kutatua tatizo hilo la msongamano wa magari Jijini Dar es Salaam?

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE DR. MILTON M. MAHANGA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mbunge wa Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Dar es Salaam ina mchango mkubwa kwenye uchumi wetu na kuwapo kwa msongamano wa magari kunaathiri uchumi na afya za wananchi wa Dar es Salaam.

Serikali kwa kutambua tatizo hilo la msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam, imeandaa mikakati mbalimbali ili kupunguza msongamano huo. Mikakati hii ni pamoja na mradi wa mabasi yaendayo kasi, upanuzi na ukarabati wa barabara kuu muhimu za Kilwa, Sam Nujoma na Mandela utakaoanza hivi karibuni, kuanzisha usafiri wa majini kwa kutumia boti kwa maeneo yaliyoko kandokando ya ufukwe wa bahari na kuboresha taa za barabarani na za kuongozea magari. Vile vile Serikali ina mpango wa kupanua barabara ya Ali Hassan Mwinyi kuwa njia nne kuanzia makutano ya Morocco hadi Tegeta.

Aidha, Serikali inashirikiana na wadau mbalimbali katika kutafakari tatizo hili la msongamano ili kupata ufumbuzi wa pamoja. Tayari mikutano miwili ya wadau wa tatizo hilo chini ya Uenyekiti wa Waziri wa Miundombinu, imekwishafanyika na mikakati ya ufumbuzi wa tatizo hili ilijadiliwa na kukubalika.

Moja ya mapendekezo muhimu ya Kamati hiyo ni kukarabati na kujenga barabara muhimu zinazounganisha barabara kuu za Jiji hilo na zile za pembezoni mwa Mji (*ring roads)* na pia kukarabati na kuboresha mfumo mzima wa taa za barabarani na za kuongozea magari. Makadirio ya gharama kwa mapendekezo ya kuboresha barabara hizo ni shilingi bilioni 8.3.

Mfumo wa taa za barabarani na za kuongezea magari kwa kutumia nishati mbadala wa mionzi ya jua *(solar energy)* ni shilingi 2.9 bilioni.

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Jiji la Dar es Salaam na Manispaa zake kupitia Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili kuhakikisha kuwa barabara za Jiji na Manispaa zinaimarishwa na hatimaye kutoa mchango katika kupunguza tatizo la msongamano Jijini Dar es Salaam.

Kwa sasa Serikali Kuu na Manispaa za Jiji la Dar es Salaam zipo mbioni kutafuta fedha hizo ili kukarabati barabara hizo muhimu ambazo zitasaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu. Kutegemea upatikanaji wa fedha, mradi huu utatekelezwa kwa awamu.

**MHE. DR. FESTUS B. LIMBU:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Nilikuwa napendekeza kwamba Serikali ichukue hatua kama ilivyochukua kwenye ujenzi wa jengo hili la Bunge lako tukufu kwa kujenga barabara za ghorofa *(fly overs)* moja litoke Boko mpaka UWT, nyingine Mailimoja mpaka UWT ziungane pale na nyingine itoke Kongowe na *Kilwa Road* na nyingine itoke Pugu ili ziungane Kamata, *(Fly overs)* hilo hatuhitaji fedha ya Serikali, hatuhitaji hela ya wafadhiri kwa sababu tatizo ni la haraka. Serikali inasemaje kutafuta wawekezaji ili barabara hizo ziweze kujengwa haraka kwa sababu magari yanazidi kuongezeka na yataongezeka zaidi katika kipindi kifupi kijacho? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, wazo alilolitoa na *fly overs* ni moja kati ya mapendekezo ya kuboresha hali ya usafiri na kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. Lakini ukweli ni kwamba *fly overs* ni ghali sana na kama Serikali ingekuwa na uwezo kwa kweli hiyo ni njia mojawapo nzuri.

Mheshimiwa Spika, tunachoweza kusema ni kwamba tunajaribu kuangalia kila aina ya njia kwa sababu kwa sasa kama unavyoona hata hizi bilioni kama kumi bado hatujazipata kwa ajili tu ya kuboresha barabara ambazo nimezitaja. *Fly overs* itakuwa ni ghali. Amependekeza kwamba inaweza kufanyika *fly overs* kwa njia ya *BOT* hili ni suala ambalo linaweza likaangaliwa lakini ukweli ni kwamba *investment* yake ni kubwa na kama anaweza akajitokeza kweli mwekezaji wa kufanya kazi hiyo tunaweza tukazungumza naye.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Waziri, kama utakumbuka mwaka 1967 kulikuwepo na *Dar es Salaam Master Plan* iliyokuwa imefadhiliwa na Serikali ya Canada. Toka wakati huo walikuwa wamependekeza kuwepo na *fly overs* kati ya Dar es Salaam mpaka sehemu za Kibaha.

Lakini kwa muda huu wote hakuna hata hatua iliyochukuliwa ili kufuata mapendekezo ya *Master Plan*. Leo hii tungekuwa tunazungumza nini kama ingekuwa tumekwishaanza kutekeleza wakati ule. Hivi sasa je, Waziri *plan* hii uliisikia, uliiona au haipo kabisa katika Wizara yenu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU (MHE DR. MILTON M. MAHANGA):** Mheshimiwa Spika, ni kwamba *master plan* hiyo ilikuwepo wakati huo mimi nilikuwa na miaka 12 tu kwa hiyo nadhani niliisikia nilikuwa mdogo mwaka 1967. Lakini, nieleze kwamba *Master Plan* kama anaweza kukumbuka na yeye zilifutwa. Sasa baadaye zilikuja kuwepo na miradi ya *sustainable cities* lakini ninachoweza kusema katika mipango yote hii lazima iendane na *investment plan.* Kama mipango ipo lakini uwezo wa kifedha haupo haiwezi kutekelezeka.

Kwa hiyo, naweza kusema ukweli kwamba tatizo limekuwa ni uwezo wa kifedha wa kutekeleza miradi hii mikubwa, pindi uwezo ukiwepo mimi nadhani miradi ambayo tunazungumzia ni ya kuboresha na nina hakika kwamba Wabunge, wana nia nzuri kama ambavyo Serikali inayo. Lakini tatizo ni uwezo pindi tukipata uwezo tutatekeleza kwa kadri ya uwezo huo na kulingana na mipango ambayo itakuwa inalingana na uwezo uliopo. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E.H. SHAH**: Ahsante Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii. Mimi nilikuwa nauliza kwamba kwa kuwa Serikali ina nia na ina uwezo wa kutaka kununua vivuko kwa ajili ya usafiri wa majini. Hivyo, ni kwa nini miaka yote ilikuwa inasita kununua vivuko cha kusafirisha abiria kati ya Mafia na Dar es Salaam ambapo ndiyo kuna watu wengi

**SPIKA:** Swali hilo ni jipya Mheshimiwa. Tunaendelea, swali linalofuata linaelekezwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

Na. 220

**Tofauti ya Ikama ya Walimu wa Sekondari**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Ikama ya walimu wa shule za sekondari hailingani kwa shule nyingi na hii inasababisha matokeo ya mitihani ya wanafunzi kutofautiana kwa kiasi kikubwa na kwa kuwa hali hiyo huzifanya shule zingine kupata sifa ya kufundisha sana na nyingine matokeo huwa mabaya:-

Je, Serikali inasema nini juu ya hali hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi kila shule ya sekondari inatakiwa iwe na ikama ya walimu iliyokamilika. Kutokana na uhaba wa walimu tulio nao nchini imekuwa vigumu kukamilisha ikama inayotakiwa katika kila shule. Hata hivyo matokeo ya mitihani ya wanafunzi hutofautiana kwa kiasi kikubwa baina ya shule za sekondari hakutokani tu na idadi ya walimu wa shule za sekondari kutolingana. Tofauti ya matokeo ya mitihani ya wanafunzi inasababishwa na mambo mbalimbali yakiwemo ya mazingira tofauti ya kufundishia na kujifunzia kama vile:-

(i) Tofauti ya upatikanaji wa huduma muhimu;

(ii) Kuwepo kwa viwango tofauti vya mwamko wa elimu katika jamii;

(iii) Kuwepo tofauti ya miundombinu ya msingi; na

(iv) Tofauti ya umahiri wa uongozi na utawala.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuwaandaa na kuwapeleka walimu kwenye maeneo yenye uhaba wa walimu kadri wanavyopatikana. Ni matumaini ya Serikali kuwa wananchi wataendelea kushirikiana na Serikali katika kuweka mazingira mazuri ya walimu ili waweze kubaki katika vituo vya kazi wanavyopangiwa, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu na kutatua kero zao katika maeneo yao ya kazi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri nina maswali madogo mawili ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa walimu wanaopangiwa kufundisha kwenye shule za vijijini hasa zile zenye kukosa miundombinu muhimu mfano nyumba, maji, zahanati, barabara na kadhalika wanakimbia kufundisha shule hizo. Je, serikali ina jitihada gani za ziada kuharakisha miunndombinu hiyo katika mikoa yote ambayo bado iko nyuma kimaendeleo ili shule hizi ziweze kuwa na walimu ambao hawatakimbia mara kwa mara?

(b) Kwa kuwa walimu wanaopangiwa kwenye shule hizi zenye mazingira magumu wanafanya kazi kwa mazingira magumu sana. Je, Serikali haioni kwamba kuna kila sababu ya kutoa posho maalum ya mazingira magumu ili iwe motisha kwa walimu wanaopangiwa shule hizo ili kuondokana na visingizio vya kukimbia shule hizo mpaka walimu sasa wanatafuta hata sababu ambazo sizo rasmi kukimbia shule hizo?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA):** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema katika jibu langu la msingi, ni kweli walimu wanaopelekwa katika shule za vijijini wengi wanakimbia kutokana na mazingira magumu na matatizo wanayoyapata hasa wakati wanapokwenda kuripoti. Lakini Serikali inasisitiza mazingira magumu ni lazima wananchi Halmashauri washirikiane ili kuweza kuondoa mazingira hayo magumu

ambayo yanawapata walimu. Ni jukumu la wananchi wenyewe ni jukumu la Halmashauri kushirikiana na Serikali ili kuweza kuyaondoa hayo mazingira hayo magumu.

Kuhusu suala la pili la posho maalum. Hili suala la kutoa posho maalum kwa walimu wanaofanya kazi katika mazingira magumu ya mikoa ile ambayo ina matatizo juu ya mazingira magumu. Serikali inalifahamu suala hili na ndiyo maana Tume imeundwa na Rais ili iweze kuangalia mazingira hayo magumu katika mikoa mbalimbali na katika mazingira mbalimbali iko namna gani halafu taarifa ile ikishapatikana tutajua ni jinsi gani ya kuweza kutoa posho au *allowance* ile ambayo itasaidia walimu katika mazingira magumu ili waweze kufanya kazi vizuri.

**WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii niongezee katika majibu aliyotoa Naibu Waziri kutokana na suala la nyongeza hasa la kwanza la Mheshimiwa Diana Chilolo, kuhusu mikakati ya Serikali. Serikali inatambua kwamba ili walimu wabakie katika maeneo yao ya kazi kwa kweli mazingira lazima yaboreshwe. Lakini kikubwa sana ni nyumba za walimu na kwa kutambua hilo kwenye Bajeti hii pia kuna fedha zimetengwa kwa ajili ya kuongeza nyumba za walimu pamoja na kwamba hazitatosheleza. Huo ni mkakati wa kwanza.

Lakini Mkakati wa pili, Serikali imeshaanza kuongea hasa ikisaidiwa na uongozi wetu wa ngazi ya juu akiwemo Mheshimiwa Rais, kuzungumza na *World Bank* ili tupate fedha za msaada wa kujenga nyumba za walimu. Na hali kadhalika tuna mazungumzo ambayo yanaendelea kati yetu sisi na Serikali ya Ireland kuona kama tunaweza kupata msaada. Zote hizi ni jitihada. Tunaweza tukapata au tusipate. Lakini ni mikakati ya Serikali kujitahidi kutatua tatizo la nyumba za walimu. Tukitambua kwamba ni muhimu sana. *(Makofi)*

Pamoja na hivyo naomba nirudie kama alivyozungumza Naibu Waziri kwamba Serikali peke yake haiwezi, hata kama tukipata misaada kutoka nje. Tunaomba Waheshimiwa Wabunge, Serikali za Halmashauri na wananchi kwa ujumla tusaidiane katika kutatua suala hili. Lazima watoto wapate elimu na jinsi ya kupata walimu ni kujenga nyumba za walimu katika maeneo yetu. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Na. 221

**Majengo yaliyokuwa Kambi za wapigania uhuru**

**MHE. RAMADHANI A. MANENO** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali iliachiwa majengo ya zilizokuwa kambi za wapigania uhuru wa nchi za Afrika Kusini:-

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa yale majengo yaliyokuwa ya Kambi ya *PAC Ruvu* – Kidogozelo yakatumika kuwa shule ya sekondari?

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI (MHE. MWANTUMU B. MAHIZA):** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ramadhani Maneno, Mbunge wa Chalinze, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kimsingi ni wazo nzuri kugeuza iliyokuwa kambi ya *PAC* Ruvu Kidogozelo kuwa Shule ya Sekondari. Hata hivyo, tunashauri yafuatavyo:-

Kwanza, wananchi kupitia Halmashauri itawalazimu kuomba umiliki wa majengo na eneo husika kutoka kwa wamiliki wa sasa. Pili, baada ya kupata umiliki Wizara yangu itatuma wataalam ili kupima uimara na kuangalia ubora wa viwango vilivyotakiwa katika kusajili wa shule mpya kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 kifungu 21(2).

**SPIKA:** Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Swali la mwisho. Naendeleza kidogo umefika muda wa kawaida kwa kipindi cha maswali kusitishwa, lakini mtakumbuka tulichukua dakika chache za kipindi hiki, kwa kutambulisha wageni. Kwa hiyo, swali la mwisho linaelekezwa kwa Usalama wa Raia. Nilitaka nataka katika hatua hii niseme kwamba Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, ambaye pia ndiyo Msemaji Mkuu upande wa Upinzani kwa Sekta ya Nishati na Madini, amefuata mfano mzuri sana wa CCM, mke wake naye kaja hapa. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Mama Fadhila yule pale amesimama anatupungia mkono. Ni mambo mazuri kwa vyama vyetu vya siasa kuigana kwa mambo mema haya. Ahsante sana. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 222

**Malipo ya Uhamisho kwa askari Polisi**

**MHE. MOHAMED HABIB MNYAA** aliuliza:-

Kwa kuwa jeshi la Polisi linapomhamisha askari mmoja toka Mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine anatakiwa afanyiwe taratibu zote za malipo ya uhamisho pamoja na familia yake; na kwa kuwa, askari yeyote akishapewa *Movement Order* ni uthibitisho kamili kwamba, anatakiwa ahame kutoka mahali alipokwenda kwenye kituo kipya alichopangiwa kazi:-

(a) Je, inakuwaje askari kubadilishiwa kituo kipya cha kazi tangu mwaka 2001 hadi leo lakini hajalipwa mafao yake licha ya kwamba hundi imeandikwa,

kama hii kwa *Movement Order No. B 017780, PF No. 58, PGO.0. No. 169 PHQ/Z/E365/12* na Hundi ya 220,000/= *PF.6?*

(b) Je, kwa nini wengine wanakataliwa kuchukua famila zao kama nilivyotaja kwenye sehemu (a) ya swali hili?

(c) Je, kwa nini uhamisho unatolewa wakati hakuna fedha za kuwalipa wahusika?
**NAIBU WAZIRI WA ISALAMA WA RAIA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed H. Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, uhamisho ni hatua inayochukuliwa na mwajiri ambapo mtumishi hutakiwa kuhama kutoka kituo kimoja cha kazi na kwenda kituo kingine kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika Idara husika au kukabili upungufu uliojitokeza katika kituo anachohamishiwa. Hata hivyo wakati mwingine uhamisho hutolewa baada ya maombi binafsi ya mtumishi mwenyewe kukubaliwa na mwajiri. Askari, anapoamriwa kuhama kutoka Wilaya moja hadi nyingine au Mkoa mmoja hadi mwingine hustahili kulipwa, posho ya kujikumu yeye na famili ayake kwa siku kumi na nne (14).

Askari ambaye huomba yeye mwenyewe kuhamishwa kutokana na sababu zake binafsi ambazo zitamridhisha mwajiri wake hupewa uhamisho, ambao hutakiwa kujigharamia mwenyewe.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo ya utangulizi, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Usalama wa Raia, napenda kumjibu Mheshimiwa Mohamed Habib Mnyaa, Mbunge wa Mkanyageni, swali lake lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, askari *Na. E4365 PC* Khamis Mohamed Khamis ambaye kituo chake cha kazi kilikuwa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja, aliomba kubadilishana Kituo cha kazi na askari Na. *F.494 PC* Said Khamis Khamis kutoka Mkoa wa Kaskazini Pemba. Askari hawa kwa pamoja na kwa hiyari zao waliuthibitihia uongozi wa Makao Makuu ya Polisi Zanzibar kwamba wako tayari kubadilishana vituo na kila mmoja yuko tayari kuligharamia uhamisho huo.

Mheshimiwa Spika, Makao Makuu ya Polisi Zanzibar yaliridhia ombi lao na kutoa amri ya uhamisho bila malipo kupitia ruhusa yenye Kumb. Na. *PHQ/Z/PF/E.4365/12* ya tarehe 31 Agosti, 2001. Hivyo basi askari Na. *E.4365 PC* Khamis Mohamed Khamis hakustahili malipo ya Tsh.220,000 kupitia hundi aliyoitaja Mheshimiwa Mbunge.

(b) Mheshimiwa Spika, baada ya amri ya uhamisho bila malipo kutolewa kwa askari Na. *E.4365 PC* Khamis Mohamed Khamis kupitia ruhusa Na. *PHQ/ZPF/E.4365/12,* askari huyu alikuwa na haki ya kuhamisha familia yake.

(c) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba baadhi ya askari wamekuwa wakihamishwa kabla ya kulipwa stahili zao za uhamisho.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2006/2007 Jeshi la Polisi limedhamiria kuondoa tatizo hili ili askari wanaopewa uhamisho waweze kulipwa stahili zao kabla ya kwenda katika kituo kipya cha kazi.

**MHE. HAFIDH ALI TAHIR:** Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Na vile vile nimshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake sahihi. Lakini inaonekana kutokana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, askari mhusika inaonekana amesema uongo.

Je, Jeshi la Polisi, limechukua hatua yoyote dhidi ya askari huyu? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ISALAMA WA RAIA:** Mheshimiwa Spika, kwa sababu taarifa za Mheshimiwa Mbunge tunazipokea na ushauri wa Mheshimiwa Mbunge tumeupata ili tuufanyie kazi ili tuone kwamba makosa yote yashughulikiwe kwa mujibu wa taratibu na kanuni za nidhamu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha. Ninayo matangazo hapa. Mheshimiwa Mussa Zungu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Mambo ya Nje, anawataarifu Wabunge Waheshimiwa wa Kamati ya Mambo ya Nje kuwa kutakuwa na kikao saa 4.30 leo chumba Na. 133. *(Makofi)*

Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mwenyekiti wa Maendeleo ya Jamii anatoa taarifa kwamba Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Jamii kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo leo saa 7 mchana baada ya kusitisha shughuli za Bunge Ukumbi Na. 231.

Naomba kuwatangazia kwamba Shirika la Taifa la Maendeleo ya Petroli *TPDC* limepanga maonyesho pale katika Ukumbi karibu Jengo la Utawala pale mnapoingia tu sehemu ile ambayo tulikuwa tunapatia barua pale.

Na ninadhani baadhi ya maonyesho mengine yapo kule upande wa maegesho ya magari. Mnaombwa Waheshimiwa Wabunge kwenda kuangalia kwa nafasi zenu shughuli za Shirika letu hili la Taifa la Maendeleo ya Petroli.

Waheshimiwa Wabunge walionunua magari kupitia *TOYOTA* wanaombwa kukutana na Makamishna wa Bunge saa 5 chumba na 133 inagongana na hiki tena. Sidhani kama Kamati ya Mambo ya Nje itamaliza mkutano kwa nusu saa. Kwa hiyo, nadhani mpange vizuri zaidi. Kwa sababu chumba hicho kinatumika na Kamati ya Mambo ya Nje.

Tangazo la mwisho Waheshimiwa Wabunge leo jioni tarehe 17 Julai, 2006 saa 2 usiku katika viwanja vya Bunge kutakuwa na burudani ya Kikundi cha band inaitwa *Rulu Arts Promoters* pamoja na vijana wa UMATI, watafanya maonyesho ya dansi hapo na Waheshimiwa Wabunge ambao wanajisikia wanaweza pia kucheza dansi. *(Makofi)*

Nadhani tayari watu wameanza kuitikia mwito ule kwamba jioni za hapa Dodoma kwa Waheshimiwa Wabunge wakati mwingine inakuwa imedorora sana sasa basi hiyo ni nafasi yenu.

Waheshimiwa Wabunge, nachukua nafasi hii kuomba kwamba kwenye dansi hilo Mheshimiwa Msindai na Mheshimiwa Halima Mdee wafungue dansi. Ahsanteni sana. *(Kicheko/Makofi)*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2006/2007 Wizara ya Nishati na Madini

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Biashara, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Matumizi ya fedha za Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2006/07.

Mheshimiwa Spika, kwenye sehemu ya utangulizi wa hotuba yangu ambayo itagawiwa kwa Waheshimiwa Wabunge ufafanuzi unapatikana katika ukurasa wa kwanza na wa pili, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mwaka 2005 na kuwa Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi (CCM) mwaka 2006.

Aidha, namshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuniteua kuiongoza Wizara hii. Pongezi zangu napenda kuzitoa kwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Dr. Ali Mohamed Shein, Waziri Mkuu Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Amani Abeid Karume

Mheshimiwa Spika, pia nitumie fursa hii kuwapongeza rasmi wewe na Naibu Spika kwa kuchaguliwa kwenu kuwa Spika na Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza Waheshimiwa Wabunge wenzangu wote kwa kupata fursa ya kuingia katika Bunge hili la Awamu ya Nne. Ninawaahidi Waheshimiwa Wabunge ushirikiano wa hali ya juu katika kutimiza majukumu yetu ya kitaifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuchukua fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Kibaha Vijijini kwa kunichagua kwa kura nyingi kuwa Mbunge wao. Nawaahidi kuwatumikia kwa uadilifu, kwa Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya.

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Utekelezaji utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2005/06 ulizingatia Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2000, Mpango wa Utekelezaji wa Ilani hiyo, Mpango wa Kimkakati wa Wizara na Programu ya Kazi ya Wizara. Kazi zilizopangwa kufanyika zilikuwa ni: kutekeleza miradi ya kupeleka umeme vijijini; kuanzisha Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini *(REA* na *REF* sawia); kusimamia, kufuatilia na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kutangaza ndani na nje ya nchi fursa zilizopo za uwekezaji katika sekta za nishati na madini; kuimarisha ukusanyaji wa mapato kutokana na sekta za nishati na madini; kuendeleza utafiti katika sekta za nishati na madini; kuboresha mazingira ya kuwasaidia wachimbaji wadogo ili kuongeza tija na uzalishaji; kuimarisha uwezo wa Wizara kutekeleza majukumu yake kwa kuwapatia watumishi mafunzo ya kazi na kujikinga na UKIMWI; kuajiri watumishi wapya na kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa kujenga na kununua majengo ya ofisi na vitendea kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 2005/2006 ni kuimarishwa kwa uwezo wa utendaji kazi wa watumishi ambapo watumishi 55 walipelekwa mafunzoni, kati yao 27 walishiriki katika mafunzo ya muda mfupi na 28 katika mafunzo ya muda mrefu. Mchakato wa kupata Bodi ya Wakurugenzi wa *REA* na *REF* na Mtendaji Mkuu wa Wakala ulianza. Ukarabati wa jengo la makao makuu ya Wizara katika Mtaa wa Samora na ununuzi wa jengo la ofisi ya madini Songea, ulifanyika. *(Makofi)*

Aidha, warsha na semina kuhusu njia za kujikinga na maambukizi ya virusi vya UKIMWI zilifanyika kwa watumishi wa Wizara, wachimbaji wadogo na wadau wengine katika maeneo ya Mahenge, Masasi, Geita na Songea. Kazi ya ukaguzi wa migodi, kusimamia matumizi ya baruti, hifadhi ya mazingira na kuzingatiwa kwa sheria na kanuni za uchimbaji na biashara ya madini ilifanyika katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo maeneo ya Merelani, Geita, Shinyanga, Kilindi, Handeni, Kigoma, Musoma na Mbeya. *(Makofi)*

Vile vile, katika kuimarisha uwezo wa utendaji kazi wa watumishi, mafunzo ya Upimaji wa Wazi wa Utendaji Kazi *(OPRAS)* yalifanyika kwa baadhi ya watumishi wa Wizara kwenye vituo vya Arusha, Dar es Salaam, Mwanza, Morogoro na Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya juu kwenye gridi ya Taifa ni Megawati *(MW) 562,* lakini kutokana na ukame ulioikabili nchi yetu katika miaka mitatu mfululizo, uwezo wa uzalishaji umeme unaotokana na maji katika mitambo ya Mtera, Kidatu, Nyumba ya Mungu, Pangani, Hale, na Kihansi, ulishuka. Uzalishaji umeme katika mitambo hiyo ulikuwa na upungufu wa wastani wa *MW120.* Hali hii iliifanya *TANESCO* kutegemea zaidi umeme unaozalishwa na vituo vya *IPTL* na Songas. Upungufu huo ulisababisha umeme utolewe kwa mgao nchini kote kuanzia tarehe 5 Februari hadi tarehe 28 Machi, 2006 na kuanzia tarehe 8 Juni, 2006 hadi sasa. Katika mgao unaoendelea, biashara na viwanda vikubwa vimelindwa ili visiathirike katika uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza miradi ya kupeleka umeme vijijini, miji mikuu ya wilaya za Urambo, Serengeti na Ukerewe ilipata umeme kati ya Septemba na Desemba, 2005. Katika kuendeleza utafutaji mafuta, mikataba mitatu ya kugawana mapato (*Production Sharing Agreements (PSA)* katika kina kirefu cha bahari *Block* 2, 6 na *Block* ya Tanga, ilisainiwa. Aidha, shughuli za utafutaji mafuta na gesi zilifanyika katika maeneo ya Nyuni, Songo Songo Mashariki, Mandawa, Kisangire, Bigwa, Rufiji, Mafia, eneo jipya la Songo Songo na eneo la utafiti katika kina kirefu cha bahari, *Block* 1 na 5.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2005/2006, kazi zilizopewa kipaumbele kwenye eneo la nishati mbadala ni kuendeleza na kuhamasisha matumizi ya majiko sanifu ya mkaa na kuni, mabaki ya mimea, na vitofali vya makaa ya mawe (*briquettes).* Wizara iliendelea kukusanya taarifa za maporomoko madogo ya maji nchini kwa mikoa ya Ruvuma, Rukwa na Iringa. Taarifa za kasi ya upepo zilichukuliwa katika vituo vipya vya Mgagao (Mwanga), Makambako (Njombe) na Kitimo (Singida). Aidha, Serikali ilisimamia utekelezaji wa miradi ya umemenuru kwa nia ya kuondoa vikwazo vya ukuaji wa soko la vifaa vitumiavyo mionzi ya jua.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kujadiliana na *Kilimanjaro Industrial Development Trust (KIDT)* ya Moshi juu ya utafiti wa kuzalisha *briquettes* kwa kutumia vyanzo vingine vya tungamotaka kwa ajili ya kupikia. Kuhusu vitofali vya makaa ya mawe, Serikali iliwezesha majadiliano kati ya *Kiwira Coal Mines Limited* na wadau kutoka Japan. Aidha, Wizara iliendelea kushirikiana na Kampuni ya *Katani Ltd,* pamoja na *UNIDO* na *Common Fund for Commodity* katika kutayarisha mradi wa bayogesi kwa ajili ya kuzalisha umeme kutokana na mabaki ya mkonge. Sampuli za maji zilizokusanywa Amboni Tanga na kwenye maziwa ya Manyara na Natron zilipelekwa maabara ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ikiwa ni sehemu ya utafiti wa jotoardhi. Matokeo ya uchunguzi yanasubiriwa.

Mheshimiwa Spika, Serikali iliendelea kusimamia na kuratibu programu ya tungamotaka (*Programme for Biomass Energy Conservation (ProBEC),* inayotekelezwa na Shirika la

Kiufundi la Ujerumani *(GTZ)*. Mpango huu unatekelezwa na baadhi ya nchi za *SADC* ikiwemo Tanzania kwa nia ya kuhakikisha matumizi bora ya tungamotaka. Mradi huu umetoa mafunzo katika mikoa ya Ruvuma na Mwanza ambapo mafundi 20 wa kutengeneza majiko walifundishwa na vituo viwili vyenye uwezo wa kuzalisha majiko sanifu 300 kwa mwezi, vilianzishwa.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Serikali wa *Geological Survey of Tanzania (GST),* ulikusanya takwimu za kijiolojia, kikemia na kijiofizikia kwenye maeneo ya wilaya za Kahama na Biharamulo. Aidha, utayarishaji wa ramani za kijiolojia katika maeneo ya Mpanda na Chunya, ulifanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005/2006 katika Chuo cha Madini, wanafunzi 15 walihitimu mafunzo ya miaka mitatu (3) ya cheti cha ufundi sanifu, wanafunzi 20 walikuwa katika mafunzo ya mwaka wa pili na wanafunzi 40 katika mafunzo ya mwaka wa kwanza. Chuo kinafanyiwa ithibati (*accreditation*) na Baraza la Vyuo vya Kiufundi Nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha utekelezaji cha mwaka 2005/2006, sekta ya nishati ilikumbwa na vikwazo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ukosefu wa maji katika mabwawa ya kuzalisha umeme, bei kubwa ya mafuta na ukosefu wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Mpango na Bajeti kwa mwaka 2006/2007 imeandaliwa kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya mwaka 2005; MKUKUTA; Mwongozo wa Utayarishaji wa Mpango na Bajeti wa mwaka 2006/2007 – 2008/2009; Sera za Jumla za Uchumi na Maendeleo ya Jamii kwa mwaka 2006/2007 -2008/2009; Maagizo ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyoyatoa alipoitembelea Wizara mwezi Januari, 2006 na Mpango wa Kimkakati wa Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005 mchango wa sekta ya nishati ya umeme kwenye Pato la Taifa ulikuwa asilimia 1.4 sawa na mwaka 2004. Ukuaji wa sekta ya nishati ya umeme ulikuwa asilimia 5.1 ikilinganishwa na asilimia 4.5 mwaka 2004. Umeme uliozalishwa kwa mwaka 2005 ulifikia *Gigawatt hours* 3,620.5 ikilinganishwa na *Gigawatt hours* 2,126.4 zilizozalishwa mwaka 2004, sawa na ongezeko la asilimia 58.7. Ongezeko hilo lilitokana na kuanza kutumika kwa mitambo miwili ya Songas Ubungo yenye jumla ya MW 75.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2006/2007 malengo ya sekta ya nishati ni pamoja na: kuimarisha na kuendeleza mfumo wa umeme nchini unaojumuisha uzalishaji, usafirishaji na usambazaji. Kuratibu utekelezaji wa mpango wa dharura na mpango wa muda wa kati na mrefu wa kupunguza utegemezi wa umeme unaozalishwa kutokana na maji kwa kutumia vyanzo vingine vya nishati vinavyopatikana nchini kama vile gesi na makaa ya mawe; kusimamia shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi; kuratibu na kusimamia maendeleo ya nishati mbadala; na kuhamasisha uwekezaji katika sekta ya nishati.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa katika mwaka 2006/2007 ni: Kupeleka umeme vijijini, kuendeleza miradi ya vyanzo mbadala katika uzalishaji umeme, kuboresha na kuipanua gridi ya Taifa ya umeme, kuboresha na kupanua mfumo wa usambazaji wa umeme, kupanua vyanzo vya ukusanyaji wa maduhuli kutoka katika sekta ya nishati, kuratibu utekelezaji wa miradi ya nishati, kuendeleza utafutaji mafuta nchini, kuiwezesha *TPDC* kushiriki katika miradi ya Songo Songo na *Mnazi Bay,* kuitangaza sekta ya nishati na kushiriki katika majadiliano na wawekezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukame wa muda mrefu uliosababisha upungufu wa maji katika mabwawa yenye mitambo ya kuzalisha umeme, Serikali imechukua hatua za muda mfupi na wa kati kukabiliana na tatizo hilo. Hatua za muda mfupi zilizochukuliwa ni pamoja na kununua mitambo ya *MW 100* itakayofungwa Ubungo na mingine ya *MW 45* itakayofungwa eneo la Tegeta. Mtambo wa Tegeta utatumia fedha za Serikali na msaada kutoka Serikali ya Uholanzi. Aidha, Serikali itakodi mitambo ya *MW 100* na kuifunga Ubungo. Mitambo hii yote itazalisha umeme kwa kutumia gesi asilia ya Songo Songo na inatarajiwa kuanza kuzalisha umeme kati ya mwezi Novemba, 2006 na Julai, 2007. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara imekamilisha majadiliano na Kampuni ya *Kiwira Coal and Power Limited (KCP)* ili kupanua uwezo wa kuzalisha umeme wa Kituo cha Kiwira kwa *MW 200* kwa kutumia makaa ya mawe yaliyopo Kiwira na Kabulo. Mkataba wa makusudio wa kuweka misingi ya uendelezaji wa mradi huo (*Agreement of Intent)* kati ya Serikali, *TANESCO* na *KCP* ulisainiwa mwezi Machi, 2006. Mchakato wa kupata ridhaa ya Serikali kwa ajili ya ujenzi wa mradi umeanza.

Mheshimiwa Spika, mpango wa muda wa kati wa kuongeza uzalishaji umeme katika gridi ya Taifa ni kufunga mitambo ya gesi ya kati ya *MW 200* hadi 300 eneo la Kinyerezi ifikapo mwaka 2010, pamoja na kutekeleza mradi wa Ruhudji wenye uwezo wa kuzalisha *MW 358* kwa kutumia nguvu ya maji ifikapo mwaka 2012.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Uunganishaji wa gridi za taifa za umeme za Zambia,Tanzania na Kenya umefikia hatua ya uendelezaji. Katika kikao cha Mawaziri wa nishati kilichofanyika Mei, 2006 Mombasa, Kenya, ratiba ya uendelezaji wa mradi iliidhinishwa. Aidha, mshauri mwelekezi atakamilisha mchakato wa kutafuta fedha ifikapo mwezi Mei, 2007.

Mheshimiwa Spika, vituo vingi vya uzalishaji umeme kutokana na maji viko katika mikoa iliyo Kusini Magharibi ya nchi. Ongezeko la uzalishaji wa umeme linatakiwa kwenda pamoja na kuimarishwa kwa gridi ya Taifa ya umeme na kupanuliwa kwa gridi hiyo ili iifikie mikoa yote ya Tanzania. Mpango na Bajeti kwa mwaka 2006/2007 umetenga fedha kwa ajili ya kuimarisha na kupanua mfumo wa gridi ya umeme nchini. Gridi ya *kV 220* kutoka Iringa hadi Singida kupitia Dodoma itaimarishwa.

Hatua za utekelezaji wa miradi ya upanuzi wa gridi ya *kV 220* kutoka Bulyanhulu kwenda Geita na kutoka Shinyanga hadi Buzwagi na ya *kV 132* kutoka Musoma hadi

Tarime, zitaanza. Aidha, hatua za awali za ujenzi wa gridi ya msongo wa *kV 132* kutoka Tabora hadi Kigoma na kutoka Makambako hadi Songea zitaanza katika mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, mifumo ya usambazaji umeme katika miji ya Arusha, Moshi na Dar es Salaam itaboreshwa ili kuimarisha upatikanaji na ubora wa umeme katika miji hiyo na kuondoa upotevu wa umeme (ulioongezeka kutoka asilimia 23 mwaka 2004 hadi asilimia 27 mwaka 2005), matatizo ya umeme kukatikakatika na umeme hafifu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, programu ya kuwezesha na kuongeza upatikanaji wa umeme vijijini *(Energizing Rural Transformation (ERT)* itaanza kutekelezwa. Miradi iliyofanyiwa upembuzi yakinifu ni ya Mtwara, Lindi, Njombe, Mufindi, Morogoro, Kilimanjaro, Manyara na Kisiwa cha Mafia. Aidha, msisitizo katika programu hii unalenga kueneza matumizi ya umemenuru kwenye makazi yaliyo mbali na mtandao wa gridi ya Taifa, mashule na kwenye zahanati. Aidha, upeo wa programu utapanuliwa ili kujumuisha maeneo mengi zaidi.

Mheshimiwa Spika, chini ya mradi wa Songo Songo, kituo cha *MW 6* kinajengwa eneo la Somanga Funga, wilayani Kilwa kwa lengo la kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia kwa ajili ya miji ya Kilwa Masoko, Utete, Ikwiriri na Kibiti. Pia, vijiji kadhaa vilivyoko katika eneo la mradi vitapatiwa umeme na maji. Kazi ya ujenzi wa kituo hicho inatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2007.

Kisiwa cha Songo Songo kimepewa upendeleo maalumu kwa kusambaziwa umeme na maji safi ya kunywa kutoka kwenye kiwanda cha kusafisha gesi cha Songas, kuboresha zahanati na kujenga kituo kidogo cha Polisi. Pia maeneo ya Kinyerezi na Salasala mkoani Dar es Salaam, yaliyotengwa kwa ajili ya wananchi waliohamishwa kwenye mkuza wa bomba la gesi, yatajengewa miundombinu ya barabara, maji na umeme ili kuboresha maisha yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali haina uwezo wa kusambaza umeme nchi nzima kwa mara moja, iliamua kutekeleza jukumu hili kwa awamu. Mpango wa awali wa usambazaji umeme ulikuwa kuanza na makao makuu ya mikoa na wilaya. Hadi sasa makao makuu ya wilaya 18 hayajapatiwa umeme. Maeneo ambayo yangefuatia ni ya sehemu za uzalishaji mkubwa, miradi mikubwa ya kijamii kama maji na hospitali na maeneo kando kando ya njia kuu za umeme. Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kupeleka umeme katika miji mikuu ya Mbinga, Orkesmet, Ushirombo, Kilolo, Utete, na Ludewa.

Aidha, maombi ya fedha kwa ajili ya makao makuu ya wilaya zilizobaki yamejumuishwa katika mpango wa Taifa uliowasilishwa kwenye Shirika la *Marekani la Millennium Challenge Corporation (MCC).* Aidha, chini ya ufadhili wa *UNDP/GEF* Wizara itaendeleza mradi wa soko la umemenuru mkoani Mwanza kwa lengo la kuondoa vikwazo vya matumizi ya umemenuru kama nishati mbadala.

Wakala na mfuko wa nishati vijijini baada ya mchakato wa kupata uongozi wa *REA* na *REF* kukamilika, utekelezaji wa majukumu yake utaanza baada ya Mtendaji

Mkuu wa Wakala na wasaidizi wake kuajiriwa. Aidha, fedha za kuanzishia Mfuko huo zimetengwa kwenye Bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati Maalumu ya Wataalamu inayojumuisha wajumbe kutoka Wizara na taasisi mbalimbali imeundwa ili kuharakisha utekelezaji wa mradi wa Mchuchuma. Hadidu za rejea za Kamati hiyo ni pamoja na kuratibu zoezi zima la kumpata mwekezaji wa mradi wa Mchuchuma na chuma cha Liganga; kufanya tathmini ya mapendekezo yaliyowasilishwa na wawekezaji; kutoa ushauri kuhusu njia bora ya kuendeleza miradi ya Mchuchuma na Liganga na kuzingatia mkakati wa utekelezaji wa Ilani ya CCM ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, mwezi Septemba, 2005 *TANESCO* iliondolewa katika orodha ya mashirika yaliyokusudiwa kubinafsishwa. Uamuzi huu ulifikiwa baada ya Serikali kutafakari upya unyeti na umuhimu wa huduma ya umeme kwa uchumi na maendeleo ya nchi. Aidha, mkataba uliopo wa uendeshaji wa *TANESCO* chini ya *NetGroup Solutions* unaisha mwezi Desemba, 2006. Serikali kwa kushirikiana na Bodi ya Wakurugenzi wa *TANESCO* inaandaa mkakati wa kuendesha *TANESCO* utakaozingatia maslahi ya nchi baada ya muda wa mkataba wa *NetGroup Solutions* kuisha.

Mheshimiwa Spika, Wizara itaendeleza juhudi za kuwavutia wawekezaji kutafuta mafuta na gesi nchini. Wizara itawasilisha mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Utafutaji na Uzalishaji Petroli ya mwaka 1980 kwa lengo la kuiwianisha na sheria nyingine ili kurahisisha utekelezaji wake. Aidha, majadiliano yanaendelea kati ya Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar juu ya namna bora ya kusimamia utafutaji mafuta kwa manufaa ya nchi yetu.

Kampuni zenye leseni na maeneo yanayoendelea kufanyiwa utafutaji ni:- *Petrobras* ya Brazil (*Block 5*); Dominion ya Uingereza (Kisangire, Mandawa na Selous); *Maurel and Prom ya Ufaransa (Bigwa, Mafia); Ndovu Resources* (eneo la Nyuni na Bonde la Ruvuma) na *Ophir Energy* za Australia (*Block* 1,3 na 4). Aidha, leseni ya kampuni ya *Antrim* ya Canada haijaanza kufanyiwa kazi katika maeneo ya Zanzibar na Pemba. Serikali inaendelea na majadiliano na kampuni kadhaa ili zianze kutafuta mafuta. Kampuni hizo ni pamoja na *Petrobras (Block 6); Statoil* ya *Norway (Block* 2) na *Petrodel* ya Uingereza (eneo la Tanga).

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *Mnazi Bay,* utekelezaji wa mradi wa kuzalisha umeme kutokana na gesi asilia ya *Mnazi Bay* unaendelea. Hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa mradi ni pamoja na uchorongaji wa kisima kingine kati ya viwili vinavyokusudiwa ili kuhakikisha upatikanaji wa gesi ya kutosha kwa ajili ya mradi wa umeme na miradi mingine itakayobuniwa. Ujenzi wa mtambo wa kusafisha gesi asilia uko katika hatua za mwisho.

Ujenzi wa bomba la kusafirisha gesi kutoka Msimbati hadi Mtwara unatarajiwa kukamilika hivi karibuni. Maandalizi ya ujenzi wa msingi kwa ajili ya kituo cha kuzalisha umeme Mtwara yamekwishaanza. Majadiliano ya mikataba ya utekelezaji wa mradi utakaosaidia kupatikana kwa umeme wa uhakika katika mikoa ya Lindi na Mtwara

kati ya Serikali na *Artumas Group* yamefikia hatua za mwisho. Aidha, makubaliano yamefikiwa kwamba katika kipindi cha mpito Artumas watawauzia umeme *TANESCO* ili waendelee kuusambaza wakati wao wakiendelea kukamilisha ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya kuunganisha Mtwara, Lindi na Masasi. Hatua hii itawafanya watumiaji wa umeme Mtwara kuanza kupata umeme kutokana na gesi asilia mapema.

Mheshimiwa Spika, Bomba la Mafuta Dar es Salaam – Mwanza, Serikali inafanya mazungumzo na wawekezaji waliojitokeza kuwekeza katika kujenga kiwanda cha kusafisha mafuta na ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Ni matumaini yetu kuwa majadiliano hayo yatakamilika katika kipindi cha mwezi mmoja ujao.

Mheshimiwa Spika, Ushiriki wa *TPDC* Katika Miradi,ushiriki wa *TPDC* katika miradi ya Songo Songo na *Mnazi Bay* utaongeza mgao wa Serikali kutokana na uwekezaji unaofanyika katika miradi hiyo. Katika *PSA, TPDC* imepewa fursa ya kushiriki kwa kiasi cha hadi asilimia 20 katika uwekezaji wowote utakaofanyika kwenye miradi ya gesi asilia ya Songo Songo na *Mnazi Bay.* Ushiriki wa asilimia 20 utaifanya *TPDC* kupata gawio kubwa la faida itakayopatikana kutokana na mradi husika na Serikali kupata gawio la kufidia gharama ilizochangia.

Aidha, kutoshiriki kwa *TPDC* katika kuwekeza kwenye miradi hiyo kunawapa fursa wawekezaji wengine kutumia fursa ya *TPDC* na hivyo kujipatia gawio kubwa kutokana na faida itakayopatikana kwenye mradi husika. Mwaka 2006/2007 *TPDC* imetengewa fedha kidogo kwa lengo hilo ingawa mahitaji yake ni makubwa.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Nishati Mbadala, kutokana na kukua kwa teknolojia za nishati mbadala Wizara itaendelea kuongeza kasi ya kuwapatia wananchi walio wengi huduma bora za nishati mbadala, kutunza mazingira na kusimamia utekelezaji wa mikataba ya kimataifa katika eneo hili kwa kuendeleza vyanzo mbadala vya nishati kama vile jua, upepo, tungamotaka, maporomoko ya maji, jotoardhi na makaa ya mawe. Aidha, baada ya Serikali kuondoa ushuru kwenye vifaa vya *solar* mwaka 2005/2006, bei ya vifaa hivyo imepungua kwa takriban asilimia 20 ikilinganishwa na bei kabla ya Julai, 2005. Matokeo ya hatua hiyo ya Serikali ni ongezeko la kasi ya ununuzi wa vifaa hivyo kama taarifa zilizopatikana kutoka kwa wadau, hususan, wale wa mkoa wa Mwanza zinavyoonesha.

Mheshimiwa Spika, mradi mwingine wa umemenuru unaofadhiliwa na Serikali ya Sweden kupitia Sida utaanza kutekelezwa katika mikoa ya Iringa, Morogoro na Kigoma. Ni matarajio ya Serikali kuwa miradi hii itakapokamilika itaonesha manufaa ya nishati hii kwa wananchi na hivyo kuchangia katika kufikisha huduma za umeme vijijini. Pamoja na miradi hiyo, asasi zisizo za kiserikali pamoja na sekta binafsi zinaendelea kuhamasisha matumizi ya umemenuru katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, uendelezaji wa bayofueli ni eneo jipya lililopewa kipaumbele katika bajeti hii. Mradi huu una lengo la kuzalisha mafuta ya mimea (dizeli na *ethanol*) kwa ajili ya kuendeshea mitambo. Pamoja na faida nyingine za bayofueli, mradi unalenga kuchangia katika kupunguza utegemezi wa mafuta ya petroli katika kuendesha mitambo.

Kamati Maalumu ya Kitaifa ya Bayofueli *(National Biofuel Task Force)* imeundwa ili kuandaa taratibu za kuwezesha maendeleo ya bayofueli nchini. Mimea inayoangaliwa hapa ni pamoja na mbono kaburi *(jatropha),* moringa, miwa, michikichi, mtama na alizeti.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007 *Programme for Biomass Energy Conservation* itaendeleza utafiti wa jiko linalotumia mkaa, kuni, tungamotaka lijulikanalo kama *rocket* ili lizalishwe hapa nchini kwa kutumia malighafi za hapa. Pia, programu itaangalia uwezekano wa kutumia matanuri bora ya kukaushia tumbaku ambayo yanatumika katika nchi ya Malawi. Aidha, jiko ambalo hutumia mafuta ya mimea liitwalo *bosch* litafanyiwa majaribio.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Madini, Ukuaji wa Sekta ya Madini, mwaka 2005 mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 3.5 ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2004. Ukuaji wa sekta hii mwaka 2005 ulikuwa asilimia 15.7 ikilinganishwa na asilimia 15.4 mwaka 2004 na hivyo kufanya sekta hii kuendelea kuwa mojawapo ya sekta zinazokua kwa kasi kubwa.

Mauzo ya madini nje kwa mwaka 2005 yalikuwa na thamani ya Dola za Marekani milioni 711.3 ikilinganishwa na Dola milioni 680.2 mwaka 2004. Ukuaji wa sekta hii ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kuanza kwa uzalishaji wa dhahabu katika mgodi wa Tulawaka na ongezeko la bei ya dhahabu katika soko la dunia.

Mheshimiwa Spika, Malengo ya Sekta ya Madini, malengo ya sekta ya madini kwa mwaka 2006/2007 ni kutekeleza ahadi zilizomo ndani ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 kuhusu kuwasaidia wachimbaji wadogo na kuongeza ajira; kuimarisha usimamizi wa sekta; kuhamasisha na kusimamia uchenjuaji wa madini yetu kwa lengo la kuyaongezea thamani; kusaidia wachimbaji wadogo kupata masoko, mikopo, teknolojia na maarifa ya kisasa katika uchimbaji madini; kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na takwimu; kuendeleza utafutaji wa madini; na kuvutia uwekezaji kwenye sekta ya madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kazi Zilizopangwa Kutekelezwa, katika sekta ya madini kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: kuboresha mfumo wa uwezeshaji wa uchimbaji mdogo wa madini; kuanza kutumia Mfumo Mpya wa Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini (*Mining Cadastral Information Management System (MCIMS*) kwa lengo la kuboresha utoaji na usimamizi wa leseni na kupunguza mwingiliano katika utoaji leseni za viwanja; kuimarisha ukusanyaji maduhuli katika sekta ya madini; na kuimarisha usimamizi wa sekta ya madini kwa kuongeza kasi ya ukaguzi wa shughuli za madini migodini na maduka ya biashara za madini.

Mheshimiwa Spika, Mradi Maalumu wa Kuboresha Utoaji na Usimamizi wa Leseni za Madini, Sekta ya Madini inakabiliwa na migogoro mingi kuhusu umiliki wa maeneo ya uchimbaji na mahusiano mabaya kati ya wachimbaji madini. Kwa upande mmoja, migogoro inatokana na teknolojia duni katika mfumo mzima wa utoaji leseni. Wizara kwa kushirikiana na *Nordic Development Fund (NDF)* ilianzisha mradi maalumu,

*MCIMS,* ambao upo katika hatua za mwisho ili uanze kufanya kazi. Katika mfumo huo, ofisi 22 zilizoko mikoani zitaunganishwa na kuwa na mawasiliano ya moja kwa moja yatakayoiwezesha kila ofisi kujua hatua zilizofikiwa na ofisi nyingine katika utoaji wa leseni za madini na malipo ya kodi zinazostahili kwa kila leseni. Aidha, marekebisho ya baadhi ya vipengele vya Sheria ya Madini yanahitajika ili iendane na mfumo mpya wa *MCIMS.* Serikali inaandaa mapendekezo ya kuboresha vipengele vya sheria husika.

Mheshimiwa Spika, Uendelezaji wa Wachimbaji Wadogo, kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005, maelekezo ya Mheshimiwa Rais na taarifa zilizopo zinazoonesha kuwa kuna wachimbaji wadogo takriban milioni moja, Serikali iliunda Kamati ya Kuandaa Mikakati ya Kuendeleza Wachimbaji Wadogo.

Mheshimiwa Spika, mikakati iliyoandaliwa ni pamoja na: kufanikisha upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya wachimbaji wadogo; kutoa mafunzo ya ufundi na ujasiriamali; kuhamasisha na kueneza matumizi ya teknolojia bora na salama; kuanzisha mfuko maalumu wa masharti nafuu; kutathmini kijiolojia maeneo ya wachimbaji wadogo; kushawishi wachimbaji wakubwa watoe huduma za kitaalamu katika maeneo ya uchimbaji mdogo. Kuzielimisha taasisi za fedha juu ya fursa za kiuchumi katika uchimbaji mdogo, uongezaji thamani na biashara ya madini, kuhamasisha uanzishwaji wa vikundi vya ushirika katika maeneo ya uchimbaji, kujenga mazingira bora ili kushamirisha uongezaji wa thamani ya madini hapa nchini, kuweka mfumo wa masoko ya kushindanisha wanunuzi katika maeneo ya uchimbaji, kuboresha usimamizi na uratibu wa shughuli za uchimbaji mdogo kwa kuziimarisha ofisi za madini na kushughulikia kwa kasi mpya masuala mtambuka katika maeneo ya uchimbaji yanayojumuisha UKIMWI, jinsia, ajira ya watoto na huduma za jamii.

Aidha, Serikali itawasiliana na wawekezaji na makampuni yanayoweza kuingia katika makubaliano na wachimbaji wadogo ili kuwawezesha kupata huduma za mikopo katika shughuli zao za uchimbaji na masoko ya kuuza madini.

Mheshimiwa Spika, Kupitia upya Mikataba ya Madini, kufuatia hotuba ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa Mei Mosi, 2006, Kamati Maalumu imeundwa kudurusu mikataba ya madini kwa lengo la kuona uwezekano wa sekta ya madini kuongeza mchango wake kwenye Pato la Taifa. Kamati hiyo imekwishawasilisha taarifa ya awali ambayo kwa sasa inafanyiwa kazi. Aidha, wakati zoezi la kudurusu mikataba hiyo likiendelea, Wizara ilisimamisha utoaji leseni kwa wawekezaji wakubwa waliotaka kuanza uzalishaji katika migodi mipya. Mojawapo ya mafanikio yaliyofikiwa katika zoezi la upitiaji upya wa mikataba ya madini ni pamoja na makubaliano yaliyofikiwa baina ya Serikali na Kampuni za uchimbaji mkubwa wa madini kukubali kuanza kulipa Dola za Marekani 200,000 kwa mwaka kwa halmashauri husika kama kodi. Malipo ya kodi hiyo kwa halmashauri yamekuwa hayafanyiki kwa kipindi kirefu kutokana na utata wa kisheria uliosababishwa na kupingana kwa mikataba ya madini na Sheria ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1982.

Majadiliano yaliyofikiwa baina ya Serikali ya Awamu ya Nne na kampuni hizo yalifanikisha kupatikana kwa ufumbuzi wa utata wa kisheria uliokuwepo na hivyo

kuruhusu malipo hayo ya kodi kwa halmashauri husika kuanza kufanyika. Hadi sasa, Kampuni ya *Barrick Gold Tanzania* inayomiliki migodi ya Bulyanhulu, Tulawaka na *North Mara* imelipa jumla ya shilingi 734,999,999 kwa wilaya za Kahama, Biharamulo na Tarime.

Kampuni ya *Resolute* itaanza kulipa kodi kwa Halmashauri ya Nzega kuanzia mwezi Septemba mwaka huu. Aidha, mashauriano kati ya Serikali na kampuni za madini yameanza katika zoezi la kudurusu mikataba ya madini kwa lengo la kuhakikisha kuwa Taifa linanufaika ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Kuboresha Sera na Sheria ya Madini,baada ya Kamati ya Kudurusu Sera ya Madini kuwasilisha taarifa yake Serikalini, Wizara imebainisha maeneo muhimu na vipengele vya sera na sheria vitakayofanyiwa marekebisho. Vipengele hivyo ni pamoja na: kuongeza mchango wa sekta ya madini katika uchumi wa Taifa kwa kuongeza fungamanisho (*linkage*) la sekta ya madini na sekta nyingine; taratibu za uwekezaji na vivutio kwa utafutaji na uchimbaji madini na ushiriki wa Serikali kimkakati katika umiliki wa migodi. Aidha, Sheria ya Usonara itafanyiwa marekebisho kwa kufuta na kuongeza baadhi ya vipengele ili kukidhi mahitaji ya sasa ya kukuza uongezaji wa thamani ya madini.

Mheshimiwa Spika, Uongezaji Thamani ya Madini,katika kutekeleza uamuzi wa Serikali wa kuhakikisha kwamba madini yanayozalishwa nchini yanaongezewa thamani badala ya kuyauza nje ya nchi yakiwa ghafi na kwa lengo la kuongeza mapato na ajira, Wizara imekamilisha ufungaji wa mitambo ya uchongaji na usanifu wa vito na mawe huko Arusha (*Arusha Gemstone Carving Centre*). Wizara inatathmini mfumo bora wa uendeshaji wa kituo hicho utakaohakikisha kinaendeshwa kibiashara na kuweza kuwasaidia wachimbaji wadogo kuongeza thamani ya madini yao. Aidha, kituo hicho kitaendelea kutoa mafunzo ya awali ya uchongaji na usanifu kwa wadau.

Ukaguzi wa Gharama za Uwekezaji na Uendeshaji Migodi, kazi hii inafanywa na kampuni ya *Alex Stewart (Assayers) Government Business Corporation (ASAGBC).* Ukaguzi wa uzalishaji na usafirishaji katika migodi mikubwa ya dhahabu hapa nchini, unaendelea. Aidha, ukaguzi wa gharama za uwekezaji kwenye migodi ya Geita: *Golden Pride* na *North Mara* umekamilika na ukaguzi katika mgodi wa Bulyanhulu, unaendelea. Taarifa kamilifu za ukaguzi kutoka *ASAGBC* kujua hali halisi ya uendeshaji wa migodi hiyo zinafanyiwa kazi. Mwaka 2006/2007, Wizara itahakikisha inajenga uwezo wa wataalamu wake kufanya kazi hiyo ya ukaguzi baada ya mkataba wa *ASAGBC* kumalizika mwaka 2007 na hivyo kutokuwa na ulazima wa kuendelea na mkataba huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha zaidi kiutendaji, Wizara imeunda Kamati ya Wataalamu kupitia na kuchambua taarifa za Mkaguzi ili kubaini upungufu uliopo kwenye udhibiti na usimamizi wa uzalishaji na usafirishaji wa madini ya dhahabu hapa nchini. Kamati itatoa mapendekezo yatakayofanyiwa kazi ili kuboresha usimamizi na udhibiti wa madini ya dhahabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ukaguzi wa Migodi, katika mwaka 2006/2007 Idara ya Madini itafanya ukaguzi katika maeneo yote ya uchimbaji yakijumuisha mikoa ya Lindi, Mtwara, Dar es Salaam, Tanga, Pwani na Morogoro.

Mheshimiwa Spika, G*eological Survey of Tanzania,* Ramani na Takwimu za Kijiolojia, katika kipindi cha mwaka 2006/2007, *GST* itaendelea kuboresha shughuli zake za ugani; kufanya utafiti wa madini katika maeneo mbalimbali hapa nchini; kukusanya, kuchambua na kutunza takwimu na sampuli za miamba; na kuboresha mazingira ya wafanyakazi wake kwa kuwapatia vitendea kazi na mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Aidha, ili kuboresha utunzaji wa sampuli za miamba, fedha zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa *core shed*. Pia, kazi ya uchoraji na uchapishaji wa ramani za Kahama na Biharamulo na *block maps* za Mpanda na Chunya itafanyika katika kipindi hiki. Aidha, *GST* itaendelea na shughuli za kukusanya takwimu za matetemeko ya ardhi na inategemea kufunga vituo vipya vitatu katika maeneo ya Kibaya, Kondoa na Manyoni. Vituo hivyo vitapatikana kwa msaada wa *International Programme for Physical Sciences (IPPS)* ya Sweden.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Madini, Chuo cha Madini kilichoko katika Manispaa ya Dodoma, eneo la Mbwanga kinatoa mafunzo ya muda mfupi na mrefu ya cheti na stashahada katika fani za jiolojia, uhandisi wa migodi, utafutaji na uchenjuaji madini kwa wataalamu wa migodi mikubwa na midogo iliyopo nchini na wa Wizara ili kukuza uwezo wao katika kusimamia ukuaji wa sekta ya madini. Katika kipindi cha mwaka 2006/2007, Chuo kinatarajia kupata wakufunzi 17 kukiongezea uwezo wa ufundishaji na kuongezewa miundombinu ya maktaba, maabara, nyumba za kuishi, zahanati na viwanja vya michezo.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha *Tansort,* Kitengo cha *Tanzania Government Diamond Sorting Organization* (*TANSORT*) kitaendelea na majukumu yake ya kuthamini almasi inayoingizwa Uingereza kutoka Mwadui na kukubaliana bei ya almasi na mnunuzi (*Diamond Trading Company*, kampuni tanzu ya *Debeers).* Aidha, katika kuimarisha utendaji kazi wa Kitengo hicho, Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kuwapeleka mafunzoni watumishi wa Kitengo na kugharimia pango la ofisi. Mchakato wa kukihamishia Kitengo hiki nchini unaendelea ili kiweze kukagua na kuthibitisha usahihi wa almasi hapa hapa nchini kama inavyofanyika katika nchi za Botswana na Namibia.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*), Shirika la Madini la Taifa linawekeza katika utafutaji wa madini na linatoa huduma za uchorongaji wa miamba kwa malipo. Kwa sasa *STAMICO* ina leseni saba za utafutaji wa madini ya dhahabu; leseni mbili za *platinum group metals* na leseni moja ya madini ya *fluorite* iliyo katika mkoa wa Mbeya. Katika eneo la Itetemia, karibu na Bulyanhulu, linalomilikiwa kwa ubia kati ya *STAMICO* na *Tancan Mining Company Limited* ya Canada, uchorongaji unafanyika ili kuthibitisha mashapo zaidi. Hadi sasa, mashapo yanayovuka wakia 900,000 za dhahabu yamegunduliwa. Utafiti katika maeneo mengine ya dhahabu unaendelea. Kwa upande wa uchorongaji miamba, *STAMICO* inazo mashine nne za zamani na iko katika hatua ya kununua mashine moja mpya ili kujiimarisha katika utoaji

wa huduma hiyo. Aidha, *STAMICO* inaendelea na uchorongaji wa miamba eneo la *Tanga Cement*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ajira na Maendeleo ya Watumishi, katika mwaka 2006/2007 Wizara inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 105 wa kada mbalimbali. Aidha, ili kuwaendeleza watumishi wake, katika bajeti hii Wizara imetenga fedha kwa ajili ya mafunzo kwa kila idara/ kitengo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2006/2007, Mpango wa Kimkakati wa Wizara wa mwaka 2003- 2006 utafanyiwa durusu ili kuweza kukidhi mahitaji na mabadiliko yaliyojitokeza katika utekelezaji wa mkakati wa awali. Kukamilika kwa zoezi hilo kutaiwezesha Wizara kutekeleza ipasavyo mfumo wa *OPRAS* kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na kuongeza ufanisi. Aidha, Wizara itaendelea kutoa semina na kuandaa mipango ya kuwapatia mahitaji muhimu kiafya waliojitokeza kuwa ni waathirika wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Ushirikiano wa Kimataifa, katika mwaka 2005/2006 sekta za nishati na madini zilinufaika kwa misaada ya wafadhili mbalimbali. Hivyo, kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani kwa serikali za nchi na mashirika ya kimataifa kwa ushirikiano na misaada waliyotoa kwa ajili ya kuendeleza sekta hizo. Naomba nizishukuru serikali za Australia, Canada, China, Denmark, Finland, Hispania, India, Japan, Marekani, Norway, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza na Ujerumani. Aidha, natoa shukrani kwa Umoja wa Mataifa na Umoja wa Nchi za Ulaya, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Rasilimali ya Ulaya, *DANIDA, GEF, FMO, IAEA, IMF, JICA, KfW, NDF, NORAD, ORET, Sida, UNDP, UNESCO, UNIDO* na *USAID.*

Mheshimiwa Spika, Shukrani, nichukue nafasi hii kuwashukuru viongozi wenzangu ambao kwa pamoja tumeweza kufanikisha shughuli za Wizara kwa mwaka 2005/2006. Kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Lawrence Masha, Naibu Waziri, kwa msaada wake mkubwa alionipa katika kusimamia shughuli za Wizara. Napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu, Bwana Arthur Mwakapugi, Wakuu wa Idara na Vitengo, viongozi wa mashirika yaliyo chini ya Wizara, zinazosimamiwa na Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika yake.

Mheshimiwa Spika, Majumuisho, sasa naliomba Bunge lako likubali na kuidhinisha mapendekezo ya Bajeti ya sh. 465,202,173,000 kwa ajili ya Matumizi ya Wizara na Mashirika yake kwa mwaka 2006/2007. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Bajeti ya Maendeleo ni sh. 432,544,995,000 ambazo kati yake sh. 224,981,995,000 ni fedha za hapa na sh. 207,563,000,000 ni fedha za nje; na

(ii) Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ni sh. 32,657,178,000 ambapo sh. 1,675,726,000 ni kwa ajili ya mishahara *(PE)* na sh. 30,981,452,000 ni matumizi mengineyo *(OC). (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE.WILLIAM H. SHELLUKINDO – MWENYEKITI WA UWEKEZAJI NA BIASHARA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa shukrani zangu kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kutoa Taarifa, kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka 2006/2007 kwa mujibu wa Kanuni Na.81(1) ya Kanuni za Bunge Toleo la Mwaka 2004.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kusema kwamba naiunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge ambao ni Wajumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara *(INTRA)* ambao ndio waliochambua Bajeti ya Wizara hii kwa umakini na ufanisi mkubwa nao ni:-

Mhe. Dr. Harrison G. Mwakyembe, Mjumbe na Makamu Mwenyekiti wa Kamati. Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Mohammed A. Chomboh, Mheshimiwa Yahya K. Issa, Mheshimiwa Asha M. Jecha, Mheshimiwa Siraju J. Kaboyonga, Mheshimiwa Mwajuma H. Khamis, Mheshimiwa Vuai A. Khamis, Mheshimiwa Fuya G. Kimbita, Mheshimiwa Eng. Stella M. Manyanya, Mheshimiwa Fatma A. Mikidadi, Mheshimiwa Herbert J. Mntangi na Mheshimiwa Mohammed H. Mnyaa.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Luhanga Joelson Mpina, Mheshimiwa Mbaruk K. Mwandoro, Mheshimiwa Saverina Silvanus Mwijage, Mheshimiwa Dr. Lucy S. Nkya, Mheshimiwa Christopher O. Ole–Sendeka, Mheshimiwa Lucy F. Owenya, Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mheshimiwa Haji J. Sereweji, Mheshimiwa Ahmed Mabkhut Shabiby, Mheshimiwa Mohammed S. Sinani, Mheshimiwa Abdallah Salum Sumry na Mheshimiwa William H. Shellukindo, ambaye ndiye Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ilivyo kawaida wakati wa kuchambua Bajeti ya Wizara, Kamati ilizingatia vipengele vifuatavyo kuhusu Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini.

1.1 Dira/Mwelekeo wa Wizara kuhusu kushughulikia masuala ya nishati na madini nchini.
1.2 Majukumu ya Wizara.
1.3 Taarifa kuhusu utekelezaji wa malengo ya Wizara katika Mwaka 2005/2006.
1.4 Taarifa ya Utekelezaji wa ushauri wa Kamati wakati wa kuchambua Bajeti ya Mwaka 2005/06.

1.5 Maelezo kuhusu Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na fedha za Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka 2005/2006.

1.6 Maelezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, Kupitia utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Ushauri Uliotolewa Wakati wa Mchakato wa Bajeti ya 2005/2006, tunapenda kuipongeza Wizara kwa hatua mbalimbali ilizozifikia katika kutekeleza ushauri wa Kamati. Pia Wizara imejitahidi kwa kiasi kikubwa kutekeleza malengo ya shughuli ilizojipangia katika hali ya ufinyu wa Bajeti na hasa kutokana na kupunguzwa kwa fedha zilizotengwa ili kukabili janga la njaa na ukame uliosababisha kupungua kwa maji kwenye mabwawa ya kuzalisha umeme. Hapa napenda niipongeze Serikali kuhusu yafuatayo:-

Shirika la Taifa la Mafuta ya Petroli *(TPDC),* Kamati imefurahishwa na juhudi zinazofanywa na Serikali kwa kutambua upeo na uwezo wa *TPDC* na kuutumia kama ilivyoonekana katika Bajeti ya mwaka huu 2006/2007 ambapo Wizara imetengewa Sh.6.2 bilioni chini ya Bajeti ya Maendeleo Fungu 58, Kifungu 3001-3115*,(Petroleum Sub sector Development).* Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha hizo kadri zinavyohitajika; kwa sababu miaka iliyopita fedha zilitengwa lakini hazikutolewa.

- Mheshimiwa Spika, Kutokana na kupanda kwa bei za nishati ya mafuta katika soko la dunia na mahitaji ya nishati mbadala nchini, Shirika litatakiwa kufanya shughuli nyingi na kwa uharaka. Shughuli za Utafiti ni muhimu sana kwa vile kuna kila dalili za kuwepo Mafuta na Gesi Asilia kwa wingi nchini, hivyo ni vizuri kuongeza kasi ya utafiti na kuipatia *TPDC* uwezo wa kushirikiana na wawekezaji katika sekta hii.

- Mheshimiwa Spika**,** uamuzi wa Serikali wa kuipatia *TPDC* nafasi ya ghorofa saba katika sehemu mojawapo ya Jengo la Mafuta *(Mafuta House),* pamoja na sehemu ya chini kwa ajili ya kuhifadhia sampuli za miamba na takwimu za utafiti wa mafuta, ni hatua nzuri ya kuthamini shughuli za Shirika hilo. Ni matumaini ya Kamati kwamba *TPDC* katika jengo husika haitaonekana kuwa ni mpangaji bali mmiliki mwenza wa jengo hilo na hivyo halitatozwa kodi ya pango la sehemu hiyo.

- Mheshimiwa Spika, Ili *TPDC* isionekane kama inafadhiliwa na pia Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC),* wapewe hisa zinazolingana na thamani ya gharama walizotumia katika ujenzi wa Jengo hilo *(Mafuta House).* Vilevil, ili kujua gharama halisi za Shirika la Hifadhi ya Taifa *(NSSF)* katika kukamilisha jengo hilo, ifanyike tathmini na mtaalam wa majengo ili kuondoa viwingu vya mashaka.

- Mheshimiwa Spika, pia Kamati imefurahishwa na uamuzi wa Serikali wa kulipa Shirika la Mafuta uwezo ili kuongeza idadi ya hisa zake kwa niaba ya Serikali katika

Kampuni ya *Pan-African Energy.* Uamuzi huo utaiwezesha Serikali kupata gawio kubwa kutokana na faida inayopatikana kutokana na mauzo ya Gesi Asilia kuliko ilivyo sasa. Vilevile Kamati inashauri kwamba, uamuzi huo utekelezwe mapema kwa kuipatia *TPDC* kiasi cha fedha zitokanazo na mauzo ya Gesi Asilia ya Songo Songo kwa ajili ya ushiriki wake katika utafiti na kuendeleza mradi wa Gesi.

Mheshimiwa Spika, Mitambo ya *Independent Power Tanzania Ltd* (*IPTL*)

- Wakati wa Hotuba ya Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2005/2006, Kamati iliishauri Serikali iharakishe mazungumzo yatakayowezesha Serikali kununua mitambo ya kuzalisha umeme ya *IPTL* Tegeta ili Taifa liweze kuepukana na gharama za malipo ya uwezo wa kuzalisha umeme (*capacity charges).*Kamati inaendelea kushauri kwamba Serikali inunue mitambo hiyo.

- Aidha, kuhusu uamuzi wa Serikali kuibadili mitambo hiyo ili iweze kutumia Gesi Asilia badala ya Mafuta Mazito, Kamati inaupongeza uamuzi huo kwa vile utapunguza gharama za uzalishaji. Na ni matumaini ya Kamati kwamba baada ya kubadilisha mfumo huo wa mafuta mazito na kutumia Gesi, gharama za umeme nazo zitapungua maana gesi ina gharama ndogo.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO),* Kamati ilifurahishwa na azma ya Wizara kuliendeleza na kulipa uwezo zaidi Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* ili liweze kumudu majukumu yake kwa ufanisi zaidi na hasa jukumu la kuwaendeleza wachimbaji wadogo wa madini. Kamati inashauri kwamba suala la kuwaendeleza na kuwawezesha wachimbaji wadogo wa madini lipewe kipaumbele maalumu katika mwaka wa fedha 2006/07 ili kuwapunguzia adha wahangaikaji hao.

Mheshimiwa Spika, Maombi ya Fedha, ili kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2006/2007 Wizara ya Nishati na Madini inaomba fedha chini ya Fungu 58 kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 4.1 | Fedha za Matumizi ya Kawaida - | Tsh. | 32,657,178,000/= |
| 4.2 | Matumizi yaMaendeleo | Tsh. | 432,544,995,000/= |
| | Jumla - | Tsh. | **465,202,173,000/=** |

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati, baada ya kupitia na kuchambua kwa makini Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini na kuridhika na kazi zitakazotekelezwa katika kipindi kijacho, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Kupatikana kwa Gesi Asilia Tanzania ni ukombozi mwingine ambao Mwenyezi Mungu ametujalia. Kamati inapenda kulipongeza Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* ambalo lilikamilisha utafiti na kugundua kuwa nchini ipo Gesi Asilia na ambayo inaweza kuvunwa kibiashara.

Kinachotakiwa sasa ni kuhakikisha kwamba utafiti unaongezewa nguvu kwa lengo la kugundua Gesi Asilia nyingine zaidi. Kazi hii iende sambamba na kuifikisha gesi hiyo mapema kule inakohitajika. Kwa sasa wenye viwanda wengi hapa nchini, Jijini

Dar-es-Salaam na nje ya Dar-es-Salaam na hata nje ya nchi wangependa kutumia nishati ya gesi katika michakato yao ya uzalishaji. *(Makofi)*

- Mheshimiwa Spika, kwa upande mwingine, Serikali ifanye maamuzi ya haraka kuhusu matumizi zaidi ya rasilimali hiyo kama vile matumizi ya kupikia majumbani na kuendeshea magari. Aidha, matumizi hayo ya gesi asilia yaende sambamba na kutoa elimu ya kutosha kwa wananchi ili waweze kukubali kutumia gesi badala ya mkaa. Pia, Serikali iweke vivutio maalum kwa wawekezaji katika shughuli za gesi na vifaa vinavyotumia gesi.

- Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Gesi ya *Mnazi Bay* kufanyike utafiti wa uwezekano wa gesi hiyo kutumika pia katika uzalishaji wa mbolea za chumvichumvi na bidhaa za nyingine.

- Mheshimiwa Spika, yapo malalamiko toka kwa baadhi ya Wateja kuwa bei ya gesi hiyo iko juu kwa vile upangaji bei zake umeegemea kwenye bei za mafuta katika soko la dunia. Ni vema bei hizo zikaangaliwa ili ziwe kivutio kwa watumiaji bila kuwepo hasara kwa wawekezaji husika. *(Makofi)*

- Mheshimiwa Spika, Utafutaji wa Mafuta Nchini, Tafiti za mafuta hapa nchini zina historia ya miaka mingi na hatua kadhaa za mafaniko zimefikiwa. Kutokana na kupanda kwa bei za mafuta katika soko la dunia, nchi nyingi sasa zinafanya tafiti nyingi za Nishati hiyo. Hapa nchini, maeneo kadhaa yametengwa kwa ajili ya tafiti hizo.

- Hata hivyo, kumekuwa na tatizo la kufanya tafiti katika eneo liitwalo "*Block* 12"; eneo hilo linaanzia kusini na linaendelea hadi sehemu ya Pwani ya Kisiwa cha Pemba. Kampuni iliyokodishiwa eneo hilo tangu mwaka 1998 hadi sasa haijaruhusiwa kuendelea na utafiti kwa sababu Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar haijaidhinisha zoezi hilo liendelee kutokana na rai ya kutaka kuangalia upya makubaliano ya ushirikiano kati yake na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa masuala ya mafuta. *(Makofi)*
- Mheshimiwa Spika, linalojitokeza sasa ni kana kwamba Serikali inataka kuvunja mkataba na Kampuni iliyopata kibali cha kufanya utafiti na hivyo kuna uwezekano wa Kampuni hiyo kuishitaki Serikali kwa kuvunja mkataba huo. Kwa hiyo, Kamati inaendelea kutoa rai kwamba rasilimali ya Mafuta ni mali ya Watanzania wote, hivyo Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zikae pamoja ili kupata muafaka kuhusu suala hilo na kuwezesha utafiti kuanza bila kuchelewa zaidi.

- Mheshimiwa Spika, Kamati inazipongeza Serikali zote mbili kwa hatua za mwanzo zinazochukuliwa zenye lengo la kuondoa utata uliopo.

Mheshimiwa Spika, Upungufu wa maji katika Mitambo ya Umeme inayoendeshwa na Maji, Kamati katika ziara zake ilifahamishwa baadhi ya sababu zinazosababisha tatizo kubwa katika mitambo ya umeme wa maji. Sababu hizo ni

pamoja na ukame, wananchi kutumia maji kwa ajili ya kumwagilia mashamba yao pamoja na kuchunga mifugo kwenye vyanzo vya maji.

Kamati inashauri kwamba hatua madhubuti zichukuliwe ili mtiririko wa maji kuelekea kwenye mitambo ya umeme usiingiliwe pamoja na kuchukua hatua kali kwa wale wote watakaokiuka maagizo ya Serikali ya kuhifadhi na kutunza vyanzo vya maji.

- Mheshimiwa Spika, Usambazaji wa Umeme. Wizara hii ina jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba watumiaji wa umeme wanaupata ipasavyo na kwa gharama nafuu. Tunaipongeza Serikali kwa mpango wake wenye malengo kwamba ifikapo mwaka 2025 Makao Makuu yote ya Wilaya yatakuwa yamefikishiwa umeme na hatimaye Makao Makuu yote ya majimbo ya Uchaguzi.

- Mheshimiwa Spika, Waziri wa Nishati na Madini katika mpango wa maendeleo, ameorodhesha Miji kadhaa ambayo itapatiwa umeme mwaka huu. Vile vile ameonyesha matumaini kwamba Miji mingine 18 itaombewa fedha kupitia mpango wa *Millenium Challenge Account* unaofadhiliwa na Marekani. Kamati inapongeza juhudi hizo maana kuna matumaini kwamba mpango huo utasaidia kupunguza muda wa kufikiwa kwa lengo lililowekwa. *(Makofi)*
- Mheshimiwa Spika, Miradi ya Chuma Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma, ahadi ya Waziri ya kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya haitafanikiwa kama hakutakuwa na ongezeko la uzalishaji wa umeme. Kamati inasikitika kwamba Uwekezaji katika miradi ya Chuma Liganga na Mkaa wa Mawe Mchuchuma umekuwa kitendawili. Kwa bahati nzuri, Kamati hii ilipata fursa ya kutembelea maeneo hayo mwezi Aprili, 2006.

- Mheshimiwa Spika, Kamati inatambua na kuamini kwamba miradi hii miwili haiwezi kuanza kwa pamoja kwani Mradi wa Chuma Liganga unategemea kwanza kuwepo kwa umeme wa kutosha kiasi cha megawati (*megawatts*) 200. Hivyo basi, Kamati inashauri kwamba mradi wa Mchuchuma uanze kwanza ili uweze kuzalisha umeme. Inasemakana kuwa mradi huo una uwezo wa kuzalisha hadi megawati (*Megawatts*) 1,600 za umeme, lakini utaanza kwa kuzalisha megawati (*Megawatts*) 200 na kuendelea kwa awamu.

- Mheshimiwa Spika, Kamati pia imeelezwa kuwa Makampuni kadhaa ya ndani na nje ya nchi yameomba kuwekeza katika mradi huo. Kamati inapenda kusisitiza kwamba mchakato wa kuipata Kampuni mahiri kwa ajili hiyo uanze mara moja na kwamba mwekezaji huyo apatikane kwa kuzingatia yafuatayo:-

(a) Uwazi katika kuitisha na kuteua mwekezaji/wawekezaji.

(b) Uwezo wa kitaalam wa kuweza kuchimba na kuchenjua madini aina mbalimbali yatakayochimbwa;

(c) Uwezo kifedha; na

(d) Uzoefu katika kufanya shughuli hizo.

- Mheshimiwa Spika, Kamati ingependa ieleweke kwamba madini yaliyoko Liganga si chuma pekee bali pia yapo madini mengine kama *Venadium* na *Titenium* ambayo thamani yake ni kubwa duniani kuliko hata hicho chuma. *(Makofi)*
- Mheshimiwa Spika, kutozingatia vigezo hivyo na kukubali mashinikizo mbalimbali Taifa linaweza kupata hasara kubwa. Ni vizuri ikaeleweka kwamba rasilimali hizo si za wananchi wa Ludewa peke yao, bali ni rasilimali ya Watanzania wote. Kuna miradi mikubwa ya uchimbaji madini Wilaya za Kahama, Geita, Shinyanga, Simanjiro, Tarime n.k. Wananchi wa Wilaya hizi wamekubali ukweli huu, kwa nini wengine wafanye tofauti. Hata hivyo Kamati, kama ilivyo kwa wananchi wa Ludewa, inapenda uwekezaji katika mradi huo uanze haraka iwezekanavyo, ili Taifa kwa jumla linufaike wakiwemo wananchi wa Wilaya ya Ludewa.

- Kutumia Malighafi Mbalimbali Katika Kuzalisha Umeme Kwa miaka mingi iliyopita kulikuwa na umeme uliozalishwa kwa mafuta na baadaye ukapatikana umeme unaozalishwa kwa maji, hali iliyowezesha kuuweka umeme huo kwenye Mtandao wa Kitaifa (*National Grid).*

- Mheshimiwa Spika, umeme sasa unazalishwa kwa kutumia Gesi Asilia pamoja na Makaa ya Mawe. Pia kuna vyanzo vingine kama vile magome ya miwati Wilayani Njombe na kadhalika. Kila kimoja cha vyanzo hivi kikitumiwa pekee hakitatosheleza mahitaji ya Umeme nchini. Hivyo basi, Kamati inaishauri Serikali iangalie utaratibu wa kutumia vyanzo vyote kwa pamoja ili kukidhi mahitaji.

- Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Kampuni ya Mkaa wa Mawe ya Kiwira (Kiwira *Coal Mines Ltd*.) kwa kuwa tayari imeanza kuzalisha umeme wa ziada na kuliuzia Shirika la Umeme Tanzania (*TANESCO*). Kampuni hiyo imepanga kuendelea kuzalisha megawati *(Megawatts) 200* za Umeme katika awamu ya kwanza na baadaye kufikia megawati (*Megawatts*) *400*

.• Mheshimiwa Spika, Machimbo ya *TANZANITE* Mererani. Kamati hii ilipata fursa ya kutembelea Machimbo ya Vito vya *TANZANITE* huko Mererani, Wilayani Simanjiro. Katika ziara hiyo, Kamati ilitembelea Wachimbaji wadogo pamoja na wachimbaji wakubwa wa Kampuni ya *TANZANITE ONE.* Katika mikutano tuliyofanya na wachimbaji hao kila upande kati ya pande hizi mbili ulikuwa unalaumu upande mwingine. Pia kulikuwa na malalamiko ya wachimbaji kukutana kati ya vitalu na vitalu *(blocks)* huko ardhini. Wachimbaji wenyewe wanaita kutobozana.

Mheshimiwa Spika, ili kumaliza matatizo hayo, Kamati inashauri ifuatavyo:-

Kwa ujumla, maeneo wanayogawiwa wachimbaji wadogo ni madogo mno na ndio sababu ya kukutana huko ardhini. Maeneo hayo yana ukubwa wa mita 50 x 50. Hivyo, Kamati inashauri kwamba wachimbaji hao washawishiwe kujiunga katika makundi ili kwa pamoja waweze kugawiwa maeneo ya kutosha na kuondoa tatizo la kutobozana.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa nchi nyingi duniani hazitoi Leseni za kuchimba vito kwa wageni, kwa mfano nchi za India, Malawi na kadhalika Kamati inashauri kwamba Serikali isitoe leseni nyingine mpya wala kuongezewa maeneo kwa Makammpuni ya kigeni na pia kwa Makampuni makubwa yaliyopo pindi leseni zao zikiisha.

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uchimbaji Madini ya Mwaka 1998 inayomtaka Mchimbaji wa madini aende chini moja kwa moja *vertically,* sheria hiyo iangaliwe upya kwa sababu ya madini ya *TANZANITE* hayafuati mteremko wa moja kwa moja yanaweza kwenda mshazari *(Horizontally)* . Kwa hiyo kuweka kanuni ya kwenda moja kwa moja chini inaleta matatizo ya kutobozana. Pamoja na kuongezwa kwa ukubwa wa vitalu, madini ya *TANZANITE* yatengenezewe kanuni zake tofauti na madini mengine kwa ajili ya hali ya uchimbaji wake.

Mheshimiwa Spika, Kuwepo kwa Nyenzo za Kisasa. Kwa kawaida wachimbaji wadogo wanakwenda chini ya ardhi hadi Mita 200 tu. Huo ndio uwezo wao kutokana na nyenzo duni walizonazo.Kamati inapendekeza kwamba Serikali iangalie uwezekano wa kuwawezesha Wachimbaji hao wapate vifaa vitakavyowawezesha wachimbe kwenda chini zaidi na hivyo kupunguza uwezekano wa kutobozana. Mheshimiwa Spika, Kuwepo na Soko la vito karibu na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro *(KIA).*

Mheshimiwa Spika, kutokuwepo na soko la uhakika kwa vito vya *TANZANITE* kumeifanya nchi ipoteze fedha nyingi kutokana na wanunuzi kununua vito hivyo kwa njia za magendo. Aidha, Wauzaji na wanunuzi wanakumbana na matatizo mengi yakiwemo ya kudhulumiana. Kutokana na hali hiyo, Kamati inapendekeza kuwepo Soko la Vito (vito vya aina zote) na lijengwe karibu na Mererani yanapopatikana madini ya *Tanzanite* ambapo wanunuzi na wauzaji wanaweza wakakutana. Eneo la Mererani liko karibu na Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro. Na kwa mnunuzi wa nje wataruka na ndege hadi *KIA* na kununua vito kwa karibu na kuingia kwenye ndege bila hofu ya kunyang'anywa fedha au vito. Pamoja na faida hiyo ya kuwa na soko la vito, hali hiyo pia itahamasisha shughuli nyingine za uchumi zinazoendana na madini ya vito.

Mheshimiwa Spika, Kumekuwepo na malalamiko mengi kwamba baadhi ya watumiaji umeme hawalipii matumizi yao ya umeme kwa vile hawajulikani na *TANESCO.* Kamati inashauri Serikali kuiagiza, napenda kurudia Kamti inashauri Serikali kuiagiza *TANESCO* ianze kufunga mita za Luku kwenye miradi mipya yote. Hali hii

itaimarisha ukusanyaji mapato ya *TANESCO* na kupunguza hasara kwa Shirika na kuwezesha Serikali kupata gawio.

Mheshimiwa Spika, kuna tatizo la mikataba katika Sekta ya Madini na Nishati. Kwa muda mrefu sasa kumekuwa na utata na viwingu vya mashaka kuhusu mikataba mbalimbali iliyoingiwa kati ya Serikali na Wawekezaji katika sekta ya nishati na pia ya madini kwamba baadhi ya vipengele vya mikataba hiyo vinakataza mikataba hiyo baada ya kusainiwa isionwe na mtu mwingine yeyote isipokuwa wale waliyoisaini. Hali hii inaleta wasiwasi kuhusu namna mikataba hii ilivyoingiwa, Kamati yangu inatambua kuwa Wizara au Serikali imeunda Tume kufuatilia mikataba mbalimbali iliyosainiwa chini ya Wizara kama ule wa *IPTL* ambao umekuwa ni mzigo mkubwa sana kwa Taifa. Tume hiyo ya Serikali na ni ya kiutendaji wa Serikali na itakuwa na muono wa Kiserikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati yangu inatoa Pendekezo kwa Bunge lako tukufu kwamba, kwa vile mikataba hii inahusu Taasisi za umma, Kamati hii inapendekeza kuwa Bunge lako Tukufu, kwa mujibu wa Kanuni Na.104 ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2004 liunde Kamati Teule ili iweze kupitia mikataba mbalimbali, nitarudia Kwa vile Mikataba hii inahusu Taasis za Umma Kamati inapendekeza kuwa Bunge lako Tukufu likubali kwa mujibu wa Kanuni Namba 104 ya Kanuni za Toleo la 2004 iunde Kamati Teule ili iweze kupitia mikataba mbalimbali ya Sekta ya Nishati na Madini yenye utata na kutoa Taarifa Bungeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Nchi inapata matatizo mengi ya mafuta wakati mwingine yanapungua hayaonekani na limeshatokea hivyo, kwa hiyo Kamati yangu inashauri kwama kuwepo na utaratibu wa kuweka akiba ya mafuta yaani *Strategic Oil/ Fuel Reserves* ili kuweza kukabili matatizo yoyote ambayo yanaweza kujitokeza wakati wowote na kwa ushauri ni kwamba yanaweza kuwepo ya muda wa siku kama 45, nchi nyingine zinafanya hivyo na kwa kuwa kwenye chakula tunafanya hivyo basi na kwenye mafuta nako tufanye hivyo vinginevyo nchi inaweza kukwama kama hakuna utaratibu mzuri wa kujikinga. Kamati inatambua kuwa Serikali inafanya kila jitihada ili kuhakikisha kuwa bei za mafuta nchini zinapungua. Kwa mfano katika Bajeti ya mwaka huu 2006/2007, Serikali imeondoa kodi ya ongezeko la thamani *VAT* lakini maamuzi hayo hayajashusha bei hizo. Hali hii inatokana kwa sababu waagizaji wakubwa wa mafuta kuungana katika kupanga bei wanafanya *cartels*. Inawezekanaje wakati mwingine bei za mafuta Dodoma zinakuwa za chini kuliko za Dar es Salaam?

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kuwa Serikali iendelee kutoa leseni kwa waagizaji wengi wa mafuta ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu waagizaji hao kutumia maghala ya kuhifadhia mafuta ya kukodi. Pia kwa vile tayari sheria ya kuanzisha Mamlaka ya Kusimamia Shughuli za Nishati na Madini *EWURA* ipo, ni vema Mamlaka hiyo ianze kazi haraka ili usimamizi wa sheria na matumizi ya maji na mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa uweze kufanyika na kudhibiti ili bei za mafuta zisipande holela.

Mheshimiwa Spika, Taifa limepata matatizo mengi ya Nishati kwa hiyo Kamati yangy baada ya kutafakari suala hili inapenda kupendekeza kwamba Serikali iandae

Mpango wa miaka mitano wa nishati na mpango huo uwasilishwe hapa Bungeni ili maandalizi ya kuupatia fedha katika bajeti ya mwaka 2007/2008 ufanyike.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho. Namalizia kwa kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa Taarifa ya Kamati yangu kuhusu Mapendekezo ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka wa fedha 2006/2007. Napenda kumshukuru sana na kwa dhati kabisa Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Lawrence Masha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini na Katibu Mkuu, Ndugu Arthur Mwakapugi na Watumishi wote pamoja na Watendaji Wakuu wa Mashirika kwa ushirikiano mkubwa waliyoipatia Kamati yangu katika mchakato mzima wa kushughulikia bajeti ya Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia natoa shukrani zangu kwa niaba ya wenzangu kwa Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S.L. Foka, kwa kuiwezesha Kamati kufanya kazi zake bila matatizo yoyote. Napenda vilevile kuwashukuru Ndugu Aggrey N. Nzowa na Ndugu Abdallah Hancha, kwa kuhudumia vizuri Kamati na kuhakikisha kwamba inatoa taarifa yake kwa wakati unaotakiwa. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha na Naunga Mkono Hoja. (*Makofi*)

**MHE. MOHAMED HABIB J. MNYAA - MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia kusimama hapa leo hii kwa niaba ya Kambi ya Upinzani kutoa maoni yetu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu Na. 43(5)(b)(c) na 81(1) Toleo la 2004 kuhusiana na shughuli za Wizara ya Nishati na Madini katika bajeti ya mwaka wa fedha 2006/2007.

Mheshimiwa Spika, kwa vile nimewasilisha mezani ninaomba inukuliwe ilivyo katika *Hansard* hata kama sitaweza kumaliza kuisoma yote.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe Mheshimiwa Samwel Sitta kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni na mchango wetu upande wa Upinzani. Naomba pia uniruhusu niwapongeze wananchi wa jimbo langu la Mkanyageni walionichagua mimi kwa moyo mkunjufu na kusababisha mimi kuwepo hapa leo hii. Aidha natoa shukrani zangu kwa chama changu cha Wananchi (*CUF*), na viongozi wake wote kwa ushirikiano walionipatia katika mchakato mzima wa uchaguzi. Bila kuwasahau viongozi wangu wa Kambi ya Upinzani hapa Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid na Mheshimiwa Dr. Wilbrod P. Slaa kwa uongozi wao madhubuti na kuifanya Kambi ifanye kazi yake kulingana na Kanuni zetu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dira ya Wizara ya Nishati na Madini kuwa kitovu cha uhamasishaji, uwezeshaji wa upatikanaji wa nishati ya uhakika na ya gharama nafuu na matumizi endelevu ya raslimali za nishati na madini ili kuchangia kwa kiwango kikubwa katika pato la taifa ifikapo mwaka 2025 basi na hilo nalipongeza lakini ilikuwa iwe tangu miaka 25 iliyopita siyo ijayo kwa maana itakuwa Tanzania tumechelewa mno.

Mheshimiwa Spika, dira hii ni nzuri na inayoleta matumaini kwa Watanzania wote lakini nasikitika sana kwamba inakwenda kinyume na baadhi ya malengo na madhumuni ya Wizara hii pale inapokubali kufungiana mikataba inayokandamiza na kuleta kero kubwa kwa wananchi katika sekta zote za Nishati na Madini.(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Haya yanadhihirika katika Mikataba ya Serikali na *IPTL, SONGAS, TANZANITE ONE, NET GROUP SOLUTION* na kadhalika. Pia masuala ya kupanda bei kwa gharama za mafuta, udhalilishaji wa wachimbaji madini wazalendo wadogo wadogo, bei kubwa za umeme zinazoongezeka mara kwa mara na kadhalika ni mambo ambayo yanaichafua dira hii nzuri. Ni miaka arobaini na mbili iliyopita ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania lakini ni 10% tu ya Watanzania watanzania wanaotumia nishati ya umeme ukilinganisha na majirani wetu, mfano tuliopakana nao Malawi tayari wameshasambaza umeme 55% ya miji yake tayari inayo umeme wa gridi ya Taifa, Zambia wanategemea 2010 watakuwa wameshasambaza 50% ya watu wake watakuwa na umeme, Kenya 15% ya nchi hiyo ina umeme wa gridi ya Taifa. Aidha, kwa ulinganisho wa gharama za umeme *(US$/kWh)* wa viwandani inaonyesha kuwa Malawi ni 0.04, Kenya ni 0.097, Uganda ni 0.06 lakini Tanzania ni 0.108 ambayo ni juu kuliko wote. Kambi ya Upinzani inashangaa kama kweli Serikali ina nia ya kumpunguzia mwananchi wa kawaida makali ya maisha na ni kwa nini haikupunguza 20% ya *VAT* katika gharama za umeme wa majumbani ambayo moja kwa moja ingelimnufaisha mwananchi huyo, na isitoshe mwnanchi huyo huyo hulipa VAT katika manunuzi mengine yanayotokana na bidhaa za viwandani. Halikadhalika nishati ya mafuta ya *petrol* na *diesel* tukilinganisha kwa nchi zenye bandari kama vile Kenya na Mozambique kwa kutumia *Common Currency* ya *Dollar* ni kama ifuatavyo:-

*Tanzania petrol $ 1.158/LT diesel $ 1.112/L Kenya petrol $ 1.077/LT diesel $ 1.05/LT Mozambique petrol $ 1.07/LT* na *diesel ni $ 1.00/LT.* Tanzania bado iko juu kwa bei hizo. Mheshimiwa Spika, baadhi ya nchi kama Uganda na Malawi, hazina bandari kama Tanzania lakini bado wana unafuu wa nishati ya umeme kuliko sisi. Malengo ya Wizara hii katika bajeti ni maneno matamu, ahadi nzuri lakini vitendo vyake ni kuwabebesha Watanzania mzigo mkubwa wa ongezeko la bei yamafuta na umeme kutokana na idadi ya kodi kubwa azinazotozwa na Serikali kwa bidhaa hizo. Utafiti wetu unaonyesha kuwa tangu bajeti ilipotangazwa bei ya Petroli haikushuka kabisa katika vituo vingine au imeshuka kidogo tu. Mathalan, Dar es Salaam Petrol ilikuwa inauzwakati ya shilingi 1350/= hadi 1480 na sasa ni 1350 ile ile na 1400 yaani imeshuka kwa shilingi 40 hadi 45 tu. Moshi nayo *Petrol* ilikuwa 1380 hadi 1480 na sasa ni kati ya 1380 ile ile na 1420 yaani imeshuka kwa wastani wa shilingi 45 tu katika vituo vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa wastani bei imeshuka kwa 4.3% tu wakati punguzo la kodi ya VAT ilikuwa asilimia 20. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa tamko sasa katika Bunge hili, unafuu uliotangazwa na Waziri wa Fedha wakati wa wa bajeti umepotelea wapi? Mbona bei za mafuta hazijapungua hadi sasa? Kuna faida gani kupunguza kodi kama haimpatii nafuu mwananchi wa kawaida. Serikali inachukua pia

hatua gani kuhakikisha kuwa bei hizo hazitapanda baada ya Bunge hili kama ilivyokuwa kawaida huko nyuma? Tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kujalia Tanzania kuwa na vyanzo vingi sana vya nishati ukilinganisha na nchi nyingine za Bara hili la Afrika. Lakini kwa bahati mbaya usemi wa Kiswahili kwamba "penye miti hapana wajenzi" unajionyesha hapa, kutokana na udhaifu wa mipangoyetu ukusanyaji mdogo wa maduhuli na utatuzi wa haraka wa matatizo yanayotukabilikatika sekta ya madini na umeme.

Mabadiliko ya hali ya hewa yanayosababisha joto kali duniani kwa sababu ya kuliwa kwa *Ozone layer* yameripotiwa si chini ya miaka 18 iliyopita, ambayo madhara yake ni upungufu mkubwa wa maji duniani ikiwemo Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo Watanzania kukosa nishati ya umeme au kuongezeka kwa bei ya bidhaa hiyo kwa kisingizio cha maji au ongezeko la gharama ya mafuta ni kutokuwatendea haki kwani inaonekana kama nchi inafanya kazi kienyeji haina mipango ya ku- *absorb shock* pindi matukio ambayo hayakuwepo yanapoweza kujitokeza wakati wowote. Japokuwa nchi ilitakiwa iweke tahadhari kwa miaka 18 iliyopita kukabiliana na matatizo yanayoweza kusababishwa na *Ozone Layer Depletion.* *(Makofi)*

Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge hili Tukufu inachukua hatua gani za makusudi za muda mfupi na mrefu kuhakikisha kuwa Taifa letu halitaathirika na majanga haya makubwa?

Mheshimiwa Spika, historia ya Makaa ya Mawe ya Mchuchuma na Katewaka ni ndefu yaligunduliwa tokea mwaka 1896. Tafiti nyingi zilifanywa hapo kabla ya uhuru na baada ya uhuru kama ile ya 1977 / 1978 iliyofanywa na Shirika la Ujerumani *GTZ* vilevile Juni 1995 pia *CMPD* ya India 1977 na mwishowe upembuzi yakinifu uliofanywa na Shirika la Taifa la Maendeleo (*NDC*) umethibitisha kuwepo kwa zaidi ya tani nusu bilioni za makaa ya mawe zenye uwezo wa kuzalisha umeme wa kutosha na wa uhakika kwa mahitaji ya Tanzania nzima na hata kukidhi mahitaji ya majirani kwa zaidi ya miaka 100 ijayo. Kinachoshangaza hapa ni kuwa Baraza la Mawaziri liliidhinisha utekelezaji wa mradi huu hapo tarehe 20 Aprili, 2004 na Baraza hilo miezi miwili baadaye yaani 16 Juni, 2004 ikaiagiza *TANESCO* kutekeleza mradi huo mara moja, hatua kwa hatua kwa kuanzia kuzalisha umeme wa *MW 200* kati ya mwaka 2007/2008. Wizara ya Nishati na Madini nayo ikatoa kibali kwa *NDC* kuunadi umeme wa Mchuchuma kwa nchi jirani za Kenya na Uganda na kwa watumiaji wakubwa kama vile migodi ya dhahabu kwa lengo la kujiridhisha kuwepo kwa soko la umeme wa ziada.

Mheshimiwa Spika, pamoja na *NDC* kuendelea na utekelezaji wa mradi huu kwa kasi inayostahili kama ilivyokuwa imeagizwa na Serikali kwa kufuata kusudio la makubaliano yaani *Agreement of Intent* lililokuwa tayari limetiwa saini kati ya Serikali na kundi la Wawekezaji likiongozwa na *Siemens Ltd*, tena kwa kutambulishwa hapa Bungeni na Mheshihimiwa Spika hapa hapa Dodoma. Baada ya hapo ndipo kilipoingia kizungumkuti yaani *misunderstanding* na mradi ukakosa msukumo wa Wizara ya Nishati na Madini na *TANESCO* yenye dhamana kisheria ya umeme. Haya ndiyo matunda tuliyovuna ya *NET GROUP SOLUTION* iliyopewa madaraka ya uongozi wa *TANESCO*

ambayo ilipigiwa makelele na kukataliwa na Watanzania walio wengi hata wafanyakazi wa *TANESCO* wenyewe lakini Serikali ililazimisha na kupeleka Polisi ili kuiweka *NET GROUP* kwa nguvu kinyume na maoni ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, siyo hayo tu baada ya *TANESCO* ikiongozwa na Wizara ya Nishati na Madini kuufuta mradi huu kwenye mpango wa Taifa wa umeme yaani *National Power System Master Plan* ndiyo kitendo kilichosababisha katika Kikao cha tarehe 21 Novemba, 2005 cha *Southern African Power Pool Priority Projects for Investors Consideration and Funding* usiingizwe kabisa na kwa maana hiyo kuwakatisha tamaa baadhi ya wawekezaji wakubwa wa mwanzo kama vile *SIEMENS LTD, CINERGY GLOBAL POWER INCORPORATION* ya Marekani, *ANGLO POERATION LTD na DUKE ENGINEERING AND SERVICES (PTY) LTD* za Afrika ya Kusini. Sababu kubwa ni kuwa Kamati hiyo ya *SADC* iligundua kuwa Mradi wa Mchuchuma umepangiwa kutekelezwa 2022 na siyo mara moja kama miradi ya *SADC* inavyotaka.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali itoe maelezo ya kina kuhusu suala la mradi wa Mchuchuma na Liganga kwa sababu katika maelezo yake na vyombo vya Habari pamoja na maelezo ya hivi karibuni alipotembelea Ludewa Mheshimiwa Waziri alisema Serikali iko tayari sasa kuanza mradi huu wa makaa ya mawe tu ndiyo utatuletea umeme wa uhakika. Mambo yafuatayo ni lazima yapate majibu ya kina:-

(a) Je, *TANESCO* chini ya *NET GROUP Solution* ilipata wapi mamlaka ya kubadilisha maamuzi ya Baraza la Mawaziri kama ilivyofanya kwa Barua yake ya tarehe 29 Machi, 2005, iliyopelekwa kwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini?

(b) Katibu wa Wizara ambaye ndiyo mtunzaji Mkuu wa Maamuzi alikaa kimya bila kujibu wala kuchukua hatua yoyote kuhusu hatua hiyo ya *NET GROUP Solution*? Ni kitu gani kitatuzuia kufikiri kuwa una wingu la rushwa hapa? *(Makofi)*

(c) Kwa vile hadi leo hii, mradi huu haujaingizwa kwenye *Power System Master Plan*, Matamshi ya Waziri yanashikilia nguzo gani, ni matashi yake binafsi au ni mpango wa Serikali na kama ni mpango wa Serikali uko wapi mpango huo? Au tuelewe basi kuwa ni matamshi ya kisiasa tu ya kuwafurahisha Watanzania? *(Makofi)*

(d) Kwa kuwa, Kambi ya Upinzani inataarifa isiyo rasmi kuwa kuna taarifa ya au Ripoti ya Kamati ya Serikali ya Uchambuzi wa Mradi wa Makaa ya Mawe wa Mchuchuma na Mradi wa Chuma wa Liganda ya Mwezi Mei, 2006, na hatimaye kuna taarifa pia kuwa Kamati hiyo hiyo ikalazimishwa na serikali kuandaa taarifa nyingine mwezi Julai 2006.

Kambi ya Upinzani na mimi kwa mamlaka yangu ya Waziri Kivuli wa Wizara hii, ninaitaka Serikali kwa mujibu wa kifungu cha 10 cha Sheria ya Bunge Namba 3 ya mwaka 1988 pamoja na marekebisho yake, yaani *Parliamentary Immunities, Powers and Privileges Act*, iwasilishe katika Bunge hili Taarifa hizo zote mbili pamoja na

makubaliano yaani *Memorandum* zote walizotiliana saini na Serikali kuhusu Uendelezaji wa Mradi huu. Kampuni hizo, pamoja na zilizotajwa hapo juu ni *MM Integrated Steel Mills Limited* ya Tanzania, *Athi River Steel Plant Limited* ya Kenya, *BSG Resources* ya Israel na *Sub Sahara Resources NL* ya Austraria ambao kwa taarifa tuliyonayo hawa *Sub Sahara* wamekubali kuipa Serikali asilimi 30 bila Serikali kulipia hisa yoyote.

(e) Kwa kuwa Kampuni ya *MMI* inayomilikiwa na *Subash Patel* na Ramanlal Patel katika kushawishi kupewa eneo la ekari zaidi ya 1,400 ya eneo hilo lenye Mkaa wa Mawe na Chuma, na katika ushawishi huo, tarehe 20/08/2005 walitoa msaada wa Mabati 500, kofia za mabati na kilo 100 za misumari kwa mradi wa shule ya Sekondari ya Amani, Liganga, na tani 97 za seruji, tani 23.5 za nondo kwa jaili ya ujenzi wa daraja la mto Katewaka, na mapema mwezi Machi 2006 Kampuni hiyohiyo imelipia Ziara ya Madiwani saba na Maafisa watatu wa Ludewa kuona shughuli za Kampuni hiyo.

Ahadi hizi nazo zimeelezwa rasmi kwa maandishi kwa Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Uwezeshaji iliyofanyika Dodoma tarehe 31 Machi, 2006. Ni kweli *Lobbying* inakubalika katika taratibu za Kibunge, lakini *Lobbying* inapoungana na utoaji wa vizawadi kwa vile Takrima imeishafutwa na Mahakama hii siyo Rushwa? Na je, Taasis ya *PCB* nayo inafanya nini? Kampuni hiyo hiyo imetoa ahadi kukarabati mradi wa maji wa Nkomang'ombe na Kimelembe. Je Serikali haioni kuwa wakati Kampuni hii imeomba kukodishiwa au kumilikishwa maeneo hayo, Zawadi hizo zinaashiria Wingu zito na Nene la Rushwa? Kambi ya Upinzani inahitaji Kauli ya Kina ya Serikali kuhusu tabia hii inayooenda kinyume na mkakati wa Taifa wa Kuzuia Rushwa wa mwaka 2000/2005? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Hata katika bajeti hii ya 2006/2007 mimi sijaona kifungu chochote cha bajeti hii kinachotaja waziwazi kuhusiana na kuanza kwa mradi huu katika bajet angalau kwa hatua za mwanzoni kama ilivyo kwenye Kitabu cha Nne cha Bajeti. Wataalamu wetu wa *NDC* wamebainisha katika upembuzi yakinifu kwamba mradi huu wa Mchuchuma utagharimu *USD.* millioni 612 wastani wa Billioni 700 fedha ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika,Waziri ametamka kuwa Mradi huu unaanza mwaka huu, Kambi ya Upinzani inataka kujua unaanza na Fedha zipi wakati haupo kwenye Bajeti? Wakati tunaandamwa na Mgawo wa Umeme wananchi wanahitaji maelezo ya uhakika kuhusu ahadi na matamko haya ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Suala la Nishati ya *Uranium* halijatajwa kabisa katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Aidha suala la nishati hii pia halimo katika taarifa ya Waziri wa Nishati na Madini kuhusu kazi na majukumu ya Wizara, Taasisi na Mashirika yake, bali liko katika Wizara ya Sayansi na Teknolojia pia madini haya hayakutajwa katika ilani ya uchaguzi ya Chama Tawala ya 2005 lakini limetajwa waziwazi katika ilani ya uchaguzi ya Vyama vingine vya Upinzani, ilani ambazo kwa kiwango kikubwa sasa hivi inatekelezwa na Serikali ya awamu ya nne hasa katika mapendekezo yake kuhusu nishati na madini. Pamoja na mazingira yake yenye utata na

kuhodhiwa na mataifa makubwa, kutawaliwa na sheria ngumu za Kimataifa lakini Serikali inalifahamu vilivyo na ndio maana Bunge lako tukufu likatunga sheria ya *ATOMIC ENERGY ACT* NAMBA 7 YA 2003.

Mheshimiwa Spika, Hivi sasa ipo haja kubwa ya kufanya mabadiliko katika sheria hii ili Nishati hii ya Uranium pia iweze kushughulikiwa kiutendaji na Wizara kubakia kitaaluma kwenye Wizara iliopo hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa iko haja kubwa ya kufanya mabadiliko hasa ya kiuchumi wakati umefika sasa na wala tusisubiri kesho kufanya upembuzi yakinifu wa Nishati hii ya *Uranium* iliyo ghali kuliko zote duniani ili hata kama haitatumika kwa kuzalisha umeme kwa miaka ya hivi karibuni lakini ni chanzo kikubwa cha kuikomboa Tanzania kiuchumi kwa umuhimu wake kitaifa na kimataifa kwa matumizi ya kawaida ya Nishati.

Mheshimiwa Spika, Kati ya mwaka 1978 – 1982, Kampuni moja ya Kijerumani iitwayo *Uranerzbergbau Gmbh (Uranez)* ilifanya utafiti kwa njia ya *reconnaissance exploration* na kugundua kwamba kuna hazina kubwa ya madini haya ya *Uranium* katika eneo la *Mkuju River Basin* Kusini mwa Tanzania na Makutupora hapa Dodoma. Pia ilithibitisha kwamba Tanzania ni moja kati ya maeneo yenye matumaini makubwa duniani ya upatikanaji wa madini ya *Uranium* kwa gharama ya chini, yaani (*Low exploration cost*) ambazo zimekadiriwa kuwa ni *US$ 4* kwa $km^2$ ukilinganisha na *US$ 16*/$km^2$ huko Afrika Magharibi, au *US$ 244*/$km^2$ *huko USA*.

Meshimiwa Spika, Jeolojia ya *Mkuju River basin* kusini mwa Tanzania inaonyesha kuwepo kwa Uranium katika ukanda wa sq.Km 2000 ndani ya Luwegu na Bonde la Ruhuhu. Ukanda wa Luwegu peke yake unakadiriwa kuwa na asilimia 30 (30%) ya machimbo yote ya Uranium yanayojulikana kwa Bara zima la Afrika. Hivi sasa majirani zetu Malawi tayari wanafanya upembuzi yakinifu katika eneo la KAYELEKERA chini ya Kampuni ya *Paladin Resources* ya Australia. Vivyo hivyo jirani zetu wa Uganda tayari wamegundua *Uranium* katika maeneo yenye ukubwa wa sq km 35000, kwa mujibu wa taarifa toka huko wanatarajia kuanza upembuzi yakinifu mwezi oktoba mwaka huu kwa ajili ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Spika, Katika suali Na 74 alilouliza Mheshimiwa Mbunge wa Kiwani, kuhusiana na madini haya ya *Uranium* Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati alitoa majibu mazuri lakini mwishowe alisema naomba kunukuu: "Mheshimiwa Spika, pamoja na teknolojia ya nyuklia kuwa ngumu lakini suala kubwa linalo kwamisha matumizi ya nishati hiyo hapa nchini ni kuwa matumizi yetu ya umeme bado ni ndogo. Uzoefu unaonyesha kuwa mtambo mmoja wa kuzalisha umeme kwa kutumia nyuklia unaanzia na uwezo wa uzalishaji wa *MW 500*. Kwa nchi kama Tanzania kuweka mtambo wa namna hiyo kiutaalam haishauriwi kwani matumizi yetu bado ni madogo kwani mahitaji yetu (*peak demand*) hayaja fikia *MW1000."* mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Spika, Kwa maana ya jibu hilo tunamtaka Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini atufafanulie yafuatayo kwa kina:-

(a) Ongezeko la *MW* ngapi tunatarajia kulipata kwa miradi yote 20 ya usambazaji umeme Vijijini iliyomo katika bajeti hii ya 2006/2007.

(b) Ongezeko la mahitaji ya umeme kwa nchi nzima kwa mwaka (*growth rate*).

(c) Madhumuni hasa ya miradi ya *Interconnector* ya Zambia –Tanzania – Kenya.

(d)Je, lengo ni kununua umeme tu kutoka kwa hao majirani zetu ? Hivi kweli kwa nchi ambayo wananchi wanaotumia umeme ni chini ya asilimia 10 tu, na kwa nchi ambayo hata sasa kabla hatujatoka kwenye mvua kuna mgawo wa Umeme Serikali iko makini kweli kutoa jibu kama lilivyotolewa hapo Juu? Hii ni kuwatania na kuwadhihaki Watanzania. *(Makofi)*

Hivyo Kambi ya Upinzani inashauri nishati hii ishughulikiwe haraka ili kuleta mabadiliko ya kweli ya kiuchumi kwa faida ya Taifa hili kama Dira ya Wizara ya Nishati na Madini inavyojieleza.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu vyanzo vingine vya nishati kama vile *biogas*, mabaki ya mkonge, miwa, maganda ya korosho na vyenginevyo vinafaa kutiliwa maanani katika Sekta binafsi za wazalendo katika Mikoa au Wilaya zinazohusika zenye malighafi (*raw material*) husika ili viongezee nguvu kwenye grid ya Taifa na kuna uwezekano mkubwa wa kupunguza gharama za umeme huko vijijini.

Ni jukumu la wizara kutekeleza na kuhamasisha usajili wa wakala wa umeme *Rural Energy Agency* na kwa yale makampuni ya kizalendo sio kupewa mamlaka ya ujenzi wa laini za umeme vijijini tu, bali hata kuzalisha umeme wa vyanzo hivyo tulivyovitaja. Mheshimiwa Spika, Nchi yetu imebarikiwa kuwa na utajiri mkubwa wa madini mengi sana, kama vile Dhahabu, Almasi, Chuma, Magadi *(Soda Ash),* Makaa ya mawe, Tanzanite pamoja na jamii nyingine ya vito madini haya hayajatumiwa na kukuza uchumi wa nchi yetu na kuboresha hali ya maisha ya wananchi wa Taifa hili.

Mheshimiwa Spika, Tuchukue mfano halisi uliotajwa katika bajeti ya Wizara hii ambayo imetaja vyanzo vya Maduhuli ikiwa pamoja na mrahaba kutokana na mauzo ya madini, mauzo ya gesi, ada za maombi ya leseni, kodi ya mwaka ya viwanja vya madini *(mineral rent)* na kadhalika.Kifungu 2001 Jumla ya kifungu hiki ni TSh.32.902.502.000/=. Sasa ukichukua *budget* ya nchi nzima ya Wizara ya Fedha mapato ya ndani. Serikali inalenga kukusanya TSh. Trilioni 2. billioni 460 millioni 995 (Shilling 2,460.995 millions). Kifungu 2001 Jumla ya kifungu hiki ni TSh.32.902.502.000/-. l *rent)* na kadhalika. Kifungu 2001 Jumla ya kifungu hiki ni TSh.32.902.502.000/-.

Sasa ukichukua *budget* ya nchi nzima ya Wizara ya Fedha mapato ya ndani . Serikali inalenga kukusanya TSh. Trilioni 2. billioni 460 millioni 995 (Shilling 2,460.995 millions). Hii maana yake ni asilimia 1.33 (1.33%).

Mheshimiwa Spika, katika *Budget* ya Wizara hii ya Nishati na Madini ya 2005/2006 ukurasa wa 9, Mheshimiwa Waziri alisema na nukuu: "Mchango wa sekta ya madini kwenye pato la Taifa umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 1.4 mwaka 1995 hadi kufikia asilimia 3.2 mwaka 2004." mwisho wa kunukuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa inakuwaje katika makadirio ya ukusanyaji wa mapato katika sekta hii ya madini 2006/2007 iwe 1.33%. Je, hilo ongezeko la asilimia 25.4 linatoka wapi? Mheshimiwa Spika hapa tunamuomba Waziri na wataalam wake watupe maelezo na ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Spika, Sasa jionee mwenyewe wakati pato la Tanzania katika Sekta ya madini ni 1.33%, katika nchi za Kusini na Magharibi ya Afrika mapato yatokanayo na madini ni asilimia 30 (30%). Hii ni kasoro kubwa sana inayosababishwa kwa kiwango kikubwa na sera mbovu za madini na mikataba yenye utata inayoleta migogoro, uhasama, udhalilishaji wa wachimbaji wadogo wadogo wenyeji hasa katika maeneo yenye wawekezaji wakubwa wa kigeni. (*Makofi*)

Katika hotuba ya bajeti ya 2003/2004. Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini wa wakati huo walitamka kuhusu azma ya Serikali kuwapa sauti wenyeji na hivyo kudhibiti vitendo viovu vya wageni vinavyoweza kulisababisha Taifa letu kukosa mapato.

Mheshimiwa Spik,a ikumbukwe kwamba mwaka huo 2003, Tanzania ilikuwa ni ya 3 kwa Afrika nzima inayozalisha Dhahabu kwa wingi. Katika migodi ya Buhemba, Bulyankulu, Geita, *Golden Pride, North* Mara walikuwa wakizalisha *kg 50,200* kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Eneo jingine lenye matatizo makubwa ni madini ya Vito kama vile *suphier, Quartz, Ruby*, *Tanzanite* na mengineyo. Madini haya ya vito yamekuwa yakichimbwa na wawekezaji wadogo wenyeji kwa miaka mingi iliyopita ambayo yanapatikana sehemu mbali mbali hapa Tanzania.Katika madini haya ya vito *TANZANITE* ni kati ya madini yenye thamani kubwa ambayo yamegundulika hapa nchini mnamo mwaka 1966 na kuanza kuchimbwa rasmi mwaka 1968. *(Makofi)*

Kwa zaidi ya miaka 30, wachimbaji hawa wadogo kama *TAMIDA* ndio waliosababisha jina la *Tanzanite* kuwa kubwa duniani na kukuza Soko la *Tanzanite* duniani.

Pamoja na jitihada hizo, wenyeji hawa hawajapata msukumo na uwezeshwaji rasmi kutoka Serikalini ya kuwaendeleza zaidi, bali ni matatizo yanayowakabili pamoja na udhalilishaji hasa baada ya Serikali kuwaingiza Wawekezaji wakubwa kama vile *Tanzanite One*, kama ilivyotokea mara kwa mara pale Mererani.

Mheshimiwa Spika, katika mfumo wa nchi nyingi duniani, ikiwa aina ya madini inapatikana katika nchi moja tu, basi madini hayo huchimbwa na wenyeji tu, sio wageni. Kwa mfano, kule Sri Lanka *(Ratna Pura)* madini ya vito aina ya *Gauda Supphire*

huchimbwa na wazawa tu (Wa-Sri Lanka). Kule Thailand *(Chantabury)* madini adimu ya Vito aina ya *Pink Ruby* huchimbwa na wenyeji tu (Wa-thailand). Pia, majirani zetu Malawi, madini ya aina ya *Blue Chalsedony* au *Blue Agate* yanachimbwa na wenyeji tu. Lakini hapa Tanzania tumeingiza Wawekezaji wa kigeni katika madini ya vito kama vile *Tanzanite* ambayo yanapatikana Tanzania pekee. Watanzania hupelekewa mbwa kama ilivyo pale Mererani na hata kuondolewa kwa risasi za moto katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la ajabu zaidi, pamoja na kuingia Kampuni hii ya *Tanzanite One,* Wawekezaji wamejisajili katika *Stock Market* ya *London* badala ya Soko la Hisa hapa kwetu na hivyo kulikosesha mapato Taifa letu na kuwakosesha Watanzania fursa ya kujiongezea kipato kwa kujinunulia hisa hizo na hata kuwa wamiliki wa rasilimali za nchi yao? Kambi ya Upinzani inahitaji majibu sahihi kuhusu hali hii ya ajabu na ya kufedhehesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mbinu za *promotion* zinazofanywa na *Tanzanite One,* sio kuwadhalilisha na kuwakosesha kuuza *Dealers* wadogo wadogo wa Kitanzania katika Soko la Kimataifa na kuhodhi *(Monopoly)* Soko lote la Kimataifa na kwamba *Tanzanite* bora na ya halali ni ile tu yenye nembo ya *Tanzanite One*.

Mheshimiwa Spika, ikumbukwe kwamba, mbinu kama hii ndiyo inayotumiwa na Kampuni ya *De Beers* ya Afrika Kusini kuhodhi *(Monopoly)* soko lote la madini ya almasi duniani. Athari kubwa ya mbinu hii ni kwamba, itafika wakati wachimbaji na wafanyabiashara wadogo, wenyeji kama vile *TAMIDA,* watashindwa kabisa kuuza *Tanzanite* kwenye Soko la Kimataifa na hivyo kulazimika kuwauzia *Tanzanite One* tu, kwa bei watakayo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi nyingi duniani zinapinga ukiritimba huu wa biashara ikiwemo Marekani kama ilivyodhihirika hivi karibuni kwenye kesi ya Kampuni kubwa ya *Microsoft* inayohodhi Soko la *Software* za Kompyuta na pia *De Beers* wenyewe kule Marekani.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya Mererani yamekuwa ni makubwa na madhara makubwa tayari yameshatokea na hivyo ni wajibu wa Wizara ya Nishati na Madini kutoyafumbia macho na yanafahamika kama ilivyo ripoti ya Mstaafu General Mboma ambayo hadi hivi leo haijatolewa hadharani. Matatizo haya yanapunguza kwa kiasi kikubwa pato la Taifa katika biashara ya madini. Kwa mfano, kodi lukuki zilizowekwa zinasababisha biashara ya ulanguzi mkubwa wa madini kwa wafanyabiashara wengi kutokujisajili kihalali na kulikoseshea pato Taifa letu.

(1) Mfano: Kenya wana leseni moja tu *Dealers* ya K.Sh.10,000/- na kodi nyingine ni *Corporate Tax 20%.*

(2) Sri-Lanka wana leseni moja tu ya *Dealers* na Serikali imeondoa kodi zote katika biashara ya madini. Lakini

Tanzania kuna kodi zaidi ya tano ikiwemo *Corporate Tax* ya 30%.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri mambo yafuatayo yazingatiwe na Wizara ya Nishati na Madini ili kuboresha Sekta hii ya Madini na kuliongezea pato Taifa na wakati huo huo kuwaenzi wenyeji kwa lengo lile lile la MKUKUTA.

Mambo yenyewe ni kama yafuatayo:-

(a) Malipo ya leseni ya wanunuzi wa madini *(Dealers)* toka nchi za nje yaongezwe hadi *USD 10,000.= (Tsh.12.5m)* na kiwango cha dhamana *(Bond)* kiwe *USD 300,000 = ( TSh.375 million).* Hii itasaidia kuwapunguza wageni uchwara wenye nia ya kuendeleza utoroshwaji wa madini nchi za nje.

(b) Kwamba, Serikali lazima iwe na hisa *(shares)* zisizopungua asilimia 30, kwa sababu ardhi iwe ya mgodi au vinginevyo, ndiyo raslimali ya Tanzania na thamani yake ni kubwa mbali ya mali iliyomo humo ndani ya ardhi yenyewe. Mwekezaji yeye analeta mashine na utaalam *(Technical know how),* inakuaje leo Tanzania ikose hisa katika baadhi ya miradi ya madini inayomilikiwa na wageni?

(c) Vyombo mbali mbali vya Serikali viwe karibu, kufuatilia kwa karibu ulipaji wa kodi mbalimbali zinazowahusu wageni wanaoishi nchini kwa kufanya biashara za madini kama vile *Directors Fees, Housing Levy* na *P.A.Y.E.* Njia zote za ukwepaji zidhibitiwe kikamilifu.

(d) Leseni zote za madini na Usonara zitolewe na chombo kimoja tu kwa lengo la kuleta ufanisi.

(e) Serikali itumie pia wataalam wa Idara ya Madini ambao ndio wenye ujuzi na uzoefu wa kufunga mizigo inayosafirishwa nje badala ya kuwatumia Maafisa wa Forodha peke yao na wawepo katika zoezi la kufunga vifurushi.

(f) Kuanzishwe viwanda vya ukataji na kusanifu madini vinavyoendeshwa na Watanzania na kuongeza ajira kwa vijana. *NSSF/PPF/Local Government Pension Fund* vitumike kuwekeza kwa majengo ya namna hiyo.

(h) Pasiruhusiwe Kampuni nyingine ya nje zaidi ya hiyo iliyopo hivi sasa kuwekeza katika madini ya vito.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka takriban mitano Serikali kupitia Jeshi la Wananchi imekuwa ikendesha shughuli za ununuaji wa dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo wadogo. Serikali imekuwa ikilieleza Bunge hili kuwa moja ya majukumu ya Kampuni hiyo ni kuwanunulia vifaa mbali mbali wachimbaji wadogo wadogo waliopo katika maeneo ya Geita na Musoma. Aidha ni pamoja na kukiendeleza kitengo cha Jeshi kinachoshughulikia uundaji wa magari cha Nyumbu.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Ulinzi ya mwaka 2003/2004 alilieleza Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Juni, 2003 dhahabu iliyochimbwa ilikuwa wakia 32,265.3 na iliingiza *USD 10,646,291.* Kati ya fedha hizo, *USD 9,075,625* zilitumika kufidia gharama za uchimbaji, usafirishaji na uuzaji wa dhahabu na *USD 1,570,665* zilitumiwa na Meremeta kwa kulipia sehemu ya mkopo wa redio zinazotumiwa na JWTZ pamoja na vifaa vya huduma kwa wchimbaji. Katika hotuba ya Waziri ya mwaka 2004/2005, Meremeta ilianza kuchimba madini na tangu Januari, 2004 hadi Juni, 2004 Kampuni ilizalisha jumla ya *4,400 kg* za dhahabu zenye thamani ya *USD 46,270,300,* ambazo *USD 35,702,000* zikiwa ni gharama za uzalishaji na uendeshaji na Kampuni ikalipa gharama za mrahaba *USD 1,340,000.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miezi sita, Kampuni ilizalisha 4,400 *kg* za dhahabu. Ni mategemeo yetu hivi sasa imekwisha zalisha tani nyingi sana. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ilieleze Bunge lako Tukufu baada ya Meremeta kuwa kitengo cha Jeshi na kuwa Kampuni iliyoundwa na kusajiliwa kisheria na Msajili wa Makampuni. Mambo yafuatayo tunaomba yafuatiliwe.

(1) Kampuni hiyo hivi sasa inamilikiwa na nani?

(2) Kama Serikali ina hisa ni kiasi gani cha hisa hizo?

(3) Ni akina nani ni wajumbe wa Bodi ya Kampuni hiyo?

(4) Je, ni kiasi gani cha fedha zimetolewa kwa vikundi mbali mbali vinavyojihusisha na uchimbaji mdogomgodo na majina ya vikundi hivyo na kiasi gani cha fedha kwa kila kikundi?

(5) Je ni kiasi gani cha fedha kimepatiwa kikosi cha Nyumbu katika kukiimarisha kati ya 2004 hadi 30 Juni, 2006?

(6) Kwa Kutumia Kifungu cha 10 cha Sheria Na. 3 ya Mwaka 1988 na kwa mamlaka yangu kama Waziri Kivuli, ninaomba hati zote za usajili wa Kampuni ya Merematа pamoja na Hati zote zinazoonyesha Hadhi ya sasa, ikiwa ni pamoja na Hati ya Mapato na Matumizi yake kwa mwaka 2001 hadi 30 Juni, 2006?

(7) Kwa utaratibu huo huo, ninaitaka Serikali kuwasilisha pia katika Bunge hili Tukufu nyaraka zote za usajili wa Kampuni ya *Mwananchi Gold Mines Ltd* ambako *BOT* ina asilimia 20 kwa niaba ya Watanzania. Ni vyema sasa Watanzania wakapata fursa ya pekee ya kujua rasilimali zao.

(8) Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge hili wakati wa kufunga hoja, hesabu ya mapato ya dhahabu iliyopata Serikali katika kipindi cha Miaka mitano iliyopita (2001-2006) ikilinganishwa na hesabu ya dhahabu yote iliyosafirishwa kwenda nje katika kipindi hicho hicho.

(9) Katika Hotuba ya Upinzani, tuliuliza kuhusu Alex Stewards, iliyopewa kazi ya kufanya Tathmini ya dhahabu inayosafirishwa nje na Waziri wa Fedha alisema Waziri anayehusika atajibu. Kambi ya Upinzani inataka majibu ya kina kama tulivyouliza.

Mheshimiwa Spika, katika Bajeti hii ya Wizara ya Nishati na Madini 2006/2007, *TANESCO* peke yake imetengewa Shilingi 207,563 kwa ajili ya miradi ya maendeleo itakayotekelezwa kwa mwaka 2006/2007. Hiyo ni sawa na asilimia 44.6 ya Wizara yote. Katika miradi hiyo, ni miradi 20 ya usambazaji umeme Vijijini kama ilivyo katika kifungu 3001 – Kasma 3112 kinavyoonyesha. Hili ni eneo ambalo Kambi ya Upinzani inaunga mkono kwa sababu miradi hii ikikamilika, angalau umeme utakuwa umesambazwa zaidi ya asilimia kumi tuliyonanyo sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, *TANESCO*, inalalamikiwa sana kutumia fedha nyingi na ni Shirika ambalo kama sio matatizo ya mikataba mibovu, lina uwezo mkubwa wa kujiendesha kibiashara. Kwa maana hiyo, Kambi ya Upinzani inamshauri Mheshimiwa Waziri kuwa mwangalifu sana kwa matumizi yanayoleta mushkel. Kwa mfano, katika ukame huu wa maji, bado Kihansi inapoteza *15MW* nusu ya mahitaji ya Kisiwa cha Unguja kwa kuyafungulia maji kwa matumizi ya vyura. Wakati huo huo Bajeti hii imetenga Sh.250,000,000/= fedha za ndani zitakazotumika kwa ajili ya utafiti zaidi na matumizi ya viumbe hao. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri inafaa atoe maelezo ya kina kuhalalisha matumizi hayo kama sio sababu nyingine ya mikataba inayoleta utata.

Mheshimiwa Spika, tunaelewa vyema suala la mazingira na tunalithamini mno, lakini inafaa tujiulize kwamba kutumia Shilingi milioni 250 kwa kuwatunza vyura wawe katika mazingira mazuri na huko nyuma zimeshatumika, zaidi ya hizo: Je, sisi tunaingiza kiasi gani kutokana na mapato ya vyura hao? Kuna nchi duniani hicho ni kitoweo, mbona hatujajuilishwa mapato yatokanayo na mauzo ya vyura hao? Ikiwa ni suala la utalii, nivyema tuelimishwe wageni wangapi wanatembelea vyura hao na kiasi gani tumeingiza? Kambi ya Upinzani haina tatizo na matunzo ya vyura ambao ni rasilimali ya nchi yetu, lakini matatizo na usahihi wa matumizi ya fedha, kiasi hicho katika mradi huu. Kwa nini fedha hizo za kutunza vyura hao zisitoke katika Ofisi ya Makamu wa Rais inayoshughulikia mazingira?

Mheshimiwa Spika, nisingependa kuzungumzia suala la *IPTL* linalochomoza kwa miaka mingi hivi sasa. Lakini ni vyema Waheshimiwa Wabunge pamoja na Watanzania wengine waelewe kwamba mbali na kinachoitwa *Capacity Charge* cha *USD 2.8 million* kwa mwezi wanazolipa *TANESCO* kwa *IPTL* bado kuna gharama za umeme unaolipwa ambao kwa kila *KWH* inayozalishwa pamoja na gharama za matengenezo *(maintenance cost)* mitambo hiyo ya *IPTL* pia hulipwa na *TANESCO*.

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba *IPTL* ni Kampuni ya Binafsi inayomilikiwa na *VIP Engineering* ya Tanzania na Kampuni ya Malaysia ambayo wao hawana *lines* za kusambaza wala kusafirisha umeme. Wakati *lines* zote za kusambaza na kusafirisha *(Transmission & Distribution),* umeme ni mali ya *TANESCO*, gharama za

mafuta zinalipwa na *TANESCO* ambazo ni *150,000 Lts* za *heavy fuel* kwa mwezi na gharama za matengenezo zinalipwa na *TANESCO*, gharama za kubadilisha mitambo inayotumia mafuta kuweka mitambo inayotumia *gas* ya *IPTL* ambayo imetengewa TSh. 18,458. Kifungu 3001-3198 katika bajeti 2006/2007 zinalipwa na *TANESCO* kupitia Wizara ya Madini na Nishati. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali ieleze hawa *IPTL* gharama zao ni zipi za *Investment* hii, ni ya wao kutafuta huo mkopo wa Benki tu?

Mheshimiwa Spika, kwa bahati mbaya kutokana na Mkataba wa *IPTL*, mikataba mingine yote hivi sasa kama vile ya *Songas* yote inafuata mtindo huo huo wa *IPTL*. Hii ni hatari na Tanzania itafilisika kwa mtindo huo.

Mheshimiwa Spika, kwa vile maneno mengi yamesemwa kuhusu utata wa mikataba ya namna hii, hata kufikia mpaka Rais wetu wa Jamhuri kulizungumzia suala hili, basi ni maoni ya Upinzani kwamba wakati umefika sasa Bunge lako Tukufu liweze kuagiza mikataba hii yote yenye utata iletwe hapa Bungeni mbele ya Kamati yako Maalum kwa kupitiwa na Bunge lako Tukufu na kuishauri Serikali ipasavyo kwa maslahi ya Taifa hili kwa mujibu wa Kifungu Na. 10 cha Sheria Na. 3 pamoja na Marekebisho yake ya Haki, Kinga na Madaraka ya Bunge ya mwaka1988.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inapendekeza yafuatayo:-

Kutokana na tatizo linalotukabili la mara kwa mara la ukosefu wa umeme nchini na kwamba maendeleo endelevu ya ukuaji wa uchumi wetu, hayawezi kupatikana bila ya kuwa na ukuaji wa viwanda pamoja na Sekta ya Kilimo ambavyo vyote vinategemea kwa kiwango kikubwa nishati ya umeme wa kutosha na wenye bei nafuu.

Ni dhahiri kwamba, sasa tunalazimika kutumia rasilimali zetu zote tulizonazo za makaa ya mawe, gesi,maji na *uranium*. Ni ushauri wa Kambi ya Upinzani kwamba nguvu zote za Serikali yetu sasa zielekezwe katika kupata nishati mchanganyiko endelevu *(sustainable power mix)* ya vyanzo vyote tulivyonavyo.

Kwamba, shirika la *NDC* hivi sasa liko katika Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko lakini kazi zake pia zina husishwa na Wizara nyengine kama vile Wizara ya Nishati na Madini. Hivyo, ipo haja ya kuandaa rasimu mpya itakayoleta ufanisi zaidi wa *NDC*.

Kwamba, Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar ziharakishe kutatua suala la mafuta bila ya kuchelewa zaidi kabla ya nishati hiyo haijapoteza thamani yake Duniani kwa sababu dunia iko mbioni kutafuta nishati mbadala na huenda gharama baadaey zikawa kubwa zaidi na kuwa vigumu kwa Makampuni kugharamia utafutaji au uchimbaji wa nishati hii.

Mheshimiwa Spika, tunaitaka Serikali ijali sana wataalam wetu na kuwapangia sehemu muafaka kwa mujibu wa taaluma zao. Baadhi ya taaluma tunao Watanzania wachache mno mathalan Wahandisi wachache tuliopeleka Ireland kujifunza utengenezaji wa injini za Magari, ambao sasa wote wametawanyika au kutawanywa na hivyo

kuinyima nchi utaalam muhimu. Wataalam hao wasihamishiwe katika nafasi za kisiasa na kuzorotesha mafanikio yaliokwishapatikana.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuyasema hayo, kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani ahsante. Umeuliza maswali mengi, natumaini Serikali itakuwa makini katika kuyajibu kwa sababu mambo haya Watanzania wote wanayasikia. Sasa pale panapokuwa ni uongo, basi Serikali ieleze. Panapokuwa kuna maelezo, yaelezwe. Kwa hiyo, tutautumia muda wetu wa Kamati ya Matumizi vizuri kesho. Serikali ikiwa wazi katika kujibu, zimeulizwa hoja za msingi hapa na ni vizuri nchi ijue. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ninao wachangiaji 31 kwenye Sekta hii. Ambaye hajachangia ni mmoja, Mheshimiwa Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa. Kwa hiyo, yeye ndiye nitamwita wa kwanza, halafu atafuatia waliochangia mara moja ambao ni Mheshimiwa Lucy Owenya, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, Mheshimiwa Jackson Makwetta na Mheshimiwa Beatrice Shellukindo. Niliowataja hao, nadhani watatosheleza kwa kipindi hiki. Baadaye nitaendelea kuwataja wengine kadri tunavyoendelea. Kwa hiyo, namwita Dr. Wilbrod Slaa, atafuatiwa na Mheshimiwa Lucy Owenya na wakati huo ajiandae Mheshimiwa Mohamed Missanga.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kwanza kabisa niweze kuchangia hotuba hii.

Lakini awali ya yote, ningependa kukupongeza wewe, Naibu Spika wako na Wenyeviti wetu kwa kuchaguliwa kuwa viongozi wa Bunge letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, siyo kwamba nimewaacha Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu, nilishawapongeza niliposimama awali katika Bunge hili.

Mheshimiwa Spika, ningependa kwa haraka haraka niingie katika mambo yafuatavyo: La kwanza kabisa, ningependa nianzie na suala la bei ya mafuta.

Mheshimiwa Spika, uchumi mzima wa nchi unategemea mafuta. Ukisafiri, bei ya nauli au gharama inategemea mafuta. Ukinunua nguo, nguo hizo zinategemea mafuta, ukinunua jembe, jembe hilo linategemea mafuta kwa sababu limesafirishwa. Kwa hiyo, unaposafirisha kitu chochote wakati bei ya mafuta iko juu na bei ya kila kitu kinapanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nipate tafsiri sahihi kutoka Serikalini. Tumepunguza *VAT* kwa asilimia 20, lakini tukaongeza ushuru *Excise Duty* na malalamiko mengi ni kwamba *Excise Duty* siyo *recoverable* kama tunavyo *recover VAT*. Kwa hiyo, bei ya mafuta ni vigumu kuteremka kwa sababu sasa wafanyabiashara hawawezi tena kupanua wigo na kwa hiyo, na wao wenyewe ndio wanaogharamia, wataendelea kubakia pale.

Mheshimiwa Spika, nataka kupata uhakika kutoka kwa Serikali kwamba, imechukua hatua gani kuhakikisha kwamba punguzo la asilimia 20 lililotolewa haliwezi kuleta athari katika uchumi wetu na wakati huo huo kuwaumiza wananchi wetu walio wengi? Bei ya mafuta sasa hivi katika nchi nzima bado ni kilio na kama utafiti wetu mdogo ulivyo kama alivyosema Msemaji wa Kambi ya Upinzani, ni asilimia nne tu ndiyo imepungua kati ya asilimia 20 tuliyopunguza sisi. Je, manufaa yake ni kwa nani?

Mheshimiwa Spika, tungependa Serikali ilitamke hilo na tungependa hatua ya makusudi iweze kuchukuliwa. Ni kweli sisi tunasema Soko ni Huria. Lakini kwa walioishi Ulaya, wanajua. Soko la Ulaya pia ni huria na linapokuwa huria, inapofika mahali Serikali inaona wananchi wake wanaumia, inatafuta mbinu ya kuingilia. Serikali yetu ni lini itatafuta mbinu ya kuingilia?

Mheshimiwa Spika, Marekani inatafuta njia hata kuleta mafuta kwenye soko yenyewe na kujaza kwenye soko ili isiharibu mfumo wa kuingilia badala yake inaweka mafuta kwenye soko ili bei ya mafuta ibaki chini. Tanzania tutafanya lini hivi tumwokoe huyu Mtanzania tunayesema kila siku, tunayeimba kila siku, tunataka kumwokoa kwa MKUKUTA, lakini hakuna hatua zinazothibitika kwamba zinaweza kumsaidia? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niende kwenye umeme. Kwanza, tatizo zima la *TANESCO* nadhani tumeishalisema. Najua kwamba kesi imekwisha huko Mahakamani, lakini najua bado sisi na *TANESCO* tunalipana mabilioni.

Tungependa sasa, baada ya kesi kwisha, kwa sababu lilipokuwa Mahakamani, Serikali ilitwambia haiwezi kutueleza mgogoro wetu na *IPTL,* sasa mgogoro umekwisha na kwa kuwa umekwisha Watanzania wanataka kujua leo, ni athari gani tumepata kwa Mkataba wetu sisi na *IPTL*? Tunalipa kwa mwezi kiasi gani cha fedha kwa kulipa *capacity charge* kwa matumizi ambayo hatuyatumii na kadhalika? Kwa taarifa tulizonazo ni zaidi ya Shilingi bilioni tatu zisizo na maana kila mwezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Shilingi bilioni tatu ni fedha nyingi sana. Ukizipeleka kwenye Wilaya yangu ya Karatu itageuka kuwa Ulaya siku hiyo hiyo na hivyo hivyo kwa Wilaya nyingi ambazo hazina maji, hazina hospitali na hazina Zahanati. Sasa tunakwenda kulipa Mkataba ambao haukuwa na manufaa kwa nchi hii. Ningependa kujua na Serikali pia ilete taarifa tujue ni akinanani walisababisha huu Mkataba usio na manufaa. Kwa hapo niseme kwamba, naungana na taarifa ya Kamati kwamba iundwe Kamati Teule ambayo itachunguza sasa kama Bunge. Serikali ni Serikali na Bunge ni Bunge.

Mheshimia Spika, kwa hiyo, Bunge namna yake ya kuisimamia Serikali ni kupitia Kamati Teule. Tungependa kazi hiyo ifanyike ili tuweze kujua hii Mikataba yote ambayo ina mushkeli tuweze kuitazama. Suala la kusema Mikataba ni kazi ya Serikali huo ni mchezo ambao hauna manufaa ndani ya Bunge hili. Jukumu la Serikali ni kutenda. Jukumu la Bunge ni kusimamia, lakini kusimamia ni pamoja na kujua nini kilitokea na huwezi kujua kama hujaletewa. Taarifa ndiyo itatufanya tuweze kujua. Tunaomba hizo taarifa zote zipatikane. Kamati Teule ndiyo njia pekee itakayotusaidia kuweza kufanya kazi hiyo.

Mheshimiwa Spika, bado suala la umeme mimi linanipa kiwewe. Ni juzi tu tumetoka kwenye mvua. Dar es Salaam mpaka juzi kulikuwa na mafuriko. Sasa bado hata kule kwenye *sources* kama Ruaha, ni miezi miwili tu mvua ndiyo imekwisha, labda hata manyunyu bado yanaendelea, lakini tuko tayari kwenye mgao. Hivi tutafikaje kwenye mvua ijayo na tukaokoka na mgao huu wa umeme uliopo? Kuna siri gani? Haiwezi kuwa tu ni wakulima ndiyo wamesababisha mmomonyoko ukaenda kwenye Ziwa likajaa!

Mheshimiwa Spika, mimi nadhani tunahitaji taarifa ya kina. Kule Mtera kuna nini? Jambo hilo la matope haliwezi kuwa limekwenda tu kwa mwaka mmoja au miaka miwili. Tope lilikuwa linateremka polepole. Tope limekwenda polepole, Serikali siku zote ilikuwa wapi? Ni kuonyeshwa kwamba hatukuwa na mipango, hatukuwa na *protective design,* waliohusika hawakuchukua hatua. Kama tumefika hapa, leo tunafikishwa kwenye hali ngumu hii! Serikali inachukua hatua gani kwa Maafisa wake walioona kwamba kuna udongo unaingia katika bwawa la Mtera na hawakuchua hatua? Serikali inatuahidi nini kwamba hao waliohusika na kuiletea hasara kubwa nchi yetu hawakuchukuliwa hatua na bado wanaendelea kufanya shughuli zao? Lazima kuna mtu alikuwa mzembe na hao waliokuwa wazembe ni lazima tufike mahali watu wachukuliwe hatua ili tuweze kuepuka mambo hayo huko tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, habari ya kwenda kununua *generato*r, habari ya kwenda kukodisha *generator* leo, ni kwa sababu ya uzembe wa watu wachache. Tumefikia hatua ya nchi kukodisha *generator*! Ni jambo nzito kweli kweli! Mimi sina tatizo kama ni mpango wa muda mfupi, ni sawa. Lakini inaonyesha ni kwa kiasi gani hatukuwa na mpango katika muda mrefu uliopita? Sina shida na Waziri, rafiki yangu pale, kwa sababu najua yeye ameingia hivi karibuni. Kwa hiyo, lazima achukue hatua. Mheshimiwa Waziri sina tatizo, lakini Serikali ni moja. Wewe ni Waziri, Ofisi iko pale, umeikuta, tunataka utueleze ni kitu gani kiko kule kwenye mabwawa yetu na hii kasoro ni nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nigusie kidogo suala la Mchuchuma. Nimeshutushwa sana na suala la Mchuchuma. Ni jambo la kusikitisha, kwa sababu mimi nilikuwepo, bahati nzuri kwenye Bunge hili tarehe 02 Julai, 2001 Mheshimiwa Spika aliyekuwepo kama alivyokuwa amekaa kwenye Kiti chake akatutambulisha wageni kwenye *gallery* yake. Walikuwepo wageni kama 20 wakiongozwa na Kampuni ya *Siemens,* tukatambulishwa kwamba hao ndiyo walikuwa Wawekezaji wetu. Tukapiga makofi. Tukaenda kushuhudia uwekaji saini huo Mkataba na sisi tukaenda kula hapa hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, leo Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake anatuambia vitu ambavyo mimi sielewi. Anasema, imeundwa Kamati Maalum ambayo inazishirikisha Wizara mbalimbali, bado inafanya tathmini kutoa ushauri kuhusu njia bora ya kuendeleza miradi hiyo. Mimi taarifa niliyonayo wale *Consortium Siemens* iliwekeza fedha kiasi cha kutosha wakijua wanakwenda kutekeleza pamoja na ndugu zao wa *NDC. NDC* ni Shirika la Taifa. Mkataba umesainiwa kati ya *NDC* kwa niaba ya Serikali yetu na

ile *Consortium* wakiwa wamejiandaa kwenda kutekeleza mradi wa Mchuchuma na kwa hatua fulani labda na wa Liganga.

Mheshimiwa Spika, Sasa tunataka kujua ni kitu gani kimetokea na mimi nina taarifa kwamba Mheshimiwa Waziri tena huyu wa sasa na nina nakala ya barua yako hiyo, ameandikiwa barua mwezi Januari na *group* hiyo ya *siemens*. Kitu gani kimetokea tumesaini Mkataba wa Kimataifa, Mkataba huo umeshindikana kwa miaka hiyo toka mwaka 2001 mpaka mwaka 2004? Ni kitu gani kimefikia hatua hiyo wakati Baraza la Mawaziri lilikwishaamua? Wakati huo huo, tuna taarifa tuliyopewa na Mheshimiwa Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwamba Baraza la Mawaziri liliamua, lakini *TANESCO* ambayo inaongozwa na *Net Group* wamebadilisha uamuzi wa Baraza la Mawaziri. Nchi hii inaongozwa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunahitaji Bunge hili lielezwe, nchi hii inaongozwa na mtu gani? Sisi tunajua kuna Mheshimiwa Rais ndiyo Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri. Kumbe maamuzi hata ya Baraza Mawaziri ambayo Mwenyekiti wake ni Rais yanaweza yakawekwa pembeni na huyo aliyoyaweka pembeni zichukuliwe hatua! Hili ni jambo la ajabu! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nchi hii imefikishwa pabaya sana. Kama tunafika mahali mtu mmoja au kundi la watu linabadilisha na hatujaambiwa katika Bunge hili limebadilishwa kwa nini, wakati Spika alisimama akatutangazia, hatukutangaziwa tena kwamba wale walishindwa kufanya ile kazi, tungetangaziwa, tungeelewa. Hivi nchi hii katika macho ya Mataifa itaaminika vipi mnaleta *Consortium* kubwa zenye uwezo mkubwa na *Consortium* hiyo mnaipa kazi, wanatumia hela, leo Mkataba unavunjwa eti kwa ajili ya Kamati ambayo inaundwa na Wizara! Hakuna utaratibu wowote uliofuatwa, sina hakika zile *clauses* zikoje! Ndiyo maana naunga mkono hoja ya Kamati Teule kwamba tunahitaji kupitia hata ile *memorandum* iliyosainiwa ili tujue Mikataba hii ilipita vipi na inasema nini na nchi yetu iweze kurudi kwenye heshima inayostahili mbele ya Vyombo vya Mataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni kweli taarifa ya Kamati yetu imetamka kwamba wako wawekezaji, lakini tabia hii mimi inanishtua. Ni kweli kama alivyosema Msemaji aliyepita kwamba, *lobbying* inafanyika duniani kote. Lakini *lobbying* inapofika mahali, mpaka Kamati ya Bunge inaambiwa. Mimi naomba, jamani mnipe hili eneo. Ekari 1400, halafu anaeleza hapo hapo, nimeshazunguka kule, wananchi nimewajengea shule na nimewapa bati 500. Hivi bati 500 zinafanana na Mchuchuma! Hivi tani 29 za sementi zinafanana na Mchuchuma wa nchi hii!

Mheshimiwa Spika, nimeambiwa pia kwamba, Kamati ya Bunge ilipokwenda kule imepewa taarifa hiyo ndani ya Kamati, imeambiwa na nje kule imeambiwa. Hivi ni kweli kwamba tukubali rushwa ya waziwazi! Kama hao watu wameshapita kwenye Serikali yetu na wapo wanaohusika, kwa nini wasijiuzulu kwa utamaduni ule wa uwajibikaji? Kama hawataki kujiuzulu, ni kwa nini *PCB* isichukue hatua wakati inaona kabisa mambo sio mazuri? Suala la wenzetu na suala la uzalendo, kama utaratibu unafuatwa sina tatizo. Lakini uzalendo unapoingia, kukiuka utaratibu kama inakiuka

*Public Procurement Act* tuliyopitisha ndani ya Bunge hili, hapo tena sio suala la uzalendo. Uzalendo huo una wingu lingine lililojificha pembeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunapenda tuelezwe hapa kwamba, kuna kitu gani hapo? Nitapenda kujua kama Mkataba wa awali ulikuwepo haujavunjwa. Kama Mkataba na *Siemens* ungevunjwa na *Consortium* yao na leo tunatafuata mwingine, mimi nitaelewa. Nataka kujua ni lini na kwa barua gani na namba gani ilivunja ule Mkataba wa awali mpaka leo tunaanza kumtafuta huyu mwekezaji mwengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ninavyosema siku zote, ninatafuta *principle*, mimi sijali ni nani anayepewa. Lakini inapokiukwa *principle,* tunaweka nchi yetu katika hali ya hatari na hali mbaya na tunaruhusu mianya ya rushwa ambayo tulikiri kwamba sisi sote tunaipiga vita.

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Mkataba huo na hata jitihada hizo za kutoa bati 500 zimeanza mwaka 2005. Ingekuwa mwaka huu, ningesema labda kwa kuwa mkakati wa Taifa wa Rushwa umeisha wakati wake. Maana yake ulikuwa 2000 - 2005. Kwa hiyo, ningesema tuko kwenye kipindi ambacho hakina Mkataba. Tuna kipindi chake, Mkataba huo tumesema uko ndani ya kipindi hicho hicho. Sisi katika Bunge hili tulitaarifiwa, leo hatutaarifiwi, lakini zinapita taratibu nyingine. Ninaelewa kilio cha watu wa kule Ludewa, ninaelewa fikra na hisia za Mheshimiwa Mbunge mwenzangu anayetokea Ludewa akipiga kelele kwamba mradi umechelewa na mimi nasema mradi huu umechelewa. Tuliazimia utekelezwe mara moja na Baraza la Mawaziri, haukutekelezwa. Umechelewa na wananchi wetu wanakosa ajira, tunakosa fedha na tunakosa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na hayo, wananchi wetu tuwaombe watuelewe kwamba tukipeleka bati 500 Mchuchuma, tumeuza nchi, ni sawa na kuuza ng'ombe kwa kesi ya kuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa muda umekwisha, naomba niongelee eneo lingine kwa haraka. Ningependa niliseme kwa ufupi sana suala la *Tanzanite* na Mererani. La kwanza, naomba kuunga mkono hoja zilizotolewa na Msemaji wa Kambi ya Upinzani. Tumefanya utafiti wa kina, Kambi ya Upinzani hatukuja tu na hoja, tumekuja na utafiti wa kina kuonyesha pale vinapopatikana vito aina ya *Tanzanite,* lakini inapatikana katika nchi moja. Wananchi wa nchi ile wanapewa kipaumbele katika kuichimba. Tumetoa mifano, imesomwa kwenye hotuba yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Tanzania sisi Mererani ni vito pekee duniani, inatokea Tanzania na ikaitwa *Tanzanite* kwa heshima yetu. Watanzania wa Mererani wanateseka, wanadhalilika, Serikali yetu inawatazama kana kwamba hatuna Serikali. Tuna taarifa za watu waliouawa zimezungumzwa ndani ya Bunge hili, waliohusika walipelekwa Mahakamani kesi haziendelei. Tuna taarifa ya watu kupelekewa mbwa, kesi haziendelei, tuna taarifa ya zile *blocks* zimepimwa wananchi wanatolewa kule kwa nguvu. Tunataka kujua taarifa sahihi: Je, rasilimali ya nchi hii Watanzania watazifurahia lini na watalindwa lini na Serikali yao? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ya pili ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika hotuba ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri Dr. Ibrahim Msabaha na Mheshimiwa Naibu Waziri Lawrence Masha kwa hotuba yao nzuri ambayo ni fupi lakini ni *well prepared.* Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nikiwa kama mwanakamati katika Kamati hii ya Nishati na Madini, napenda nimpongeze Mheshimiwa William Shellukindo kwa hotuba yake nzuri aliyoitoa muda fupi uliopita.

Vilevile, napenda nimpongeze sana Msemaji wa Kambi ya Upinzani kwa hotuba yake nzuri ambayo ni *well researched,* imegusa katika sehemu zote za nishati na madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi sitakuwa na mengi sana ya kuchangia kwa sababu mengi yamezungumzwa na Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, amenipunja kidogo. Lakini kwa sababu umeme ni sehemu kubwa ya maendeleo ya Taifa na kumekuwa na tatizo kubwa sana la umeme na tatizo la umeme wanalizungumzia ni kuhusu maji kwenda Mtera, mvua zinanyesha lakini bwawa halijai, kama Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa alivyozungumza, kuna tatizo gani Mtera? Ni lini lile bwawa lilifanyiwa *service*? Matope yaliondolewa lini siku ya mwisho? Je, *life span* ya zile mashine ni za muda gani? Au mashine ziko chakavu au kuna tatizo gani? Tunaomba Mheshimiwa Waziri atueleze ili Watanzania waweze kuelewa tatizo la umeme hapa Tanzania linatokana na nini? Maana yake hili bwawa halijai hata siku moja. Kuna tatizo gani?

Vilevile, namshukuru Mheshimiwa Waziri, amezungumza kwamba watatafuta njia ya kutengeneza umeme mbadala kama vile gesi, umeme wa jua, pamoja na umeme wa mkaa. Mimi nikiwa kama mwana Kamati tulitembelea makaa ya mawe kule mchuchuma, utafiti umeshafanyika, inaonyesha kwamba kule mchuchuma, umeme unaweza kuzalishwa kwa *Megawatt 1600.* Sasa tatizo ni nini? Kama *NDC* ilishafanya uchunguzi, kwa nini hii *project* haianzi? Umeme unaweza ukatutosha Tanzania nzima, pia tukaweza kuuza umeme kwenye nchi jirani.

Mimi nafikiri Serikali iwe *serious* kidogo kuweka mkazo katika huu mradi wa mchuchuma, ili tuweze kupata umeme kwa bei nafuu na vilevile itasaidia watu waweze kutumia makaa kwa ajili ya kupikia na kutunza mazingira yetu. *(Makofi)*

Vilevile, kama tukiweza kupata umeme wa kutosha na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini amezungumzia, ataimarisha umeme kwenye Vijiji na umeme huu uwe ni wa bei nafuu. Umeme ukipelekwa Vijijini, ina maana viwanda vidogo vidogo vinaweza vikatengenezwa na kwa sababu asilimia 80 ya Watanzania wanaishi Vijijini, ina maana wanaweza wakazalisha kule Vijijini na watu wana uhakika wa kupeleka

mazao yao kwenye viwanda hata wafugaji wanaweza wakatengeneza siagi na wanakuwa na uhakika wa kusindika matunda yao na kadhalika. Hii ita-*create* ajira na watu hawawezi kukimbilia Mjini. Sasa hivi watu wengi wanakimbilia Mjini kwa sababu ya matatizo ya ajira na hii itapelekea Watanzania wengi na Serikali kuweza kutekeleza ile sera ya CCM inayosema maisha bora kwa kila Mtanzania.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine, tunajiuliza, kwa nini vyanzo vya maji vinachezewa. Hii ni kwa sababu hakuna umeme Vijijini, vyanzo vya maji. Mtu yupo Kijijini anaambiwa asilime nyanya kwa sababu maji yanahitajika kuzalisha umeme, hivyo wasinyeshewe. Sasa yule mtu wa Kijijini hawezi kuelewa, lakini akipelekewa umeme kule Kijijini itampa motisha na ataona kwamba anapata kazi na umeme anaupata na kuyaona manufaa yake.

Kitu kingine, ni kuhusu bei ya petroli. Bei ya petroli imekuwa ikipanda kila leo. Nashukuru katika kikao kilichopita, kwenye swali langu la msingi, niliomba *VAT* iondolewe katika bei ya mafuta na nashukuru Wizara ya Fedha imeondoa *VAT* hiyo. Lakini cha kusikitisha ni kwamba bei za mafuta hazishuki. Unakwenda kwenye *petrol station,* leo unauziwa mafuta lita moja Sh.1,350/= wanakwambia petroli imekwisha. Ukienda kesho yake, wanakuuzia bei ile ile ya Sh.1,350/=, ukiwauliza kwa nini bei haijateremka, wanakwambia mafuta hayajakwisha *Depot.* Kweli haya mafuta yatakaa yaishe *Depot.* Mimi nafikiri ni wakati muafaka sasa Serikali kuangalia ni jinsi gani ya ku-*control* hizi bei za mafuta. Pengine lile Shirika la *TIPPER* lirudi tuwe na malighafi, petroli iwe *processed* hapa nchini. Hii itasaidia Serikali ku-*control* bei ya mafuta na mafuta yatakuwa bei nafuu kwa kila mtu.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ni kuhusu madini. Kila mtu amekuwa akizungumzia suala la madini na watu wanauawa Mererani. Je, haki za binadamu zinafanya nini na kwa nini watu hawa wasisaidiwe? Kwa nini *STAMICO* isisimamie miradi ya madini ikawa inakuwa-*controlled* na Kampuni moja badala ya kuficha hii Mikataba ili watu wasiione? Namuunga mkono kabisa Msemaji wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara kwamba Mikataba iletwe hadharani na tuione na iundwe hiyo Kamati ili iweze kusimamia Mikataba hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sina mengi ya kuzungumza. Nakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED H. MISSANGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja iliyoko mbele yetu, hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Kwanza, nichukue nafasi hii baada ya kukushukuru wewe kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioko kwenye Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa muda mfupi ambapo wamekuwepo kwenye Wizara hii. Matunda yao nadhani yanaonekana kwa walio wengi.

Mheshimiwa Spika, kama unavyofahamu, ni kwamba Wizara hii imekumbwa na matatizo ya ukame ambao umesababisha matatizo ya maji yaliyosababisha uhaba wa umeme na kuingia kwenye mgao. Lakini kwa umahiri wa wenzetu hawa, Dr. Msabaha, Naibu wake na Watendaji kwa ujumla, wameweza kuifanya kazi hiyo na sasa matumaini yanaonekana. Ingawa inaweza kuchukua muda kiasi kidogo, lakini maelezo yaliyotolewa na nia ya Serikali ya Awamu ya Nne ilileta matumaini kwamba baada ya muda mfupi tunaweza tukajikomboa kabisa katika suala la umeme kwa mipango iliyopo. Kwa hiyo, mimi nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya waendelee hivyo hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilipochangia mwaka 2005 katika hoja ya Wizara hii, nilieleza sana kilio changu cha umeme kwa upande wa Ihanja. Juzi nilikuwa naangalia *Hansard* kuona nilichangia nini, nikakuta kwamba kwa kweli nilichangia katika hali ya kusikitika sana na kuvunjika moyo sana na lugha nyingine pengine haikuwa ya kistaarabu. Lakini nakumbuka maneno mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwamba nifanye subira na kwa sababu tunahimizwa kufanya subira, basi nimefanya subira na kweli subira imeleta matunda mazuri kwamba Mheshimiwa Waziri alipokuwa anatoa maelezo yake ametaja eneo hilo la Ihanja kwamba litapata umeme.

Kwa hiyo, napenda kutumia nafasi hii ya kwanza kabisa kumshukuru sana ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Msabaha na wenzake kwa kusikiliza kilio changu, lakini kwa kweli kwa kusikiliza kilio cha wananchi wa Ihanja cha kupata umeme kwa muda mrefu toka mwaka 1998 walipoonjeshwa nguzo mpaka sasa hawajapata umeme. Sasa ni matumaini yangu kwamba, baada ya kuwekwa katika mpango wa mwaka huu wa fedha wa 2005/2006, basi haitachukuwa tena muda mrefu kupatiwa umeme. Maana, kuwekwa kwenye mpango ni jambo moja na kupatiwa umeme ni jambo lingine. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri ahakikishe kwamba wananchi wale wanapata umeme muda sio mrefu, kwa sababu ni kama kilomita 12 kutoka pale Puma.

Mheshimiwa Spika, lakini vile vile ninayo taarifa kama alivyosema mwenyewe kwamba atatupa baadaye kiambatisho ambacho kinaeleza kwamba Tarafa ya Sepuka ambayo ndiyo ilikuwa ni Tarafa ya pekee katika Mkoa wa Singida ambayo ilikuwa haikuwa umeme, sasa nasubiri kiambatisho, lakini taarifa za awali nilizopata ni kwamba hata Sepuka nao watapata umeme. Kwa hiyo, nataka nichukue nafasi hii vile vile kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwamba vilio vyangu vyote viwili angalau vimesikilizwa na nina hakika wananchi wananisikia, wananchi wa Ihanja, Singida, kwa hiyo, wajiandae sasa kuutumia vizuri umeme hasa vijana, watumie umeme utakapofika kwa ajili ya kujipatia ajira ili kutekeleza vizuri ukamilifu sera ya Chama cha Mapinduzi ya kutengeneza ajira angalau milioni moja katika kipindi cha miaka mitano. Nadhani umeme huu utachangia kwa kiasi kikubwa katika hizo ajira milioni moja ambazo nimeahidiwa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, pamoja na pongezi hizo nataka niongeze au nirudie kwa kweli maombi yangu ya umeme katika maeneo yafuatayo: Moja, niliomba kwamba, pale Isuna, umeme unapita ule uliopoozwa unakwenda Ikungi na kuna Shule pale ya Ufundi ambayo inamilikiwa na *Mission*. Ni kama kilomita moja na nusu kutoka kwenye laini

kubwa. Wanahangaika sana wale watu, ningemwomba sana Mheshimiwa Waziri angalau wasaidiwe kwa sababu kama alivyosema, sera ni kuwapatia wananchi wale walioko katika laini na wale walioko pale, ningeomba sana iwasaidie ili Shule yetu ile ambayo inaendeshwa na wenzetu Wamisionari iweze kufanikiwa kupata umeme.

Mheshimiwa Spika, lakini eneo lingine ambalo nataka niliombee umeme ni Kijiji kimoja kinachoitwa Sambaru, Kata ya Mang'oni, Tarafa ya Ikungi, kumegundulika madini ya dhahabu. Sasa hivi wachimbaji wadogo wadogo wanachangamka kweli kweli kwa ajili ya dhahabu pale. Hata wachimbaji wakubwa sasa hivi wanakuja, kwa sababu yuko mwekezaji mmoja ambaye tayari ameshatujengea Uwanja wa Ndege pale, ingawa Singida penyewe hakuna Uwanja wa Ndege, lakini pale Vijijini yuko mwekezaji amejenga Uwanja wa Ndege pale kwa ajili ya kurahisisha habari ya kwenda kuangalia madini pale.

Kwa hiyo, tuwaunge mkono wale wachimbaji wadogo wadogo pale kwa kupatiwa umeme. Kutoka Ikungi ulipo umeme mpaka pale Sambaru ninaposema kwenye madini ni kama kilomita 25 au 26, hazizidi 30. Nadhani ni eneo zuri ni eneo sio refu ambalo linaweza kabisa likasaidiwa likapata umeme ili wachimbaji wadogo wadogo na wengine watakaokuja waweze kurahisisha kufanya kazi za uchimbaji madini, jambo ambalo litasaidia kuongeza kipato kwa wananchi wa Singida, uchumi wa Singida utaimarika lakini pia uchumi wa nchi na Pato la Taifa litaimarika. Hilo ni eneo la pili ambalo ningependa kuliombea.

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu, kuna Kijiji kinaitwa Unyankanya, kipo karibu sana na Kijiji cha Suyu ambapo upo umeme. Sijui Mheshimiwa Waziri atakumbuka kwamba, tulikwenda pale, ile Shule ya Sekondari ya Paroti wanashukuru sana kwa kazi nzuri aliyoifanya ya kuwapatia umeme, vijana wanasoma vizuri sana. Sasa Kijiji jirani cha Paroti pia wanaomba umeme, ni kama kilomita mbili kutoka pale Suyu, napo sio mbali sana. Ningependa pia nitumie nafasi hii kuwaombea na hao ili waweze kupata umeme waweze kufanya kazi zao za kawaida.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nataka niseme kwamba, ni azma ya Serikali ya Awamu ya Nne kupeleka umeme Vijijini kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwamba, huu mpango wa *Energizing Rural Transformation (ERT)* nadhani ni mpango mzuri ambao utasaidia kueneza umeme Vijijini ambao utakuwa na faida nyingi, kazi kwa vijana na matumizi mengine. Lakini kubwa zaidi, utasaidia sana kupunguza uharibifu wa mazingira kule Vijijini kwa maana ya kukata kuni na kadhalika. Ni wazo zuri, lakini nataka nishauri kwamba ili kuendelea kuwaunga mkono hawa wananchi wa Vijijini ambao umeme unapita kule au upo kule, kwa kweli kwa *tariff* hii ya sasa ya kawaida ya *TANESCO* pengine itakuwa kikwazo kwao. Kwa hiyo, nia ya Serikali ya kuwapelekea wananchi umeme kule Vijijini itakuwa kidogo imedhoofika au haitawezekana.

Mheshimiwa Spika, nilitaka nishauri kwamba pengine kuanzishwe *tariff* maalum kwa ajili ya watu waliotumiwa umeme Vijijini. Kuwe na *tariff* ya Mjini,, lakini pia kuwe na *tariff* ya Vijijini kwa kuzingatia kwamba uchumi na uwezo wa wananchi walioko

Vijijini uwezo wao ni mdogo, hawawezi ku-*manage* kuwa na *tariff* ya kawaida. Hilo sio jambo geni. Huko nyuma nakumbuka kulikuwa na mishahara, kima cha chini cha Mjini na kima cha chini Vijijini. Huko tunakotoka ilikuwa hivyo. Kwa hiyo, ni jambo ambalo linawezekana kwa sababu wakati ule ilidhaniwa kule Kijijini kima cha chini kidogo kwa sababu hali ya maisha ilikuwa chini. Lakini sasa hivi ilijulikana hata kule hali ya maisha ni ngumu, ndiyo maana kima cha chini kimekuwa ni kimoja bila ya kujali Mjini na Vijijini.

Lakini kwa upande wa umeme, nasema kama utaratibu wa sasa sijui kuingiza umeme shilingi laki mbili, laki tatu kwa mwananchi wa kawaida, ataona umeme unapita hapa, lakini hawezi akauingiza. Kama bili ya shilingi elfu tano au elfu sita na elfu saba, mwananchi wa kawaida hatamudu. Kwa hiyo, ile azma nzuri ya Serikali ya kupeleka umeme Vijijini haitapatikana.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu ni kwamba, Serikali iangalie uwezekano wa kuwa na *tariff* maalum kwa ajili ya umeme Vijijini ili kuwasaidia wananchi wa Vijijini waweze kuwa na umeme kwa kazi mbalimbali, lakini jambo hilo pia litasaidia kuweza kupunguza athari za uharibifu wa mazingira ya kukata kuni kwa sababu kutakuwa na umeme mbadala. Hivi sasa naambiwa na sio naambiwa, ni ukweli kwamba hata baadhi yetu sisi humu ndani, Mawaziri humu ndani, hakuna mtu ambaye anatumia jiko la umeme kule nyumbani. Wote ni mkaa tu, kwa sababu tunashindwa kulipa. Sasa kama sisi na hali hii tuliyonayo tunashindwa kulipa umeme, sembuse wenzetu walioko Vijijini, wataweza kulipa vipi umeme? Ningeomba tuwafikirie ili kusudi tuone kwamba wanapata fursa ya kutumia umeme huko Vijijini kama tunavyowatarajia.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka niseme ni kuhusu madini. Nimeshagusia pale kwamba katika eneo la Sambaru, nimeeleza Sambaru Kata ya Mang'oni kuna madini pale. Lakini yapo matatizo mawili. Moja la umeme nimelieleza, sina sababu ya kurudia, naomba muwapatie umeme. Lakini la pili, kuna ucheleweshaji wa kuwapa leseni wale wachimbaji wadogo wadogo. Wako wengine wameomba leseni toka mwaka 2003, wapo wengine wameomba umeme toka mwaka 2004 na mpaka sasa hawajapata leseni. Mwaka 2003 alikwenda Kamishna Msaidizi wa Madini akawaahidi kwamba atatoa leseni zaidi ya 100, lakini alitoa siku ile 40 tu na tangu wakati huo mpaka sasa hakuna mtu yoyote ambaye amepata umeme. Sasa wanajiuliza kuna tatizo gani?

Wale ambao wanapata nafasi ya kwenda Dar es Salaam kwenda kusukuma sukuma na nini, wanaweza wakapata leseni, wale ambao hawana uwezo wa kwenda Dar es Salaam hawapati hizo leseni. Sasa inaleta wimbi la mashaka mashaka kwamba ili upate leseni, basi inabidi uhangaike kwa namna moja au nyingine. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri awasaidie wenzetu wachimbaji wadogo wadogo wapate leseni zao bila vikwazo vyote vyote ili waweze kuendelea na shughuli nzuri ambayo wanaifanya.

Mheshimiwa Spika, Kijiji cha Sambaru, labda nitoe mfano, yuko mchimbaji mdogo anaitwa Limbu Magambo. Yeye toka mwaka 2004 ameomba lakini hajapata leseni mpaka leo. Yuko mwingine anaitwa Abdallah Kagondi ameomba toka mwaka 2004 hajapata mpaka leo na yuko mwingine Belta Mkumbo naye ameomba leseni toka

mwaka 2004 pia hajapata mpaka leo hii. Huo ni mfano tu, lakini nasema wako wengi ambao wameomba hawajapatiwa. Tatizo ni nini na wakati Kamishna Msaidizi aliwahi kuwaona?

Mheshimiwa Spika, imezungumzwa habari ya bei ya mafuta. Mimi nilikuwa nimejiandaa hapa kwamba ni jambo ambalo linasikitisha kwa kweli, kwamba, Serikali katika Bajeti yake, imeondoa *VAT* katika mafuta, lakini hali halisi imeonyesha kabisa kwamba bei ya mafuta bado iko pale pale katika Vituo vyetu. Sh. 1,400/=, Sh.1,300/= ni jambo la kusikitisha. Mwaka 2003 ndugu yangu Mheshimiwa Mramba alipokuwa Waziri wa Fedha, aliwahi kupunguza kodi katika mafuta mazito, *Heavy Finest Oil* kitu kama hicho, kwa mategemeo kwamba bidhaa zitapungua. Lakini toka wakati ule alipopunguza Mheshimiwa Mramba au Serikali kwa ujumla sio bati, sementi, nondo ambayo ilipungua, ingawa ule msaada ulikuwepo na wale wenye viwanda walipata. Sasa na hapa tena bei zimepunguzwa, lakini mafuta bei imebaki pale pale.

Sasa najiuliza, hivi nafuu hii anayepewa ni nani? Nia ya Serikali ni kuwapa wenye viwanda unafuu watakapopunguza *VAT* na kodi nyingine, au nia ni kumsaidia mwananchi wa kawaida? Ushahidi uliopo ni kwamba kwa kweli mwananchi hafaidiki kwa mfano huo niliotoa wa *Heavy Finest Oil* mwaka 2003 ambao hakuna bei imepungua. Singida sasa hivi tunanunua sementi Sh.12,000/= mpaka 13,000/=, bati tunanunua Sh.11,000/= mpaka Sh. 12,000/= halafu unamwambia mtu ajenge nyumba ya kisasa ya kimaendeleo, atajenga kwa namna gani? Kama sisi wenyewe inatushinda, je, wale wananchi wa kawaida itakuwaje?

Kwa hiyo, ningeiomba Serikali inapoamua kupunguza kodi au kuondoa *VAT,* lazima wawe na *mechanism* ya kuhakikisha kwamba msaada ule, huruma ile imewafikia wale walengwa ambao ni wananchi. Vinginevyo, itakuwa inawaendea hawa watu wengine ambao hawakuhusika.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. LUCAS L. SELELII:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii ambayo nimeipata. Kwanza, napenda kutambua uwepo wa Mwalimu wangu, Mheshimiwa Kahumbi, Mbunge wa Bukene, ambaye yuko hapa na sisi leo. Ni Mwalimu ambaye amenifundisha siasa na katika miongoni mwa watu ambao walizungumza na kupiga kelele sana kwa ajili ya kupata umeme Bukene, naomba wananchi wa Bukene wamshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Kahumbi kwa kazi aliyoifanya. Nimeona nianzie na hili nisije nikasahau kwa sababu lazima tuwaenzi ambao wametutangulia. Ahsante sana Mheshimiwa Kahumbi kwa kazi nzuri uliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini inabeba upande mmoja mambo mazuri, lakini upande mwingine mambo mabaya sana. Lakini kama utamaduni, nataka nianzie na yale mazuri. Naishukuru Serikali ya Awamu ya Nne kwa kuwekeza fedha nyingi kwa ajili ya kuweka umeme Vijijini. Nitatoa mfano kwa Wilaya ya Nzega. Wilaya ya Nzega Makao Makuu ya Wilaya imepata umeme miaka ya 1980. Lakini ni Vijiji vitano tu ambavyo viliweza kupatiwa umeme katika Wilaya ya Nzega. Kwenye

Bajeti hii, nashukuru kwamba Serikali imekumbuka kutenga hela kwa ajili ya kupeleka umeme Bukene na kwa ajili ya kupeleka umeme Puge na Ndala. Kwa hiyo nashukuru sana kwa juhudi ambazo Serikali imefanya.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho naomba upande huu wa umeme ni kwamba Serikali iweze kuzingatia kuwezesha Shirika hili la *TANESCO* na hasa baada ya kuondoka hawa wawekezaji wa *Net Group Solution.* Hawa kwa kweli *Net Group Solution* hata juzi nilipouliza walikuja kuzoa na kupata faida ambayo hawakuwahi kuwekeza hata kidogo. Kwa hali hiyo, Serikali yetu naomba sana iwezeshe Shirika la *TANESCO* liweze kuwekeza. Sasa hivi *TANESCO* hata ukiuliza mita tu, hawana. Tulipewa matumaini makubwa sana wakati *Net Group Solution* wanakuja kwamba itaondoa matatizo madogo madogo. Kilichokuja kufanyika, ni kupandisha bei na kukusanya basi. Kwa hiyo, hapa ningependa Shirika la *TANESCO* liweze kuwezeshwa ili liweze kuwekeza na hasa kuondoa matatizo madogo madogo ya kusambaza umeme Vijijini na hata katika maeneo mengine, lakini vile vile kuondosha tatizo la kuwa na mita.

Mheshimiwa Spika, naingia kule kubaya. Lakini kabla sijafika kubaya, kabla sijasahau, kwa kweli napenda kwa moyo wa dhati nimshukuru sana Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Awamu ya Nne. Kwa kweli Rais huyu ni Rais anayesikia na anayejali maneno ambayo anaambiwa na wananchi na hasa kwa kukubali kuingia kuona Mikataba hii ambayo imeingiwa na wachimbaji wakubwa na kukubali kwamba ianze kuzungumzwa na kuifanyia marekebisho. Namshukuru sana Mheshimiwa Rais pamoja na Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini Nishati na Madini katika mambo ambayo ni mabaya, ni wenye Mikataba hii ya wachimbaji wakubwa wakubwa. Ni mabaya kupindukia. Nadhani kama ni dhambi kubwa ndiyo kwenye dhambi, mimi nawalaumu sana na kwa kweli nawalaumu Wanasheria wetu wa nchi hii. Kwa kweli nitaendelea kuwalaumu Wanasheria wetu wa nchi hii kwa sababu wanatuingiza kwenye Mikataba ambayo haina maslahi ya Taifa na tunapokuja kusimama kusema, wanaanza kusema tunazungumza mambo ya kisiasa. Sisi tumeanza kulalamikia Mikataba hii ya Madini mwaka 1998, Mheshimiwa Kahumbi yupo hapa ni shahidi. Serikali ilikuwa inasimama inasema kwamba ninyi mnaleta ukabila, nyinyi mnaleta ukanda, nyinyi sijui mnaleta kitu gani, lakini mbona Mheshimiwa Rais Kikwete sasa hivi anazungumza hamumwambii? Ndiyo! Ilikuwa haki yetu! Mimi wa kwanza kuwalaumu Wanasheria. Kwa kweli ifikie mahali tuwawajibishe kwa jinsi ambavyo wanalipeleka Taifa letu kubaya. Sasa hivi tuanze kurudia Mikataba hii, lakini nchi hii imeporwa raslimali yake yote bila manufaa kwa wananchi wetu. Sisi tunaotoka kwenye maeneo ya madini tunaelewa. Sisi tunaotoka maeneo yenye wachimbaji wakubwa tunaelewa.

Kwa mfano, Nzega. Nzega ulikuwa Mji maarufu sana wakati wa wachimbaji wadogo wadogo. Lakini walipokuja wachimbaji wakubwa, tukapewa matumaini kwamba tutafanya hili, tutapewa maji, tunaweka na barabara za lami na mambo mazuri utadhani unaambiwa kwenda mbinguni. Matokeo yake, biashara hakuna. Wanaagiza hata vitunguu na nyanya kutoka nje, lakini ukiangalia bei ya dhahabu toka mwaka 2001 nimeangalia kwenye *internet* ilikuwa Dola ya Kimarekani 265.90. Leo hii Julai, 2006 ni

Dola 725, imepanda maradufu. Lakini kile kinachopatikana kwa wananchi watakwambia gharama za uendeshaji zimepanda, gharama sijui za nini zimepanda hawana lolote, ni waongo! Wa kuwalaumu zaidi ni hao hao kama sio Wanasheria, ni nyinyi ambao mmekaa mbele watu wa Serikali. Kwa sababu gani?

Mheshimiwa Spika, mikataba hii imewaachia uhuru wa kutosha Wawekezaji wafanye wanavyotaka. Imewaachia uhuru wa kutosha wa misamaha, imewaachia uhuru wa kutosha achimbe, apakie, asafirishe auze ndiyo akupe *return.* Hivi mfanyabiashara gani mjinga atakwambia ukweli? Ni kichekesho! Anapakia mwenyewe, anasafirisha mwenyewe, anauza halafu ndio anakuletea *return!* Nchi nyingine hawafanyi hivyo! Ukiangalia kweli, mrabaha nchi zote ni asilimia tatu na asilimia tano kwa almasi. Mrabaha ndio uko hivyo karibu nchi zote. Lakini wenzetu wako makini kwenye misamaha na kwenye usafirishaji. Leo anapakia mwenyewe, anasafirisha mwenyewe, anauza mwenyewe halafu anakuletea *return,* hawezi kukuambia ukweli.

Kuna Shirika la *South Africa* moja la kwao sijui liko kwa niaba ya Serikali! Linapofika kule, akishauza, anaangalia *return* zao. Hivi kweli Mzungu, wewe Mwafrika akuonee huruma akwambie ukweli hapa ndio pa kwanza ambako kuna ubovu. Kwa nini isiwepo *TRA* ikaangalia amepakia nini, akawepo kwenye kusafirisha aone amesafirisha nini, akawepo kwenye kupokea, amepokea nini na imeuzwa nini? Hapo ndio tutasema kwamba madini yetu yatatunufaisha. Lakini vinginevyo, hapa tunawanufaisha wawekezaji Wazungu. Wazungu hawatupendi sisi Waafrika hata siku moja! *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madini yako Tanzania. Kwa mfano *Tanzanite* iko Tanzania peke yake. Lakini sisi Tanzania kwa jinsi ambavyo Wanasheria na Wanasiasa wa Serikali wanaokaa mbele ambako hatuko makini, bado mnajitoa kwa asilimia mia moja wafanye wanavyotaka. Wakati gani wewe Mtanzania ungeweza kuingia ubia wa kuwa na rasilimali ya ardhi? Wao hawana madini! Ingekuwa madini ni Kiwanda cha Kutengeneza Sabuni, wangeweza kutengeneza huko huko. Lakini kwa sababu hawana madini, wanakuja kwetu. Kwa sababu hawana madini, wana fedha. Sisi hatuna fedha, lakini tuna madini. Mwalimu Nyerere aliacha madini ili tupate akili, lakini tumekuja sisi sijui akili yetu ikoje, tunawaachia hivyo hivyo yalivyo. Mwalimu Nyerere angerudi hapa angetusuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasema kwa uchungu sana kwamba, maeneo yetu ya Kanda ya Magharibi, narudia tena, sijakosea maeneo yetu ya Kanda ya Magharibi Mungu ameyajalia kuwa ni maeneo ambayo yana madini kuanzia Tabora, Shinyanga, Mwanza, Kagera na Sumbawanga. Ni maeneo ambayo yamejaliwa na Mwenyezi Mungu kuwa na madini. Mungu ana sababu yake! Lakini maeneo hayo kwa jinsi ambavyo yametelekezwa na Serikali, tutaachiwa mashimo. Aibu!

Mheshimiwa Spika, mimi ningependekeza kwanza yafuatayo kabla sijaendelea vizuri zaidi: La kwanza, napendekeza ukubali Tume iundwe na Bunge washiriki kuingia kuona Mikataba hii. Naomba hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama unaona Kanuni ina matatizo, mbona huwa tunatengua Kanuni nyingine za kuwaruhusu watu waingie? Tutengue Kanuni! Kama kweli tuna uchungu za mustakabali wa nchi yetu, tafadhali sana kubali Waheshimiwa Wabunge waingie kusaidiana na hao Wanasheria na Serikali. Tukiwaachia tu Serikali peke yao, tutakuja kulaumiwa. Tunaokuja kupata adhabu ni sisi wanasiasa. Kwa sababu wananchi wanakutegemea Mbunge wao utakwenda kuwatetea. Wanakutegemea Mbunge utakwenda kuwasemea, kumbe kwenye Mkataba haumo.

Mheshimiwa Spika, naomba hili la kwanza, ukubali kama ni kutengua Kanuni, tutengue ili Tume ya Bunge iundwe ili tuweze kusaidiana kuona kwamba maslahi ya Taifa ni maslahi ya Watanzania wote.

Mheshimiwa Spika, la pili, nilikuwa naiomba Serikali kwamba, baada ya kukubali wawekezaji kulipa kodi ya Dola laki mbili, mimi kwa Nzega bado sijakubali. Kwa sababu wachimbaji wa Nzega wameanza kuchimba mwaka 1998. Hapa nataka nilipwe *areas*. Haiwezekani tukalipwa Dola laki mbili ikawa basi, Dola laki mbili ni nini?

Mheshimiwa Spika, kwa bei ambayo nimekwambia hapa ya dhahabu ilivyo, hawana hasara. Dola laki mbili kwao ni *penalty.* Kwa hiyo, hapa nataka kieleweke. Lazima Halmashauri ya Nzega walipe *areas,* hapo ndipo tutaelewana. Haiwezekani sisi tumekaa pale, wako wafanyakazi wa Tanzania pale wananyanyaswa sio kawaida, mshahara anaopata *Engineer* Mtanzania ni mdogo kuliko anaopata Mzungu. Mshahara anaopata Mtanzania ni mdogo kuliko wanaolipwa wenzao weupe. Sasa angalau tumeshapata Serikali inasikia kulipa Dola laki mbili, hapa mimi sijakubali, naomba tulipwe *areas* ili iweze kufanana na madhara ambayo yametokea kwenye Mji wetu wa Nzega. Hilo la pili. Kwa hili Mheshimiwa Msabaha kwa kweli unanijua. Nitasimamia mpaka mwisho tuone kwamba hapa *areas* wanalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la tatu, tuweke Kanuni au utaratibu huu wa kuweka Wakala wa kuangalia mauzo ya madini kule nje, ukome. Badala yake, *TRA* iweze kusimamia kwa niaba ya Serikali ya Tanzania. Katika hilo nitakubaliana kwa sababu Wanasheria hawa hawa ndio waliotupeleka kubaya. Angalia Mikataba ambayo tunahangaika nayo ya *IPTL*, *ATC*, *TANESCO* na Mikataba ya Madini. Ni hao hao! Kwa hiyo, mimi ningependa mambo mengine tuwe tunaamua, maana yake sisi ndio tumebeba dhamana ya kuwa na Watanzania. Sisi ndio ndio midomo yao kwa niaba ya Watanzania, sisi ndio Wawakilishi wa Tanzania. Kwa hiyo, mambo mengine, Serikali ituambie kwamba Bunge limesema. Lakini ukiangalia tu kwa misemo ya Serikali, watakwambia hii ni siri.

Lakini siri mimi kwenye kura nakosa, haiwezekani. Hapa lazima ieleweke, hapa ndio mwisho wa siri hasa kwenye Bunge lako hili la *standard* na *speed.* Itakuwaje siri kwenye mambo yenye maslahi kwa Watanzania? Itakuwaje siri kwenye mambo ambayo yanawagusa Watanzania? Haitawezekana, haifai.

Mheshimiwa Spika, mimi namaliza ili niokoe na muda wengine wachangie hoja hii ya Waziri wa Nishati na Madini, lakini kwa kweli bado sijakubali.

Mheshimiwa Spika, hapa naomba Bunge lako likubali kuunda Tume, likubali kuwa na sisi Wabunge kwa sababu ndio Wawakilishi wa Tanzania ambao tunakaa nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MHE. FAUSTINE K. RWILOMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi, nami nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Naomba kwa ruhusa yako niwe pamoja na Mheshimiwa Msabaha. Juzi tarehe 15 Julai, 2006 alikuwa Buhemba na jana tarehe 16 Julai, 2006 nasikia walikuwa Songosongo wanaangalia mambo ya Nishati na Madini. Mimi ni Mwalimu, naomba nimhamishe kitaswira Mheshimiwa Msabaha sasa hivi twende Geita. Sasa tuko kwenye ndege tunafika pale Geita.

Mheshimiwa Spika, naomba ruhusa yako nimfikishe Geita Mheshimiwa Msabaha. Alifika pale mwaka 2002, alikuta milima. Sasa hivi tuko Geita, Mheshimiwa Msabaha angalia kulia na kushoto hakuna milima, milima imekutana sasa hivi Geita. Kulikuwa na miti mirefu sasa hivi ni vumbi, Mheshimiwa Msabaha. Sasa tutoke Geita, ule Mto haupo tena, wanasema binadamu hukutana, milima haikutani, lakini milima ya Geita imekutana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpeleke Mheshimiwa Msabaha Katolo kwenye ghorofa alipolala wakati amelala kama anakumbuka *generato*r ilizimika kabla hajaoga ukawa kwenye giza na mpaka leo hawajapata umeme. Tulilala pale tukafanya harambee. Tuko Geita sasa, tunakwenda Rwamgasa. Nakumbuka Mheshimiwa Msabaha tuliongea na wewe na wananchi wa Rwamgasa walikwambia wanahitaji umeme na wanahitaji eneo angalau wapewe eneo moja lililochukuliwa na *East AFrican Mine.* Mpaka sasa hivi lile eneo bado ndio mambo yamepamba moto, wanatiwa virungu wakisogea kule, hawana eneo na hawana umeme.

Tulitoka hapo Mheshimiwa Msabaha tukaenda Nyarugusu. Kumbuka walikuonyesha jenereta pale na pampu ambazo hayafanyi kazi, uliona wananchi wanashindwa kutoa maji kwa sababu ya kukosa umeme. Kumbuka kulikuwa na mashine za kusagia, watu wengi sana walikusanyika walikuomba umeme, mpaka leo hawajapata umeme. Tukaondoka tukaenda Nyakagwe tukapitia Bukoli tukafika Kahama tukaagana. Sasa Mheshimiwa Msabaha nakurudisha hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kuniruhusu nikaenda naye, sasa nianze. Kwa nafasi hii, mimi nina faraja kubwa sana, kubwa kuliko ya miaka mitano iliyopita. Kwa miaka iliyopita nilikuwa mnyonge, nasema hivyo kwa kujivunia Rais wetu Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kuthubutu kuwaambia Wawekezaji kwamba ni wakati sasa waangalie maslahi ya Watanzania. Kwa kweli tulikuwa tunajisikia wanyonge sana. Sisi tuliokuwepo tulinyanyasika, kuna hotuba zilikuwa zinatolewa mpaka tunaonekana kama hii sio nchi yako. Napenda nikupongeze na wewe Mheshimiwa Msabaha kwa hotuba

uliyoitoa *Kunduchi Beach Hotel* juzi. Ile hotuba ilikuwa inagusa, kama Wawekezaji kweli wanawajua Watanzania, watajibu. Lakini kama hawata-*react* kufanya chochote kuwasaidia wananchi walioko kwenye maeneo ya migodi, basi hatuna Wawekezaji, tuna wavunaji. Anakuja, anavuna, anaondoka. *(Makofi)*

Sasa nadhani wapo kama hawapo, watapata taarifa, waone aibu kuishi na wananchi ambao ni maskini. Wilaya ya Geita imesomwa hapa, ni Wilaya ya mwisho, ingawa kuna dhahabu nyingi. Sasa Wawekezaji waone aibu, waone, walituahidi wataweka barabara, wataweka maji, watuletee vitu vizuri vizuri, viko wapi? Mimi nadhani hatuwagombezi waone aibu, mahali fulani waone aibu na Serikali vilevile naiomba ifike mahali fulani ijiulize je, imeshashtuka, tutaomba majibu baadaye kwamba wameshashtuka kiasi gani walipoambiwa Geita ni ya mwisho, ina mikakati gani sasa kuondoa ile hali kusaidia wananchi?

Mheshimiwa Spika, jitihada zinazofanywa na Serikali, naomba iendelee kuwa jasiri. Mimi nilikuwa kwenye Tume, kuna maeneo mengi ya kufanyia kazi na Wawekezaji wetu wanasema hawapati faida, lakini wapo wanaendelea. Wanasema mpaka watakapopata faida ndipo walipe *cooperate tax*. Ukiangalia jinsi wanavyoweka *investment*, wanavyoongeza kununua vifaa na wanavyozidi kuweka mitambo, kwa maana hiyo ni kwamba haitatokea wapate faida. Kwa hiyo, wataendelea kuweka tu na ninaitahadharisha Serikali iangalie sana katika biashara hii ya madini. Biashara ya madini inahitaji akili na uangalizi wa hali ya juu, kwanza yanakwisha na tusijidanganye kwamba tutakuwa kama Ghana kwamba wamechimba miaka mia moja bado dhahabu ipo.

Mheshmimiwa Spika, sasa hivi *technology* imebadilika. Milima inang'olewa! Mlima mzima unang'olewa kwa siku tatu na wanachukua sehemu zilizo tamu tamu. Sasa kama kuna mabadiliko ya kuangalia Mikataba ya kurekebisha, tufanye haraka haraka, vinginevyo tutajikuta tumechelewa. Namshukuru vilevile mwenzangu, amezungumza, lakini ni vizuri kusisitiza. Tumepewa Dola 200, ingawa Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ukurasa wa 24, nashangaa hukutaja mgodi wa Geita katika kupata Dola 200, kodi za Halmashauri. Umetaja Tarime, Biharamulo na Kahama, Geita haimo, lakini nadhani kama hukusahau, nafikiri kuna tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Dola 200 zilizotolewa, mimi najiuliza kwanini zitolewe sasa hivi? Kwa sababu tumezidai muda mrefu na Serikali ilikuwepo. Naomba tusaidieni, tunaiomba Serikali itusaidie kuwaambia wale watu, watulipe *areas* zetu zile za nyuma kama alivyosema mwenzangu. Zile *areas* ni muhimu, hivi misaada tunayopewa ya kwenda unasimama getini unaombaomba mpaka utafute rafiki kule, Mbunge mzima unakaa masaa matatu, *you become a beggar in your country,* kwa kweli hilo hatupendi. Tunaomba tuliangalie. *(Makofi)*

Nichukue nafasi kuwashukuru watu wa *IM Gold*, juzi wemenipa Shilingi milioni 60 kwa ajili ya chakula cha njaa. Wamepeleka fedha nyingine Serikali Kuu na nyingine wameleta kule, nadhani ni mfano mzuri na Wawekezaji wengine wajifunze. Wamelisha mdomo badala ya kupeleka kwenye pua. Wewe unapeleka kule wakati watu, ombaomba wenye matatizo wamekuzunguka! Sasa wenyewe wameanzia pale, nawashukuru kwa

hilo. Tena cha ajabu ni kwamba hawajaanza kuchimba, kwa hiyo, ni moyo mzuri, nadhani kama hawanidanganyi, watakuwa watu wazuri maana wanabadilikabadilika, walikuja wale wengine wakatudanganya kwamba wataweka maji na nini, hakuna kitu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba Serikali ifanye haraka kuangalia hii sheria ya madini. Sehemu nyingine inagandamiza wananchi, sheria ya kumpa mwekezaji Wilaya nzima au nusu Wilaya, akiwa na fedha akiwaambia waondoke, watakwenda wapi? Naomba jibu.

Kwa mfano, mimi nina tatizo la Rwamgasa, Katoro, Kaseme na Bukoli. Limechukuliwa na watu wa *East African Mine*, wana uhalali na sheria, inawaruhusu. Lakini sasa hivi wachimbaji wale wengine wote, nje! Wakulima inabidi wafuate mashariti yao. Sasa wananchi pale wananyanyasika. Sheria inatakiwa iangaliwe na hata wakiwepo kama mwananchi anaishi pale hatakiwi kujenga kitu ambacho ni cha kudumu, anaweka vitu vidogo vidogo, utaishije bila kufanya *development* katika nchi yako? Mtu unampa masharti eti ni *co-existence*, *co-existence* gani, wewe unafanya mambo makubwa, mimi unaniambia tu kwamba endelea kulima mahindi, viazi, mgomba, aah! Huo sikuukuta, ni sheria gani hiyo? *(Makofi)*

Mimi nadhani kuna mambo mengi sana ya kuangalia na mahusiano katika migodi sio mazuri. Kwenye Tume niliyokuwemo, tulipendekeza kwamba Madiwani, Wenyeviti wa Kamati, *DC* na watu wa Madini pamoja na Mkurugenzi na Viongozi wengine, washirikishwe katika Kamati ile na watambuliwe na sheria. Lakini sasa hivi *DC* akienda kule kwenye mgodi hata akipigwa risasi hakuna sheria inamlinda na Mbunge akienda kule hakuna anapotajwa. Kwa hiyo, naomba katika kurekebisha, hilo liangaliwe. Tu-*encourage local sourcing*, vyakula vinunuliwe hapa, vile vinavyotoka nje au vitu vyovyote vinavyotoka nje, viwekewe kodi kubwa hata mafuta yawekewe kodi. Mbona ukianza tu kabiashara kadogo unapigwa kodi? Kwanini hawa wanapewa msamaha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine, naomba Serikali nayo iimarishe miundombinu, sio kudai tu kodi. Sasa hivi Nyarugusu kuna mgodi wa *IM Gold,* utaanza nafikiri mwaka 2007. Ni mikakati gani imeanza? Mnakusudia kupeleka umeme Bukombe, sasa umeme unakwenda juu, mpaka Bukombe, kwa wananchi huku chini hakuna. Lakini ukipitisha umeme Bukoli, ukapitisha umeme Nyarugusu ukapeleka Katoro, pale utafanya biashara. Sasa sielewi wanauchumi wenu wanafanya nini? Unapeleka tu, unaacha bila kusaidia kule umeme unakopita! Naomba umeme upite pale. Mheshimiwa Msabaha nimekupeleka kule kwa njia ya taswira, baadaye kwenye vifungu naomba unisaidie ni lini umeme utashuka pale wakati unapeleka Bukombe?

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba suala la Meremeta. Meremeta hatima yao ni ipi? Nimemwona Katibu Mkuu Wizara ya Ulinzi, akasema, watalipwa mwezi Januari na Gavana wa Benki Kuu wakasema watalipwa. Lakini wale watu wanateseka, wamekaa pale hawalipwi, hakieleweki kipi kinachoendelea, nitapenda nipewe jibu.

Naomba sana, kwa sasa hivi wakati mnalifanyia kazi, wananchi wa Rwamgasa na wananchi Nyarugusu, wachimbaji wadogo ambao sehemu kubwa imechukuliwa na *East African Mine*, ni eneo kubwa wamechukua, basi wafikirie sehemu zile ambazo hazitafanyiwa kazi wawaachie wananchi na wenyewe hajihangaikiea pale. Ajira pale itawasaidia. Naomba sana watu wa migodi oneni aibu kuishi na watu maskini. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Nishati na Madini. Lakini kabla ya kutoa mchango wangu, ningependa nitumie nafasi hii kutoa salamu zangu za shukrani kwa niaba ya familia ya Profesa Chachage, ndugu na marafiki kwa wale wote waliotoa salamu zao za rambirambi, waliochangia kwa hali na mali, walioshiriki kwenye mazishi ya Marehemu ya Profesa Chachage ambaye alikuwa mpigakura wangu. Lakini zaidi ya yote ningependa kutoa shukrani kwa Rais, Mheshimiwa Jakaya Kikwete na Mama Salma Kikwete kwa heshima waliyotoa ya kwenda kutoa heshima za mwisho kwa Marehemu Profesa Seith Chachage. Wazazi, ndugu na familia wamepata faraja kubwa sana kwa kitendo hiki, kimeonyesha ni kwa jinsi gani Rais wetu ni Mkuu asiye na Makuu na anathamini watu waliomweka madarakani. *It is a loss, a big loss and irreparable loss. Prof. Seith Chachage is dead, long leave Chachage*.

Mheshimiwa Spika, baada ya salamu hizo, ningependa kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wote wa Wizara hii na Mashirika yake, kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendeleza nchi hii hasa kupitia Shirika la *TANESCO*. Shirika la *TANESCO* limetoa mchango mkubwa sana, sidhani kwamba kuna Shirika kama *TANESCO* katika Bara la Afrika lililofanya kazi kubwa kama Shirika la *TANESCO*, licha ya matatizo yake. Wakati mwingine, tunajali zaidi matatizo bila kuthamini kazi kubwa zinazofanywa na Mashirika yetu. Shirika hili linapata matatizo mengi ya kutopata mtaji wa kutosha na fedha za kutosha, lakini kazi zinazofanywa na Shirika hili kwa kweli ni kubwa na huenda kwa njia nzuri tutatambua baada ya kulinyonga kama tulivyonyonga baadhi ya vyombo vya umma katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 1947, wakati nchi ya India inapata uhuru, Neru, Waziri Mkuu wa nchi ya India alipita kwenye Mitaa ya Miji ya India akiwaelezea Wahindi kwamba walikuwa huru. Lakini raia mmoja wa India ambaye alikuwa haoni tofauti aliuliza swali: “Neru, mbona sioni tofauti kati ya jana wakati tuko chini ya Wakoloni na leo sasa uko wewe Neru, mzalendo mwenzetu?” Neru akajibu kwamba: “Tofauti ni hiyo, kwamba leo unaweza kuuliza maswali kama hayo kwa Kiongozi Mkuu wa nchi yako. Ungeuliza wakati ule kabla ya uhuru ungewekwa ndani.” Sasa huenda hii ni *spider* moja katika nchi huru kwamba uwe mpinzani, uwe nani unaweza ukatoa mambo yako na ukavumiliwa wakati mahali pangine usingevumiliwa. *(Makofi)*

Nalisema hili kwa maana kwamba, pamoja na lengo la kukosoa, tulenge kujenga. Umaskini wa nchi hii tunaujua. Kabla ya karne ya 19 au wakati wa karne ya 19, Bara la Afrika lilijulikana kama Bara la Giza *(Dark Continent).* Leo hii kama ungepata nafasi ya kutembea kwa ndege usiku, utembee dunia nzima, ungeona Bara la Afrika ndilo Bara

ambalo linakosa mwanga au liko kwenye hali ya giza kuliko mabara yote duniani. *It is the darkest continent!* Halina umeme! Labda kidogo Afrika Kusini na upande wa Afrika ya Kaskazini. Lakini ni Bara ambalo linakosa umeme kuliko mabara mengine yote katika dunia.

Kwa hiyo bado ni *dark continent,* kwa maana ya kukosa umeme, kwa maana ya kukosa mwanga, lakini vile vile kwa maana ya kukosa maendeleo kwa maana ya teknolojia, kwa maana ya mambo mengi tu. Kwa wakati ule liliitwa *Dark Continent* kwa sababu habari zake zilikuwa hazijulikani Ulaya na watu wake walikuwa hawajui kusoma na kuandika. Lakini bado ni giza! Liliitwa *Sindelela* ya dunia iliyoendelea na leo bado ni *Sindelela* ya dunia inayoendelea. Kwa hiyo, ningeomba na kushauri Serikali kwamba Shirika hili lipewe nguvu na tusipolipa nguvu litakufa na likifa hatutapata mbadala kwa sababu uzoefu wake ni mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa katika hili tuseme tu kwamba umeme ni nyenzo muhimu ya maendeleo na mahali pengine kigezo kikubwa cha kupima maendeleo ya nchi ni kutazama wanavyotumia umeme. Sasa kwa sisi hapa, umeme tunaotumia unatokana kwa kiwango kikubwa na maji. Kuna watu wanadadisi chanzo hiki, lakini ningependa kuwashauri kwamba tusipokuwa na vyanzo ambavyo ni endelevu kama vile maji au umeme wa nuru au wa upepo, vyanzo hivi vingine sio endelevu.

Kwa mfano, tunaweza tukaacha maji labda kwa sababu ya tatizo hili la *global warming*, lakini chanzo kama cha makaa ya mawe nacho sio endelevu, ni kama chanzo cha mafuta ya petroli. Hivi sasa hofu ya dunia ni kwamba, baada ya mafuta kwisha tutaendeshaje mashine zetu zinazotegemea petroli? Hii ndiyo hofu kubwa ya dunia. Wengine wanafikiria kwamba labda tutatumia nguvu ya jua, lakini haijulikani. Lakini chanzo ambacho ni rahisi na cha kuaminika ni maji. Kwa hiyo, suala la kutunza vyanzo vya maji ni suala la kuhakikisha kwamba tuna chanzo cha kuaminika cha kutupatia umeme ambao ni endelevu. Vinginevyo, tutamaliza makaa ya mawe, tutamaliza mafuta, tutajikuta tena tumerudi kwenye giza. Afadhali sisi Waafrika tumezoea giza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini fikiria hali inavyokuwa bila ya umeme humu ndani. Teknolojia yote sasa inatumia umeme na bila umeme hakuna maendeleo na sasa hivi tunaomba umeme uendelee Vijijini, lakini kwa muujiza gani?

Mheshimiwa Spika, *is a paradox.* Nchi tajiri kama Tanzania, ndiyo nchi inayoongoza kwa umaskini katika dunia. Ni nchi tajiri, lakini watu wake ni maskini na ni maskini kwa sababu ni maskini na watabaki maskini kwa sababu ya umaskini wa kufikiri wa ku-*device* njia ambazo zitawasaidia kujiokoa katika hali hii ya duara la umaskini. Inahitaji kufanya maendeleo katika mazingira haya. Lazima uwe *liberals* kwa maana nzuri zaidi. Lakini kama utaamua kufanya maendeleo kwa ku-*maintain status* hiyo hutabadilika. Kwa sababu katika dunia ya sasa, hakuna kitakachodumu isipokuwa mabadiliko *(nothing injures except change)*. *(Makofi*)

Vyanzo ambavyo sisi tunaweza tukavifanya kama ni vyanzo vya kuaminika ni umeme wa maji, vilevile tukatumia umeme wa makaa ya mawe ambao vilevile ni wa

muda. Umeme wa gesi sawa, nao ni wa muda, lakini wataalam wengine wanatuuliza, hivi kama tuna wazo la kujenga kiwanda cha mbolea na hiki ni chanzo kikubwa cha maligafi ya kutengenezea mbolea halafu tunachoma: Je, isingekuwa vizuri kuelekeza nguvu yetu kwenye vyanzo vingine bila kuathiri lengo letu la kueneza umeme katika nchi yetu hii? Ni mawazo ambayo hayawezi kukubalika au kupendwa, lakini ndiyo ukweli kwamba kama unajenga kiwanda cha mbolea halafu tunachoma malighafi muhimu kama hii, kwa wenzetu waliondelea wangetushangaa, lakini kwa sisi tuko maskini. Mtu maskini ni mtu aghali sana. Anaomba kila kitu, anaomba kiatu, anaomba suruali, shati, chakula na maji. Ukimwuliza *what is your priority,* anashindwa kujibu kwa sababu vyote ni muhimu, lakini vyote hana. Kwa hiyo, ndiyo maana anashia hata kuchoma gesi ambayo ni malighali muhimu kwa ujenzi wa kiwanda.

Vilevile, umeme wa upepo, nchi yetu hii imejaliwa kuwa na upepo mwingi. Hiki ni chanzo kikubwa sana katika chanzo cha umeme katika dunia ya sasa. Umeme wa miti, kule Njombe nadhani Waziri amesema hapa, umeme kutoka miti tunayoipanda, watu wanapanda miti inakuwa ni chanzo cha umeme ambao ni endelevu maana kinakuwa sio kama *source* nyingine ambazo zinatoweka. Katika mazingira haya ambayo tuna tatizo la *global warming,* kufikiri ni kazi na ni jambo la lazima, lakini watu hawataki kufikiri. Kufikiri kunaleta mashaka, kwa hiyo, ndiyo maana watu wanataka kunakili tu mambo yaliyopo kama *robot,* kwa sababu kufikiria ndiyo kunafanya useme mambo usiyokuwa na uhakika. Watu wanataka kufanya mambo waliyo na uhakikanayo. Kwa sababu hiyo, hawafanyi uvumbuzi kwa sababu kuvumbua lazima ufikiri mambo ambayo hayapo. Sasa tukifanya hivi katika nchi yetu hii na katika mazingira haya, kwa kweli hatuwezi kwenda mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, ningepanda niishikuru Wizara kwa mambo makubwa matatu, moja kwa kushusha umeme pale Makambako ambao utaenezwa katika Vijiji vingi vya Wilaya ya Njombe pamoja na maeneo ya wakulima wa chai.

Sasa kwa upande wa chai tunapenda na tunaomba Wizara ieneze umeme kwenye eneo la Idamba ambako wananchi wananuia kujenga kiwanda na vilevile kwenye maeneo yenye Shule katika Wilaya ya Njombe kusudi nyenzo hii itumike katika kufundisha, kwa sababu bila kompyuta kwa Shule za sasa, hawa watu watakuwa na elimu isiyo na maana. Hawawezi kupata Elimu ya Sekondari kwa kukaa kwenye majengo tu yaliyoandikwa *Secondary* au *by osmosis* ni lazima wapate nyenzo ambazo zitasaidia kupata elimu hiyo. Hilo ni moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili, maeneo ambayo umeme unapita hivi sasa, kwa mfano katika Vijiji vya Mhaji, Igima, umeme umepita juu halafu unawasha mbele. Hawa watu hawaelewi. Ndiyo maswali mengine ambayo baadhi ya Wabunge wanauliza, tuwe *reasonable* na tujaribu ku-*solve* maswali ambayo kwa kweli tunayaweza.

Baada ya hayo, kulikuwa na sheria tuliyopitisha inayosema kwamba kama mtu anaanzisha mradi wake au Kampuni binafsi, Serikali itachangia asilimia 25 ya gharama za ujenzi wa mradi huo. Tulipitisha sheria ya namna hiyo hapa. Nauliza hivi, wapi

tumechangia nguvu ya namna hiyo? Kwa sababu Njome kuna watu kadhaa, Wamisionari na wengine wako tayari kufanya kazi hii na wangetaka kujua kama wakianza mradi wa namna hiyo; je, Serikali itachangia chochote?

Mheshimiwa Spika, baada ya salam hizo ningependa nikushukuru kwa kusema kwamba, eneza umeme kwanza na mengine yote yatafuata. Asante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Asante sana na sasa msemaji wetu wa mwisho kwa asubuhi hii ni Mheshimiwa Beatrice Shellukindo.

**MHE. BEATRICE M. SHELLUKINDO:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushukuru tena kwa kunipa nafasi kwa mara ya pili katika kuchangia katika Bajeti hii. Awali ya yote, nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa kuteuliwa kwao katika Wizara hii nyeti na muhimu sana hasa kwa wananchi wa Wilaya ya Kilindi. Lakini la pili, basi pia niwapongeze kwa kazi nzuri sana na nzito ambayo wanaifanya katika hali ya mikingamo mikubwa.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya madini kwa upande wangu hayako kwa uongozi kama Waziri na Naibu Waziri kwa sababu nimeona ushirikiano wao wa ajabu kwangu mimi na kwa Wilaya ya Kilindi. Lakini matatizo yako kwa Watendaji wao wengi, kuanzia Wizarani hadi chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea kuongea, naomba niwashukuru sana Wawakilishi wangu kutoka Kilindi, Wawakilishi wa wachimbaji wadogo wadogo ambao wamechangiwa na wachimbaji wengine wote waweze kufika hapa siku ya leo kuweza kusikiliza mjadala huu na kuona hatima yao ni nini. Wanasubiriwa warudi na majibu. *(Makofi)*

Siku ya leo kule Kilindi tuna Halmashauri Kuu ya Wilaya *"full council"* lakini kutokana na umuhimu wa Sekta hii imebidi tuache niwepo hapa. Nasema nakusudia kuchangia mambo mawili tu, leo lakini ninasikitika kwamba nimepewa nafasi ya kuwa mchangiaji wa mwisho. Nakusudia kuongea mambo mazito, mambo magumu sana, kanuni haziniruhusu kutaja majina, kwa hiyo, nitaongea nitakavyoongea, lakini nina hakika baada ya hapa, wengi mtapoteza *appetite* ya kula chakula cha mchana, lakini ndio hali halisi ya Watanzania ambayo tunakutana nayo hasa kule Vijijini.

Mheshimiwa Spika, naomba nilitoe wasiwasi Bunge lako Tukufu pamoja na *Chief Whip* kwamba uthibitisho wote uko hapa, mwanzo mpaka mwisho, yote nitakayoyasema na kama utahitaji nitaweka Mezani vilevile. *(Makofi)*

Kwanza kabisa, niishukuru Serikali kwa kunipatia Shilingi milioni 450 kwa awamu hii kwa ajili ya umeme. Ni kweli kabisa tulikuwa na umeme uliokuwa unatoka Handeni, lakini uliishia Kwedi-Boma awamu ya kwanza. Umeme huu upo kwa muda mrefu, lakini cha kushangaza *transformer* hazipo za kutosha. Kwa hiyo, unakuta unapita maeneo mengi, hasa ukizingatia kuna Sekondari ya Mkuyu pale, nguzo zimepita tu na umeme unaendelea mbele, Zahanati maeneo mengine muhimu hakuna *transformer,*

lakini ukifika Kwedi-Boma na kwa wale wachache kwa kweli wanaweza kupata, lakini nilikuwa naomba sana hapa Mheshimiwa Waziri uweze kuliangalia suala hilo. Lakini vilevile ninashukuru kwamba sasa nimepatiwa hizo fedha kwa awamu hii umeme uweze kufika Makao Makuu ya Wilaya. Ninaomba basi kazi ianze.

Mheshimiwa Spika, nimeambiwa utafiti wa awali umeanza, lakini sijawahi kuona gari la *TANESCO* kule wala wale washauri wangu hawajawahi kuniambia gari wameliona na wanashangaa, nikiwaambia utafiti unafanyika.

Lakini naomba iwe kweli basi, ili na mimi nisipate maswali mengi sana ya kujibu. Lakini kwa zile Kata ambazo kama Negero, Kimbe, Kilindi, Saunyi, Masagalu, Lwande mpaka Kikunde na Pagwi ambazo bado hazijapata umeme, basi naomba muweze kutufikiria na sisi tuweze kupata umeme. Lakini kwa upande huo niseme kwamba kwa kweli ninashukuru sana. Msemaji mmoja amesema umaskini wa nchi hii tunaujua, kwa kweli mimi siujui! Nchi hii sio maskini! Umaskini upo kwenye mipango yetu, Viongozi ambao hawana uzalendo na wananchi kukosa uwezeshaji, lakini nchi hii ni tajiri sana, inategemea labda tunaangalia umaskini kwa mkakati upi. Lakini mimi kwa upande wangu sidhani kama hilo lina matatizo.

Mheshimiwa Spika, nije kwenye upande wa madini. Kilindi tuna madini ya aina ya dhahabu, alluvia na vilevile tuna madini ambayo ni vito vya thamani, *gems stones.* Lakini naomba kusema kwamba pale Kilindi hili suala nimekuwa nikilirudia na kurudia kwa sababu ni kilio chetu. Kweli kabisa, hata ukiangalia mapato ya Halmashauri, hakuna mahali ambapo inaonekana madini yanachangia nini?

Kwanza kabisa, viongozi tuseme Afisa Madini yuko Handeni, niliwahi kumwandikia hata Waziri barua binafsi kama Mbunge, nikisisitiza naomba Afisa Madini wa Wilaya ya Kilindi na Watendaji wake pengine itasaidia. Lakini yuko Handeni.

Lakini, hata hivyo jambo la kushangaza, pamoja na madini yote ambayo tumekuwanayo, utashangaa kusikia, mimi ndio maana nilikuwa namwambia Mwenyekiti wa Kamati wa Uwekezaji, kwa kweli mtanisamehe lakini hii Sheria ya Madini imepitwa na wakati kabisa. Sijui walioitunga wakati ule walikuwa na maana gani? Hata kwa wakati ule ilikuwa imepitwa na wakati. Huwezi kuniambia kwamba mnakwenda kutoa vibali vya madini hata kama ni utafiti, eti wale watu wa eneo lile wasijue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kilindi imekuwa ndio tabia, mnasikia eneo hili marufuku sasa hivi limetolewa sijui kwa nani, sijui kwa nani, sasa basi hata hao watu wafanye jambo kwenye maeneo waliyopewa. Kuna watu wameshikilia ardhi pale muda mrefu zaidi ya miaka sijui mingapi na hakuna kilichofanyika, matokeo yake wananchi wa Kilindi wakienda wanaambiwa ni wavamizi, wanapigwa, wanauwawa na mambo na mengine mengi. Kwa kweli, hapana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iangalie sasa, hasa kwa upande wa Kilindi ambako nina ushahidi nako. Vile vile, nilikuwa nataka kusema kwamba hivi karibuni, niliuliza swali hapa Bungeni na Mheshimiwa Naibu Waziri alinijibu vizuri sana,

akanielezea, akataja hizo *prospective licence* zilizotolewa ambazo kule hata taarifa, nilipokwenda kwenye maeneo husika na kuwaambia wananchi na kuonyesha majibu, walibaki wanashangaa.

Sasa mimi nikawaahidi kwamba hakuna mtu yoyote kuja, awe anafanya utafiti wala nini bila kuwasiliana na Kijiji na ule uongozi wa pale wapate kujua hawa ni akina nani na wameiingiaje? Vinginevyo, sisi wananchi wa Kilindi turuhusiwe twende tukachimbe mali ambayo kwa bahati nzuri Mwenyezi Mungu ameiweka kwenye maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo mengi pia yametolewa kiholela, wala sio kwa Wizara ya Nishati na Madini, kwa mfano machimboni kule Masagalu, unashangaa tu asubuhi, unakuta kibao cha mtu kabandika pale kwamba: "Mimi sasa hivi ndio nachimba hapa." Unashangaa hata Kijiji hakijui! Nilikwenda Kata moja ya Negero, nafika pale Mwenyekiti wa Kijiji ananiambia tumeona kibao cha fulani kimebandikwa hapa juzi. Nani kampa hayo machimbo? Kumwuliza Afisa Madini wa Wilaya ya Handeni, hana habari.

Sasa kwa kweli haya mambo tunaomba Wizara ya Nishati na Madini, tunaomba kidogo, siseme kwamba hamko *serious,* lakini naomba sasa muweze kuja kuangalia kwenye maeneo ambapo tunazungumzia umaskini uliopindukia, lakini kuna rasilimali ya kutosha ambayo sisi Kilindi ingekuwa tunakopesha maeneo mengine na sio sisi tunaomba misaada. Ninaomba sana hilo.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli namshukuru Mheshimiwa Rais kwa suala la Mikataba, ameona iangaliwe upya. Nimefurahi sana. Lakini kwa upande wa Kilindi, hivi hii Mikataba kwanza walioshiriki katika kukubaliana na hiyo Mikataba si ndio hao hao wanaoundwa tena kwenda kuiangalia jamani! Yanawezekana hayo? Mimi nina wasiwasi sana wa haki kutendeka. Kweli kabisa nina wasiwasi.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji wakati anasoma hotuba yake, amesema kwamba anakusudia kuunda Tume teule, Kamati au Tume teule, sasa mimi nilikuwa nasema hivi, ninaomba, tafadhali sana wale wadau wa maeneo husika ambako kuna Mikataba, wahusishwe kwa asilimia mia moja kwenye kufanya hiyo kazi ili tupate ukweli wa mambo yote.

Sasa nakuja kwenye yale ambayo nasema yanasikitisha. Msione wale watu wamechangiwa wamekuja hapa ndugu zangu, Machimbo ya Mafulila, nimeyazungumzia mara kadhaa, miongoni mwa viongozi waliokuja, kuna baadhi yao ambao waligundua mwanzo hii dhahabu iko mahali pale, wakafanya utaratibu wakawasiliana na waliowasiliana nao wakapeleka mpaka *samples*, mpaka *Siamic Dar es Salaam* na kadhalika na utafiti wao ukafanyika. Sasa katika hatua za kuanza kutafuta kupata kibali na kuwasilina na Wizara ndipo mambo yalipoanza. Ndugu zangu inasikitisha.

Nchi iliyopata uhuru miaka zaidi ya 40, majibu mnayopata kwa Sekta ambayo watu mnajua kwamba ingeweza kuwasaidia, hawa watu wakaanza kuzungushwa na

kibali, nenda rudi, nenda rudi, wakajiunga wakawa kikundi cha wachimbaji 361, wakaenda, wakarudi. Mara ya mwisho wakaenda wakitegemea kupata ile hati, wakaambiwa nyie rudini kule kwenu tutawasiliana nanyi.

Mheshimiwa Spika, hapa itabidi ninukuu kwa sababu ni nzito kidogo, kwa sababu inabidi nitaje majina. Mimi ninataja taarifa yao waliyoileta. Ni kwamba Wanakwenda kule wanamkuta Mkuu wa Wilaya, wanamkuta Mbunge wakati huo sio mimi, wanamkuta na Afisa wa Kanda Bwana John Bosco, wapo pale Kijijini wamekuja na watu wa *Ashanti Anglo Gold*, wanasema hiki hapa ndicho kibali chenu na baada ya kibali chenu, tumewaletea Wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, palifanyika utafiti, yakaonekana yale maeneo ambayo yana dhahabu zaidi, basi wapewe Wachimbaji wadogowadogo. Jamani, siyo wizi huo! *Plot* 9, *10* zinafahamika na mpaka hata mwananchi wa kawaida, eti zile sasa ndiyo wanapewa Wachimbaji wadogo wadogo kisha wanaambiwa siyo ya kwenu, tumewaleteeni Wawekezaji hawa hapa. Wakaanza kushangaa! Usiku, usiku akachukuliwa Mtendaji wa Kata, Mtendaji wa Kijiji na Mwenyekiti wa Kijiji, wakapelekwa Makao Makuu ya Wilaya. Usiku kwa usiku, kwa misingi ambayo siwezi kuitamka hapa ndani. Wakafika pale, wakasaini. Walivyorudi sasa, wakafika, inasema hapa kwenye taarifa yao, naomba ninukuu: "Baada ya hapo, walivyokwisha kusaini, ndipo Mkuu wa Wilaya akaja kuwafukuza watu wote tuliokuwa tunachimba kwenye eneo tulilotafiti na kusema hapa ni mahali patakatifu, huwezi kuwaachia mbwa wakapaharibu."

Mheshimiwa Spika, niwie radhi. Mimi huku ni nyumbani. Inafika hatua hiyo, watu wanadai haki yao, wanaambiwa maneno hayo. Ikaendelea, wakaendelea kufuatilia, ndipo anasema katika taarifa yao, wanasema hata hivyo mawasiliano kati ya Mkuu wa Wilaya, yaani hawa viongozi na hicho kikundi chao waliamua kwenda. Hata hivyo, mawasiliano kati ya Mkuu wa Wilaya, Mbunge na huyo Bwana John Bosco pamoja na Diwani na Maafisa Watendaji wa Kijiji, hayakufua dafu. Hawakuwa karibu mno, huku sisi wadau wa madini tukiachwa bila kupewa kipaumbele tulichokitarajia, huku Mkuu huyo wa Wilaya akisema kwamba: "Hakuna takataka itakayothubutu kuhoji juu ya maamuzi yangu, hata Mkuu wa Mkoa Jaka Mwambi au Waziri wa Nishati na Madini, hana mamlaka ya kuhoji juu yangu."

Mheshimiwa Spika, hawa ndio viongozi wetu huko chini, ndio maana nasema Waziri hana tatizo wala Naibu Waziri, ni hawa Watendaji mamluki na wako wengi mnaendelea kuwafuga pale ndugu zangu. Jamani, hebu badilisheni, wamekuwa sasa wanafanya kwamba hii ni haki yao.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli, mimi ninaomba sana, hawa watu wameleeza kwenye barua yao ambayo ni ndefu sana na maelezo yao ni mengi, niseme tu kwa upande wangu wakati nakwenda kuomba kura wakati wa kampeni, wananchi waliniweka kitimoto, wakasema hatukupi kura mpaka suala hili utubadilishie. Makaburi ya babu zetu yako huko na mila zetu unazijua. Wazee wakasema sisi hatukubali, hatuwezi kukupa kura. Nilifanya kazi na kutoa ahadi kwamba nitashughulikia, wanipe tu kura zao.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri hapa alipojibu swali langu alisema kwamba Wizara yenyewe ikishatoa kibali kama ilivyotoa, yaliyobaki ni ya kwetu sisi ambao tumeingia Mkataba. Kwa hiyo, twende Mahakamani na kadhalika. Naomba niseme, ni kweli pengine taratibu zinasema hivyo, lakini uangalie ukweli wenyewe. Kwanza, hii ni rasilimali ya Serikali, lakini la pili basi, hawa watu wa Mafulila wana uwezo gani? Wana elimu gani ya kuweza kuwapeleka hawa *Ashanti Anglo Gold* kule? *Ashanti Anglo Gold* wametoa lori linaitwa *Mafulila Mining Company*, mara naliona linatoka Mwanza linaleta mahindi kuja Dar es salaam, mara linakwenda wapi, hata wale watu hawalioni hilo lori. Wameambiwa wanapewa Dola 30,000 mwaka wa kwanza, mwaka wa pili 40,000 na kadhalika. Lakini, za kufanya nini na ziko wapi?

Mheshimiwa Spika, ndio maana nasema, jamani, hata huu utafiti tuuangalie. Utafiti wa muda gani? Hawa wananchi wa kawaida walikuwa wanakwenda na nyundo, wanagonga, wanatoka na dhahabu ya kutosha. Leo hii mtu anakuja na mashine kubwa, ataendelea kuchimba na tunaona magari yanavyoondoka na mali, yanaingia, yanatoka. Baadaye atasema aah, kwa kweli mali haitoshi, ni kidogo. Kumbe ameshavuna ameondoka.

Mheshimiwa Spika, mimi kwa kweli naomba Mheshimiwa Waziri nirejee tena, tunaomba Afisa Madini Wilaya ya Kilindi aweko mapema iwezekanavyo ili tuweze kufanya kazi kwa usahihi zaidi. Lakini vile vile kuna watu wengi na humu ndani ya Bunge, pia wako wengi wameomba machimbo Kilindi, wanangoja mwaka wa tatu sasa. Kisa ni kwamba, hakuna fedha za kwenda kupima yale maeneo. Imeshaandikwa barua Wizara ya Nishati na Madini. Ninaomba jamani katika angalau mwezi mmoja, tupate hizo fedha kwa sababu tunachangia hela nyingi sana kwenye vibali, hawa watu wametoa hela zao ili angalau vile viwanja vipimwe sasa, watu wagawiwe, tuendelee na kazi za maendeleo.

Mheshimiwa Spika, lakini mwisho kabisa, ninaomba tena, wananchi wale wa Mafulila pale wanasubiri kuondoka na jibu. Tunaomba Wizara itoe tamko na mimi sitaunga mkono hoja kwa sasa, mpaka hapo nitakaposikia wale watu wanaondoka na jibu gani, kwa sababu hamwezi kutuachia. Mmesema mimi Mbunge nishirikiane nao, sina uwezo huo! Tunahitaji Mwanasheria na hii Sekta mnaijua ugumu wake. Pia, tunahitaji ujuzi. Kwa hiyo, ninaomba nipate jibu kamili kutoka Serikalini itaingiliaje kati ili hawa Ashanti ikiwezekana hata waondoke kwa amani, yale maeneo yagawiwe hata hawa wengine walio humu ndani na wananchi wengine walioomba wagawiwe ili haki iweze kutendeka.

Mheshimiwa Spika, siyo kawaida sana, lakini naomba nimalizie kwa kuwapongeza sana wafanyakazi wote wa Wizara ya Madini, kwa kweli wanatoa ushirikiano hasa kule kwangu Handeni, japo wako Handeni, lakini Mheshimiwa Mangowi na Timu yake kwa kweli wametoa ushirikiano mkubwa wa kifanya kazi chini ya mazingira magumu kama hao viongozi niliowatajia hususan *DC*.

Kwa hiyo, ninaomba sana niwashukuru. Baada ya kusema hayo, ninaishia hapo, hoja nitaiunga mkono baada ya kupata majibu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautuwezeshi wachangiaji hoja kuendelea tena kwa sasa. Nataka tu nisome majina ya Waheshimiwa watakaochangia saa za jioni ili wajiandae na waweze kuwepo.

Saa 11.00 tutaanza na Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula, halafu Mheshimiwa Anna K. Malecela, atafuatia Mheshimiwa Dr. Harisson G. Mwakyembe, Mheshimiwa Eustace O. Katagira, Mheshimiwa Dr. Chrisant M. Mzindakaya, Mheshimiwa Dorah H. Mushi, Mheshimiwa Abubakar Khamis Bakary, atafuatiwa na Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka atakayefuatiwa na Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo na hapo naona itakuwa ni saa 01.30.

Kwa hiyo, labda hao wasiwepo ndio wengine hawa kama Mheshimiwa Chacha Z. Wangwe, Mheshimiwa Rosemary K. Kirigini, wanaweza wakapata nafasi. Lakini mkumbuke tu kwamba kwa hoja hii ya Nishati na Madini ni siku mbili.

Kwa hiyo, wale ambao sijawataja, bado nitawataja jioni wale ambao ni wa asubuhi ya kesho.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, kwa kuwa muda uliopo haututoshelezi kuendelea, zimebakia dakika mbili, tatu tu. Kwa hiyo, nasitisha shughuli za Bunge hadi hapo saa 11.00 jioni.

*(Saa 06.58 mchana, Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

**MHE. EMMANUEL J. LUHAHULA:** Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani zangu kwa kunipa nafasi hii, ili niweze kuwa mchangiaji wa kwanza wa bajeti hii, siku ya leo katika kikao chetu cha jioni.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda kutoa pongezi kwa Serikali yetu ya Awamu ya Nne na Viongozi wake wote, chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake mahiri na makini, ulio katika ari mpya, nguvu mpya na kasi mpya. *(Makofi)*

Lakini natoa pongezi kwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji walio katika Wizara hiyo, kwa kuweza kupata muda wa kuandaa Bajeti, ambayo leo tunaijadili na hatimaye inatuelekeza katika ufanisi wa mwaka wetu huu mmoja, tunaouendea na pengine ikawa ni dira katika miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niingie katika Sekta ya Madini. Katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, ibara ya 39 (d) na (e) imetamka kwamba, tutawawezesha wachimbaji wadogo wadogo. *(Makofi)*

Lakini katika ibara hiyo hiyo, kipengele (a) kinasema kwamba, Serikali hii itafanya kila jitihada, kuvutia wawekezaji na kuwaruhusu ili waweze kufungua migodi na sehemu mbalimbali ili tuwe na wawekezaji wakubwa. Katika hili, nilikuwa najaribu kufikiri jinsi gani makampuni yanaingia katika nchi yetu na kufanya utafiti unaochukua muda mrefu sana. Siku ile wakati najibiwa swali langu nililouliza hapa, niliambiwa katika Wilaya ya Bukombe, kuna leseni 145 zilizotolewa, lakini tulisema, yako makampuni yamekaa miaka mingi sana.

Nikawa na wazo kama inawezekana, Serikali iangalie utaratibu wa makampuni haya yanayofanya utafiti, yapangiwe muda maalum, kwa sababu Wabunge tunakaa miaka mitano na Rais anakaa miaka mitano, lakini watafiti wanakaa miaka isiyojulikana. Wanaendelea kusema bado wanatafiti, inawezekana sasa nipo mwaka wa kwanza katika Bunge hili Tukufu, miaka mitano itaisha, bado utafiti utaendelea. Lakini kwa sababu wao wanaendelea, wanachukua vitu, nani anayekwenda kuwahakiki? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika hili wazo langu, nilikuwa naomba Serikali iwapangie muda maalum wa utafiti wao, ili tuweze kujua kwamba, hapo walipokaa kwa muda huu kama hawapati basi waondoke. Kama wamepata basi wanafungua, wanawekeza kitu ambacho kinakuwa na faida katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, lakini upande wa kuwekeza wachimbaji wadogo wadogo, nashukuru nilikuwa napitia kitabu hiki, taarifa ya jumla kuhusu Sekta za Nishati na Madini ukurasa wa 48, Wizara imesema wameunda Kamati ya kuandaa mikakati ya kuwaendeleza wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, kweli naamini kwamba, maeneo yetu mengi yanayo wachimbaji wadogo wadogo, ambao wanahitaji kuwezeshwa. Sasa ni muda muafaka wa kuweza kuwasaidia watu hawa, kwa sababu wamekwisha kuunda vikundi vyao, wengine wamesajiliwa, wana vyama vyao ushirika, lakini wanakosa mitaji na sehemu kubwa ambayo inaweza ikatoa ajira ni sehemu za wachimbaji wadogo wadogo.

Kama tutaamua kuwawezesha kikweli kikweli, usiwe mkakati wa kwenye karatasi, ninaamini ndani ya miaka mitano, nchi yetu itakuwa imefikia sehemu nzuri sana na hata maisha bora kwa kila Mtanzania yatawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee wachimbaji walioko katika eneo la Matabe. Katika tamko la Serikali, ambalo lililotoka Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, likitaka wachimbaji wadogo wadogo katika maeneo ya Matabe waondoke, kwa ajili ya uchafuzi wa mazingira. Lakini wachimbaji wale, naamini nilipokwenda pale kwenye kampeni, walikuwepo watu wengi sana karibu 100,000 na watu wengi wao wanaishi katika Wilaya ya Bukombe ingawa Matabe iko Biharamulo. Hawa watu maisha yao na uchumi wao, wamekuwa wakitegemea sana uchimbaji.

Niliwahi kushauri hili kwenye Kamati, hata juzi kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, niliandika mchango kwa maandishi nikasema kwamba, kama inawezekana, uwepo mkakati mzuri badala ya kuwasukuma wale watu kuondoka ghafla

na wale watu najua wakiondoka, wote watamwagika pale Ushirombo, Makao Makuu ya Wilaya ya Bukombe watakuwa hawana kazi. Nashauri Wizara husika kama inawezekana, uwepo mkakati, kwa sababu Wilaya ya Bukombe ina maeneo ya Ushirombo na Katente, kuna dhahabu nyingi ambazo wananchi wamekuwa wakichimba siku nyingi lakini hawana vitendea kazi. Pawepo ushirikiano wa Wizara ya Nishati na Madini na Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira, ikiwezekana watu hawa wafanyiwe *mobilization* ili waweze kupatiwa vifaa hivi. Lazima watu watafanikisha, wakishapata watu wa Matabe, wataondoka vizuri tu tena kwa hiari yao na hapatakuwa na vurugu yoyote, ambayo inaweza ikajitokeza na kuwatia katika shida na matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee kuhusiana na makampuni makubwa, hasa nioongelee Kampuni ya TULAWAKA. Tunasema kwamba, makampuni haya yanatakiwa yasaidie wananchi wanaozunguka maeneo hayo. Lakini nashukuru hata kwenye kitabu hiki, taarifa ya jumla nilikuwa napitia Sekta ya Nishati na Madini, nikaona inasema inaunda Kamati ya kupitia upya Mikataba ya Madini na wakasema upembuzi yakinifu wa Mradi wa Madini TULAWAKA.

Mheshimiwa Spika, unakuta wananchi wanaozunguka maeneo yale, hawapati faida yoyote na makampuni haya. Mimi nasema kwa sababu maeneo ya kule TULAWAKA napafahamu, wananchi wa pale hawana maji, wananchi wa pale barabara ni mbovu, wananchi wa pale hata zahanati hawana. Lakini pia ninafikiri kwa sababu sasa ni wakati mzuri ambapo Mheshimiwa Rais wetu, amesema kupitia upya mikataba hii. Wizara ya Nishati na Madini, iweze kupitia sera zake upya, pamoja na sheria. Ili kabla ya kuwekeza au kabla ya kufungua mgodi sehemu, pawepo na wamiliki wa aina tatu. Kwa sababu wananchi wanaoishi maeneo yale, ndio wamekutwa pale, Mwenyezi Mungu kawapa utajiri ule katika maeneo hayo. Lakini kinachotokea, wananchi wanaweza wakahamishwa, wakapewa *compensation* ambazo ni ndogo sana. Lakini kama wananchi watapewa hisa zao katika eneo hilo na Serikali ikachukua hisa zake na mwekezaji akachukua hisa zake, basi maisha bora kwa kila Mtanzania yatawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa kuishauri Serikali iweze kufanya hivyo na kuliangalia kama inawezekana. Lakini pia ardhi zetu zipimwe, kwa sababu makampuni haya sidhani kama yanaweka mipaka yake halali na kujua kwamba, sasa mpaka huu unaishia hapa, kampuni kwa mfano ya *Barrick* inaishia hapa. Hujui mpaka ni kwa sababu ardhi ile haijapimwa. Naamini kama ikishirikiana na Wizara ya Nishati na Madini, ikashirikiana na Wizara ya Ardhi, ikapimwa ile ardhi ikafahamika, uthamani wake hata makampuni yanapokuja basi wananchi wetu wanaendelea kunufaika.

Mheshimiwa Spika, niombe Serikali iweze kuangalia na wananchi wetu watafika sehemu ambapo watafurahia kuwa na rasilimali ya madini katika nchi yetu. Kwa sababu sasa hivi unaweza ukakuta hata sehemu ambazo wachimbaji wapo, barabara zetu ni mbaya. Wananchi wetu wanahangaika na wakati makampuni yanapita yanaondoka, yanachukua vitu, wakati mwingine hata ajira zinatoka mbali. Napenda kushauri hilo kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, niende katika upande wa nishati. Napenda kuipongeza sana Wizara ya Nishati ya Madini, kwa kukubali kupeleka umeme

Wilayani Bukombe, kwa sababu nafikiri imetenga bajeti kubwa. Nakumbuka wakati nachaguliwa kuwa Mbunge katika Jimbo la Bukombe, kabla ya kuondoka kuja mara ya kwanza Bungeni, nilikaa na Mbunge Mstaafu Mheshimiwa Robert Kaji Mashalla, nikamwuliza kuna miradi gani aliyoianzisha ikaishia njiani na mimi nikaiendeleze. Akaniambia mradi wa umeme, ambapo akasema alikuwa anasaidiwa sana na Mheshimiwa Dr. Ibrahimu Msabaha, akiwa Naibu Waziri kipindi hicho. Wakati naongea naye, akaniambia sasa hivi kwa sababu amekuwa Waziri kamili, naamini atakusaidia zaidi. *(Makofi)*

Nakumbuka miaka mitano iliyoisha, tulikuwa tumeahidiwa Bukombe tutapewa umeme. Sasa tumeanza awamu hii na Mheshimiwa Dr. Ibrahimu Msabaha, yeye ndiye amekamata rungu lote. Naomba umeme ufike Bukombe, naamini kabisa maeneo ambayo yatahitajika kunufaika ni pamoja na Gereza la Kanegele katika *ginnery* ya *Cargil,* Masumbwe, Ushirombo, Uyovu, tukielekeza kuwapelekea Tulawaka. Kwa hiyo, katika hili naamini kwamba, Serikali itakuwa imewawezesha wananchi wake kwa hatua kubwa sana. Haiwezekani nchi ikaendelea pasipo umeme. *(Makofi)*

Jana nilikuwa Dar es Salaam, nilikwenda *saloon* zote nikakuta zimefungwa. Siku moja kuna Mbunge mmoja hapa alichangia akasema, ni nchi gani inaweza ikaendelea wananchi wake saa 12 wanalala? Sasa mimi leo nasema ni wananchi gani wanaweza kuendelea, wakati hawana umeme, *saloon* zao zimefungwa, wanafungua usiku na sisi tumelala? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, ilibidi nilipofika hapa Dodoma usiku nikaenda *saloon*. Lakini ninaomba Serikali, iweze kupeleka umeme Bukombe. Naamini Bukombe tukipata umeme, hakika wawekezaji wakubwa watakuja katika Wilaya ya Bukombe na wafanyabiashara kutoka nchi jirani za Burundi, Rwanda, Kibondo, Biharamulo na Ngara, watanunua bidhaa katika Wilaya ya Bukombe. Katika hali hiyo, Bukombe tutaipanua sana. *(Makofi)*

Nashukuru sana kwa sababu umekusudia hilo na ninaamini kwamba, hamtaniangusha na wala hamtawaangusha wananchi wa Bukombe, kwa sababu ni makusudio. Naomba sana Mungu abariki na kwa sababu wanasema kwamba, Tanzania ni tajiri, kuna mmoja alikataa kwamba, Tanzania si maskini na mimi ninakataa. Uko msemo unasema "ukibadilika unavyosema na ukibadilika unavyoamini na hali yako ya maisha inabadilika." Sasa tukiendelea kuamini sisi ni maskini, tutaendelea kuwa maskini. Bukombe ni tajiri, tunaomba umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ni vigumu kuelewa kwa nini Mheshimiwa Emmanuel J. Luhahula anakwenda *saloon*, basi kwa leo ni Nishati na Madini. *(Kicheko)*

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja. Naipongeza Serikali kwa Hotuba ya Nishati na Madini, ambayo tumeielewa lakini

lazima Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, waelewe kwamba, hii ni Wizara ambayo ni nyeti sana, kwa hiyo, watuvumilie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza, mimi nina masuala mawili tu ya kuzungumza, leo sitazungumza sana. Moja linahusu jimbo langu ninaloliwakilisha na la pili linahusu nchi yangu. Naomba ninukuu barua aliyoniandikia Naibu Waziri wa Nishati na Madini, yenye kumbukumbu Na. CAB 85/241/01. Mheshimiwa Naibu Waziri, aliniandikia barua hii akijibu barua yangu. Nilikuwa nimemwomba aniorodheshee vijiji vya jimbo langu, ambavyo vilikuwa vimeidhinishwa kuwekewa umeme katika bajeti ya mwaka 2005/2006. Mheshimiwa Naibu Waziri, aliniandikia miradi minne. Mradi wa kwanza, ulikuwa Mradi wa Kadando, wa pili ulikuwa ni Mradi wa Parane Miamba, Mpinji, Ivuga, Bwambo, wa tatu ulikuwa ni Mradi wa Mtii, Mtii ni Kata kubwa sana na Mradi wa nne ulikuwa wa Kizerui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Miradi yote hii ilielezwa vizuri sana kulingana na barua ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Mradi wa Mtii ilikuwa ujenzi wa njia ya urefu wa kilomita mbili na kuweka *transformer*, Kadando hivyo hivyo, Kizerui hivyo hivyo na Parane Miamba kule milimani kabisa, Kata kama sita, ilikuwa yote iwe na njia za umeme lakini pamoja na *transformer*. Miradi hii kwa kweli ilianza lakini haikukamilika, kama ambavyo Serikali ilikuwa imetegemea. Mfano Mradi wa Kadando, wananchi walichimba mashimo wao wenyewe, kwa sababu walihamasishwa na *TANESCO,* mwaka mmoja uliopita *TANESCO* ilipeleka nguzo ikazilaza pale. Mwaka mmoja uliopita mvua ziliponyesha, yale mashimo ambayo wananchi walichimba yalifunikwa na udongo na sasa hayapo tena. Mradi huo umeishia hapo hapo ninapozungumzia. Hiyo ni Kadando. Kizerui ni hivyo hivyo, mwaka mmoja uliopita wananchi walichimba mashimo kwa msalagambo wao. Sisi tuna utaratibu wa Msalagambo, mvua iliponyesha mashimo yale yalifunikwa, *TANESCO* walipeleka nguzo lakini Mradi uliishia hapo, hakuna kilichoendelea.

Mheshimiwa Spika, ukienda Mradi wa Mtii, hawa walijitahidi kwa sababu walitandaza nyaya lakini hawakuweka *transformer,* Mradi uliishia hapo. Mradi wa Parane Pinji, Ivuga, Bwambo, wametandaza nyaya mpaka mwisho kama walivyokuwa wamedhamiria na pia umeme uliwaka kwa majaribio na *transformer* waliweka. Kwanza, mimi nawashukuru sana kwa haya waliyoyafanya. Lakini sasa naisihi Serikali kwamba, kabla ya kufanya kitu kingine chochote, hii Miradi ikamilike. Ninawasihi sana kwa sababu wananchi walikuwa wamepata tamaa ya kupata mwangaza, kupata nishati, wakachimba mashimo wenyewe, wakaweka mpaka waya kwenye nyumba zao, wakitegemea umeme unakuja lakini sasa wamekata tamaa. Mheshimiwa Waziri, wakati unahitimisha, tutaelewana tu endapo utaniambia ni lini kazi za hii Miradi minne zitakamilika.

Mheshimiwa Spika, mimi jimbo langu lina Kata nne kwenye tambarare na Kata kumi milimani. Milimani kuna miti mingi sana; kuna minazi, kuna mazao kama ndizi, kuna migomba, ikifika saa 11.00 kunakuwa na giza, wananchi wanalazimika kulala saa 11.00 siyo haki kabisa. Katika haki za binadamu, hakuna binadamu anayelala saa 11.00.

Kwa hiyo, ningeomba sana Serikali ione umuhimu wa kupeleka umeme milimani, kwa sababu giza linatokana na jinsi nyumba zao zilivyo katikati ya mazao. Saa 11.00 unaingia kitandani, utaamka saa ngapi? Naomba Serikali ione umuhimu wa kupeleka umeme milimani. Nafikiri Waziri amenielewa *(Makofi/Kickeko)*

Mheshimiwa Spika, sasa niongelee jambo kubwa kweli kweli linalohusu nchi na hapo naomba Mheshimiwa Waziri Mkuu unisikilize, nakusihi sana na nina hakika na Mheshimiwa Rais atasikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninakataa sentensi ya kusema Tanzania ni maskini. Mheshimiwa Mbunge, aliyemaliza kuongea sasa hivi, namwunga mkono *ooh!* Tanzania ni maskini, *no* hatuna umaskini. Hakuna nchi ambayo ni tajiri ya rasilimali kama Tanzania. Tanzania ina madini ya aina ya peke yake ya *Tanzanite*, Tanzania ina dhahabu, Tanzania ina almasi, Tanzania ina madini mengi ya aina nyingi sana. Nina uhakika Tanzania nchi yote kuna madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie mfano nchi ya China. Nchi ya China katika miaka ya 60, *income per capital* yake ilikuwa chini kuliko *income per capital* ya Tanzania. Nimesoma kwenye kitabu, katika miaka ya 60 Wachina walianza kuchimba madini yao wenyewe, kwa majembe ya mkono. Sisi tumeshajiwekea *vocabulary* moja, ambayo ni mbaya sana, hatuwezi kuchimba madini wenyewe, Tanzania tulishakubali eti hatuwezi. Mimi nasema tutaweza kama tutataka. Nakubali kwamba, kipindi hiki tuna wawekezaji, lakini hakuna kitu kizuri kama kufanya maamuzi magumu. Binadamu yeyote, anayefanya maamuzi magumu yanayohusu maendeleo, anaendelea. Viongozi wote wanaoongoza nchi, wanaothubutu nafikiri ni Kiswahili kinachoeleweka, basi nchi inaendelea. *(Makofi)*)

Naomba tumkumbuke Baba wa Taifa, mwaka 61 alifanya maamuzi magumu akasema, hapa lazima tupate Uhuru, akawatayarisha wananchi kisaikolojia, tukaimba wimbo mmoja tutaweza kumfukuza mkoloni, tukamfukuza au hatukumfukuza? Tulimfukuza, leo hii tunamkumbuka Baba wa Taifa, kwa sababu alithubutu kusimama imara, akafanya maamuzi magumu, akatutayarisha wananchi kisaikolojia, tukamwunga mkono, nchi ikapata Uhuru. Tunamkumbuka na tutamkumbuka na vitukuu vitamkumbuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, twende kwa Marehemu Abeid Amani Karume, alifanya maamuzi magumu, alithubutu kusema kwamba, tumfukuze Sultani, akawatayarisha wananchi kisaikolojia, Sultani akaondoka, jamani hakuondoka? Aliondoka ni maamuzi magumu. Sasa ni wakati wa Awamu ya Nne, Viongozi wetu, Rais, Waziri Mkuu, tunaomba mfanye maamuzi magumu. Sisemi mara moja, hapana tunaweka mipango ya muda mrefu kwamba, tupeane miaka kumi, baada ya miaka kumi tuchimbe madini wenyewe. *(Makofi)*

Ndugu zangu mimi ni mfanyabiashara, wamachinga ni wafanyabiashara, wawekezaji ni wafanyabiashara, hakuna mfanyabiashara atakayekuambia ukweli hata siku moja. Mimi nakuambieni ukweli, mfanyabiashara nia yake anataka ku-*maximize margin* yake basi. Sasa hawa wenzetu wanaotuchimbia madini ni wafanyabiashara,

wanatoka kwao wanakuja wanakaa Tanzania miaka kumi, wameacha familia zao kule, unafikiri wao ni wajinga? *(Makofi)*

Wanachimba madini, ukweli mimi naomba niamini kwamba, kiasi tunachopata ni kidogo, kiasi kikubwa huyu ni mfanyabiashara jamani. Sifa ya mfanyabiashara anachotaka ni *margin* yake iwe juu, yuko tayari kumdhulumu nani, yule anayemtolea huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa Serikali ianze pole pole, tunachohitaji teknolojia, pamoja vifaa vya kisasa, tuanze pole pole, sisemi tuanze sasa hivi. Hebu tuwe na *long term plans, in ten years time* tutakuwa asilimia 50 ya madini tunachimba wenyewe. Jamani Tanzania tukitaka tutaweza, kwani Mchina yeye ana tofauti gani na sisi?

*Commitment, we lack commitment.* Watanzania hatuna *commitment* kwenye kazi zetu, kisha tumeshajenga *negative attitude,* sisi hatuwezi kuchimba madini wenyewe, kwa nini; hivi una sababu ya msingi? *(Makofi)*

Serikali tunaomba *plan* tuanze kujikomboa kidogo kidogo. Tumepata Uhuru wa Bendera mwaka 1961, lakini wale wale ambao tulisema tumepata Uhuru kutoka kwao, sasa wameshika Uhuru wetu wa Uchumi. Sasa kipi kikubwa wamekamata uchumi, sisi tunajiita maskini mpaka kesho, sisi ni maskini kasema nani? Usiposema mimi ni tajiri, sema mimi ni tajiri na nitaweza. Naiomba Serikali kuanzia leo, *vocabulary* ya hatuwezi, isisikike mahali popote. *(Makofi)*

Serikali tutumie *vocabulary* ya tutaweza, tuanze pole pole. Nawasihi sana, kazi kubwa ya Mbunge ni kuishauri Serikali na mimi nilichofanya hapa ni kushauri. Tunagombania shilingi bilioni 17 hapa na Waziri wa Miundombinu juzi, ni umaskini, hivi shilingi bilioni 17 ni hela nyingi hizo. Lakini tumegombana hapa, tatizo kubwa ni umaskini. Hebu tuanze pole pole kuondoa huu umaskini, kwa kuwa na *plan* ambazo ni za kuanza kujitegemea wenyewe.

Anayechimba madini ndugu zangu ni mfanyabiashara na wafanyabiashara wana akili kweli kweli, pamoja na mimi, kabisa. Unaangalia unavyofanya biashara yako, mtu akija nipunguzie Mama Malecela, hiyo bei ndiyo hiyo hiyo niliyonunulia. Sasa ndiyo hivyo hivyo tunavyofanywa na hawa wenzetu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuanzia leo, tushirikiane pamoja. Viongozi mtakao thubutu na kufanya maamuzi makubwa, mjue kwamba tutawakumbukeni maisha yenu yote, mkiondoka duniani. Mpaka leo tunamkumbuka Baba wa Taifa alithubutu na tunamkumbuka Abeid Amani Karume kwa sababu alithubutu. *(Makofi)*

Naomba nimnukuu mwanafalsafa mmoja wa Kiarabu, alikuwa anaitwa Ibin Batuta, ambaye alisafiri ulimwengu wote, nafikiri mliosoma historia mnamjua, naomba nimnukuu: “Tutakapokuwa tumeondoka hapa duniani, msitutafute kwenye makaburi yaliyopakwa chokaa nyeupe, bali mtutafute kwenye mioyo ya watu tuliowatumikia.” *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mheshimiwa Rais, mtakapofanya maamuzi ambayo yataleta *impact* kwenye nchi, tutawakumbukeni daima. Lakini msipofanya hivyo tutawasahau mara moja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. DR. HARISSON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba nzuri na vile vile naipongeza Serikali, kwa uamuzi mzuri wa kuachana na Kampuni ya *NetGroup* ya Afrika ya Kusini katika kuliongoza Shirika letu la *TANESCO*, utakapofika mwisho wa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, Watanzania tumelelewa na Azimio la Arusha, tumelelewa tukiamini kwa dhati kabisa kwamba, ili tuendelee tunahitaji vitu vinne tu; ardhi, watu, siasa safi na uongozi bora. Hapa katikati hapa sijui ni haka kaupepo ka utandawazi, tumeanza kubadilika na kutetereka na kulikarabati Azimio la Arusha.

Tukaingiza kigezo cha tano, ili tuendelee tunahitaji watu, ardhi, siasa safi, uongozi bora na Mzungu. Ndipo hapo tukaanza kufungulia mlango wazi, *TTCL* ipo inalegalega, dawa ni kumleta mtu kutoka Uholanzi *(MSI)*, aje atusakizie Mzungu bila kuwekeza chochote, tuna *TANESCO* inalegalega, tumekimbilia kumleta Mzungu.

Mheshimiwa Spika, dhana hii mpya ya Mzungu ilianza kweli kulitafuna Taifa letu. Huwezi kuendelea kama Taifa, kama huthamini watu wako, *your own human resource.* Mwalimu aliwekeza sana kwenye elimu ili kila sekta ijitosheleze na wataalam wake wenyewe na hawa vijana wa *TANESCO* tuliwaweka pembeni ili *NetGroup* waje. Walikuwa ni vijana waliosomeshwa na Watanzania wenyewe na walikuwa wamebobea kwenye sekta ya umeme. Walichokosa hawa vijana, ilikuwa ni mtaji wa kutosha kuiendesha *TANESCO*. Lakini kila wakiomba mtaji, tulikuwa tunawaona kama wanatuletea kero na hawa vijana kila walipojitahidi kukusanya ankara za umeme, kuna wakati Wizara nyeti zilikuwa zinawatisha hawa vijana kuwafukuza kazi. Tumewaita hawa Wazungu, *NetGroup* ambao nathubutu kusema, hata sifa zao kitaaluma zilikuwa duni kupita hawa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina ushahidi wa kitengo kikiongozwa na fundi mchundo, wakati kijana wetu ana digrii ya Chuo Kikuu ya *Electrical Engineering.* Ushahidi upo tele. Lakini *qualification* kubwa ni ngozi.

Mheshimiwa Spika, tumeelezwa mara nyingi na Serikali kwamba, *NetGroup* wamesaidia sana hata kukusanya ankara ambazo zilikuwa hazikusanywi huko nyuma. Mimi sikubaliani na hilo, waliokuwa wanakusanya ni sisi. Hivi mliwaona Wazungu wakikusanya hizo ankara? Tulikuwa tunakusanya sisi wenyewe. Halafu tuliwafagilia njia wamekuja tu, Serikali yenyewe ikamwambia kila mtu, lipa kodi bwana, hawa watu hawana sijui Ofisi nyeti wala wapi. Kweli ofisi zetu tunazoziheshimu zilishakatiwa

umeme na Wazungu hawa. Tuliwapa sisi wenyewe *blank cheque,* halafu leo tunawasifia. Hatujawahi kuwapa *blank cheque* vijana wetu huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kitu kimoja, natoa rai kwa Serikali kwamba, utakapofika mwisho wa mwaka, vijana wetu wa Kitanzania waki-*take over* wakichukua uongozi wa *TANESCO,* hebu tuwape heshima kama Wazungu, tuwasikilize na tuwaamini. Lakini si hivyo tu, hao vijana waliona wenzao walikuwa wanapata kiasi gani cha pesa, tuwaongezee mshahara kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipato kizuri si halali kwa Mzungu tu, hata kwa Mswahili pale unapotaka tija. Taarifa ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara, imegusia suala ambalo limewagusa Watanzania wengi, bei ya petroli na dizeli imebaki juu licha ya uamuzi mzuri wa Serikali wa kuondoa kodi ya ongezeko la thamani. Sababu ni zipi? Kamati imebaini kuwa nguvu za soko zimeingiliwa na waagizaji wakubwa wa mafuta. Wanapanga bei. Sasa tutatoka tokaje huko? Mimi nauona utatuzi mmoja tu kwamba, tuliruhusu Shirika letu la Taifa la Mafuta *(TPDC),* liingize nchini, nusu ya mahitaji ya mafuta ya petroli na dizeli kama ambavyo nchi nyingine zinafanya.

Mheshimiwa Spika, tukifanya hilo, hizi bei za ubabaishaji zitakuwa zimekufa. Nenda Uchina, tena nisiende mbali. Juzi kuna mwenzetu mmoja alikuwa *Mozambique* anasema, *Mozambique* Shirika la Taifa *a hundred percent* linaingiza mafuta. Kenya hawajawaachia wafanya biashara peke yao na Uganda. Nchi nyingine zote, ni sisi tu, uchumi huria umekuwa ni uchumi holela. Ndiyo maana makampuni ya mafuta yanafunguliwa kila siku na vituo vya mafuta vinajengwa kila siku, kwa sababu wenzetu wamegundua sehemu pekee ya kutajirikia kwa haraka ni Tanzania.

Mheshimiwa Spika, tunaiomba Serikali, iiruhusu *TPDC* ianze kuingiza mafuta hapa, angalau nusu au hata theluthi moja ili kuleta ushindani kwenye soko. Kama Serikali itashindwa kweli kufanya hivyo, basi mimi nisizuiwe kuwa na wasiwasi kwamba, pengine baadhi ya viongozi wetu, wana maslahi kwenye hayo makampuni ya mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaihitaji *TPDC*, kwa sababu kubwa tatu. Kwanza, kuleta ushindani wa kweli kwa bei za mafuta. Lakini pili, kutuanzishia kitu ambacho Kamati yetu imesema, Hifadhi ya Taifa ya Mafuta *(National Strategic Oil Reserve)*. *(Makofi)*

Huwezi ukamtegemea *Oil Com* akuwekee hifadhi ya mafuta. Utakuwa unaota! Lakini tatu, mimi naamini mafuta ni usalama wa Taifa. Tumepigana vita na Uganda, wengine walikuwa wadogo sana pengine hapa. Makampuni ya mafuta, yalikataa kutupelekea mafuta kwenye *battle flont*, ikabidi *TPDC* iombwe kufanya hiyo kazi. Ilifanya kazi vizuri, tusiisahau leo. Tuipe hilo jukumu, ni usalama wa Taifa huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesikitishwa sana na kufedheheshwa sana na malumbano ya muda mrefu, kuhusu dalili za mafuta Unguja na Pemba na huku tukijiita kuwa ni Muungano wa kutolewa mfano Afrika. Naomba nitahadharishe kuwa, wakati

tunalumbana kuhusu Uzanzibari na Umuungano wa hayo mafuta, wenzetu Uganda wameshapata mafuta na wameingia kuchimba visima vingine. Wakati sisi tunalumbana, wenzetu Kenya wanahangaika kweli kweli, kutafuta mafuta. Wanachimba kila siku, sisi tunalumbana. Watanzania ni wataalam kweli kulumbana kwa maneno lakini siyo vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunalumbana, nchi zilizoendelea zinawekeza kweli kweli kutafuta vyanzo mbadala vya nishati. Mheshimiwa Waziri ameelezea *bio diezel,* mafuta kutokana na mimea. Mimi naamini tutakapokuwa tumemaliza hayo malumbano kuhusu mgao wa fedha utakuwaje na baadaye mnajua kwani sisi ni mafundi wa kulumbana, tutaanza pia malumbano ya mgao wa nafasi ya madaraka kwenye hayo mashirika ya mafuta. Wangapi watatoka Pemba, wangapi watatoka *Mbamba Bay.* Tutakapokuwa tumemaliza kufikia muafaka kuhusu mafuta, mafuta ya kutoka ardhini yatakuwa hayana thamani tena duniani hapa.

Mheshimiwa Spika, asubuhi ulitutangazia kuhusu uwepo wa Maonesho ya *TPDC.* Ni elimu kubwa kwenda kuwasikiliza mabingwa hao. Nimewasikiliza mimi leo mchana, wameniambia kilichogundulika Zanzibar mwaka 1957 na Pemba mwaka 1962 ni kile wanaita *oil seepage,* yaani uvujo tu wa mafuta. Uvujo wa mafuta ni dalili tu ya mafuta kuwepo, siyo mafuta kuwepo. Hiyo dalili lazima uifanyie kazi. Kuna kazi kubwa kweli ili upate mafuta. Watanzania tunapigania dalili, halafu si hivyo tu, ukiona dalili inabidi uchimbe visima vingi. Kila kisima wananiambia ni kati ya shilingi bilioni 21 hadi bilioni 35. Leo Watanzania tunacheza, badala ya kuanza kukopa fedha kuchimba visima. Tunalumbana kuhusu mgao na kuhusu Meneja Mkuu atatokea Pemba, atatokea *Mbamba Bay.*

Mheshimiwa Spika, kweli hatuwezi kujenga Taifa namna hiyo. Hii *ashakum* si matusi, ni sawa na kesi ya mimba changa, ukaiangalia ukasema pale ni Gavana wa Benki. ni Mbunge wa Kyela.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Uwekezaji ya Biashara na Wabunge wenzangu, wameongelea kwa kirefu suala la Mchuchuma na Liganga na kengele imenigogea hapa. Kanuni ya 50(2), inanizuia kurudia yale yaliyokwishasemwa hivyo, naungana na Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuwa, wakati umefika kuunda Kamati Teule ya Bunge, kuipitia Mikataba yote ya Nishati na Madini. Vile vile hii Mikataba mipya ya Mchuchuma na Liganga ili Bunge letu litekeleze wajibu wake wa Kikatiba wa kuisimamia Serikali chini ya Ibara ya 63 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwamba ipo hali ya viongozi kuisahau sahau Kyela wakifirikia pengine kwamba tupo Malawi, pengine ni kutokana na ule mto Songwe. Mto Songwe mvua zikinyesha sana. Ile sehemu iliyokuwa Tanzania inaenda Malawi na walionipigia kura sasa hivi kwa kweli wananiona sasa hivi Malawi. Jamani mimi bado ni Mbunge wenu na tutawasiliana mvua zikipungua. Kwa hiyo, kuna hali ya kutusahau. Nasema hivyo baada ya kusoma hii taarifa ya jumla kuhusu Sekta ya Nishati ukurasa wa 14, 15, 16 na 17. Nimeshangaa na kuona wivu hapo hapo. Kuna

Wilayaambazo vijiji vyao kumi kwa mkupuo kwa mwaka mmoja, vina umeme, mimi Kyela kule sijapata umeme hata kijiji kimoja. Kwa kukosa umeme Kyela, kwenye vijiji vyetu, tumeshindwa kabisa kutumia fursa pekee tuliyonayo ya kutawala kabisa biashara kwenye nchi jirani ya Malawi.

Mheshimiwa Spika, kutawala biashara kwa kutumia kijinga cha moto, usiku ukiuza mchele mzuri wa Kyela, huwezi. Kwa hiyo, tunaomba Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, unikumbuke ndugu yako na Wataalam wako kwamba, sisi wana-Kyela tulioko Ngana, Katumba Songwe, Ngonga, Ikolo, Bujonde, Kajunjumele, Mwaya, Makwale, Matema, Muungano na Ipande, tunahitaji umeme ili kwa kweli tuweze kuitumia nafasi tuliyonayo, kubadilisha mazingira yetu na kutawala biashara ya mpakani.

Mheshimiwa Spika, sio vizuri kunigongea kengele. Naomba nimalizie hapo na kusema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. EUSTACE O. KATAGIRA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii, niweze na mimi kuchangia katika hoja hii ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini. Awali ya yote, naomba nimpongeze Waziri wa Wizara hiyo, pamoja na Naibu Waziri wake, lakini na Watendaji wote wa Wizara hiyo, kwa kuandaa bajeti nzuri. Zaidi ya hapo, napenda niwapongeze kwa kuendesha Wizara jinsi anavyoiendesha.

Mheshimiwa Spika, naomba niwasihi wanaoendesha Wizara ya Nishati na Madini, ni Wizara tofauti na Wizara nyingine. Ni Wizara muhimu na ni Wizara nyeti. Wizara hii si sawa na Wizara ya Kazi, si sawa na Wizara ya Elimu. Uendeshaji wa Wizara hii, unaweza ukabadilisha Taifa letu likawa Taifa tajiri kabisa. Tukaondokana na umaskini au inaweza ikaendeshwa vibaya, tukabaki pale ambapo tupo. Tunalilia umaskini, wakati tungeweza kutajirika na kuendesha nchi yetu, tofauti na nchi ambazo ni maskini. Kwa hiyo, nawaasa waweke bidii, kuwa na *strategies* nzuri ili tuweze kubadilisha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, naleta shukrani za wananchi wa Wilaya ya Karagwe, hususan Jimbo la Kyerwa, wana taarifa kwamba, watapelekewa umeme vijijini. Wana taarifa katika jimbo la Kyerwa kwamba, umeme sasa utasambazwa kwenda sehemu za Rwabwere, Nkwenda, Rukuraijo Kagenyi na *Kyerwa Mines* na viunga vyake, Vijiji vya Nyaruzumbura, Isingiro, Kaisho mpaka Murongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niieleze Wizara kwamba, wananchi baada ya kupata taarifa hizi, sasa wanajiandaa kikamilifu, kutumia fursa hii ya umeme ukishawafikia. Wapo ambao wameshaanza mipango ya kununua mashine za kuweza kuranda, wako ambao tunajiandaa kununua mashine ndogo ndogo za kukoboa kahawa ili badala ya ilivyo sasa, ambapo mashine nne katika Wilaya ya Karagwe za kukoboa kahawa zipo katika Mji wa Wilaya, hiyo Kayanga na viunga vyake, inabidi sasa hivi vijana wafuate ajira katika viwanda hivi katika Mji wa Wilaya hiyo. Akina mama ambao wanachambua kahawa ili ziwe na *quality* nzuri, inabidi waondoke majumbani kwao vijijini waende kufuata ajira hiyo pale Wilayani. Sasa wanajiandaa ili viwanda hivi vidogo vidogo, vijengwe katika Kata ambako kahawa inazalishwa ili ajira hizi zipatikane katika sehemu hizo ambako

kahawa inalimwa, iwe inavunwa na kukaushwa ili yale maganda ya kahawa yaweze kutumika kama mbolea katika vijiji hivyo na katika Kata hizo.

Mheshimiwa Spika, tunazo shule za Sekondari katika maeneo hayo, shule hizo wameshanipigia simu na kuniuliza niwahakikishie kama umeme utakwenda kama ulivyopangwa. Kwa sababu sasa hivi wana mipango ya kununua jenereta, lakini kama wakihakikishiwa kama kweli huu Mradi upo na utatekelezwa kwa wakati, wananiuliza, je, pesa hizi za kununua jenereta wajenge bweni la wasichana? Kweli tukihakikishiwa kwamba, huu Mradi utatekelezwa jinsi ulivyopangwa, basi hizi fedha badala ya kununua jenereta, wanaweza wakaendeleza kujenga mabweni, madarasa au maabara.

Mheshimiwa Spika, nina hakika na mategemeo makubwa kwamba, hata kweli haya ambayo yameelezwa na Mheshimiwa Anne K. Malecela, yaliyotokea katika Jimbo lake la uchaguzi, nina matumaini kwamba, hii Miradi itatekelezwa kama jinsi ambavyo wananchi tumeambiwa.

Mheshimiwa Spika, Karagwe ni Wilaya kubwa sana na ndiyo maana tunao mkakati na tumeanza kuomba kwamba, Wilaya hii igawanywe katika Wilaya mbili; Wilaya ya Karagwe na Wilaya ya Kyerwa. Jimbo la Kyerwa ni kubwa sana. Nashukuru tumo katika Mradi huu wa kusambaza umeme vijijini. Lakini Mradi huu ulivyoelezwa, hautasambaza umeme katika Kata zote za Jimbo la Kyerwa, bado kuna Kata ambazo hazikuingizwa kwenye Mradi. Kata hizo ni Kata ya Kamuli, Kata ya Kimuli, Kata ya Mabira na Kata ya Bugomora.

Mheshimiwa Spika, naomba Wizara ijitahidi ili sasa ipangilie pia kuvipatia umeme Vijiji vilivyoko katika Kata hizo nne nilizozieleza. Hizi ni Kata kubwa, ni Kata ambazo pia zinazalisha kahawa kwa wingi. Ni Kata ambazo zina shule za sekondari na pia na wao wanahitaji waweze kujenga viwanda vya kukoboa kahawa. Kahawa hiyo ikobolewe pale pale katika Kata zao, mbolea inayotokana na maganda ya kahawa itumike katika kuendeleza kilimo chao na pia shule zao za sekondari ziweze kupata umeme. Nafahamu sasa hivi kama hakuna umeme, inakuwa ni matatizo makubwa. Vijana hawawezi kusoma na wakawa washindani, kama ikibidi ikitimia saa moja jioni wasiendelee na masomo au wawashe karabai, lakini pia maabara nzuri inahitaji vifaa vya umeme. Hata wanafunzi wenyewe katika shughuli zote za kujiendeleza, watahitaji kutumia vifaa vya umeme.

Mheshimkiwa Spika, kwa hiyo, naomba Wizara iweze kuweka Kata hizi nne nilizozitaja Kamuli, Kimuli, Mabira na Bugomora katika mpango wake wa kusambaza umeme vijijini. Lakini kubwa zaidi ni kwamba, Kata mojawapo ya Bugomora inapakana na nchi jirani ya Uganda na nchi ya Uganda ninavyoelewa, wana mpango wa haraka wa kuleta umeme pale mpakani, ambapo tunapakana nao katika Kata ya Bugomora. Itakuwa ni jambo la kusikitisha, kama wenzao watakuwa wanaonekana wana umeme wanawasha, wanashughulika, wanajiendeleza, lakini ng'ambo tu ya mpaka, itakuwa ni kwamba kila mara ni kiza. Itakuwa ni kwamba, viwanda vyao mpaka wanunue jenereta ili kuweza kuviendesha, itabidi tujitahidi. Ombi la wananchi hao na wao tuwatafutie Mradi wa kusambaza umeme katika vijiji katika Kata hizo nne.

Mheshimiwa Spika, suala la bei ya umeme limeongelewa sana kila mara kwamba, bei ya umeme ni kubwa. Lakini mimi naona bei ya umeme inapanda kwa *factors* nyingi. Lakini *factor* mojawapo ni ile ambayo Serikali ilianza mtindo wa kutokuzalisha umeme, ikaanza kuwa nayo inakuwa mkaa kati badala ya kuzalisha umeme, inatafuta watu wanazalisha umeme, yenyewe inanunua kupitia Shirika lake la *TANESCO,* halafu sasa inaanza kuuza umeme huo. Kila mara kama kuna msululu mwingi katika kuuza kitu chochote, lazima bei itapanda. Nafarijika kwamba, sasa katika mambo yanayotendeka, inaelekea Serikali imelitambua jambo hili na katika shughuli za sasa hivi, inanunua vifaa yenyewe. Inataka pia izalishe umeme yenyewe, nina hakika hili litakuwa la msaada katika kuweza kupunguza bei ya umeme. Bei ya umeme isipopungua, gharama za maisha zinapanda na gharama za familia zinapanda. Mtu ndani ya nyumba unagombana na watoto, kwa nini mnawasha taa; kwa nini mnawasha kompyuta.

Mheshimiwa Spika, lakini zaidi ya hayo bei ya umeme ikipanda, gharama za uzalishaji zinapanda na vitu vinapanda bei, *inflation* inalipuka, bei ya sarafu inateremka, mambo yote yanategemea umeme na mafuta.

Mheshimiwa Spika, nawaasa Wizara na Serikali kwa ujumla, tuache mtindo wa kutaka kuwa wakaa kati, wa kusubiri fulani azalishe umeme sisi tuununue, halafu tuchuuze kwa wananchi. Tuzalishe umeme wetu wenyewe, tuuze kwa wananchi na kwa bei ambayo italeta maendeleo na bei ambayo itakuwa ni bei muafaka.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru tena kwa kuniruhusu nichangie. Nasema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Wizara ya Nishati na Madini. Kwanza kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, kwa hoja yake aliyoiwasilisha Bungeni na vile vile nirudie kumpongeza kwa kuwa Waziri wa Wizara hii, kwa sababu alikuwa Naibu Waziri na amepanda cheo kutokana na kazi yake nzuri alipokuwa akisaidia katika Wizara hii. *(Makofi)*

Tunaamini tutakaposema, atatuelewa kwa sababu anaelewa mambo mengi yaliyo katika Wizara hii. Vile vile labda nianze kuelezea kabla sijasema ya Taifa, niseme yale yanayohusu Jimbo langu na majimbo ya wenzangu Mkoa wa Rukwa. Sisi umeme tunaotumia Sumbawanga unatoka Zambia, unatoka kwenye gridi ya Zambia. Lakini mpaka sasa tunapata usumbufu mkubwa sana, kwa sababu kila siku ule umeme unazimwa. Mwanzo tuliambiwa kwamba, bado mitambo inarekebishwa, itakapotulia umeme hautasumbua, lakini mpaka sasa ni usumbufu mkubwa sana. Vile vile nimefurahi kusikia Wabunge wenzangu, wakizungumzia umeme kuhusiana na Kata na Vijiji. Sisi Mkoa wa Rukwa, umeme upo Sumbawanga na Mpanda tu, Makao Makuu ya Mkoa na Makao Makuu ya Wilaya ya Mpanda, lakini Namanyere ambayo ni Wilaya haina umeme.

Mheshimiwa Spika, halafu vile vile tunayo Tarafa ya Matai, umeme unaotoka Zambia unapita vijiji vya Jimbo la mwenzangu Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila,

mpaka Matai, umeme unawapita watu wanaushangaa, wanasema hivi vyuma vya nini? Wanaambiwa umeme, unakwenda kuwaka Sumbawanga, lakini unawapita wananchi. Sasa teknolojia hiyo ni ya zamani, inawezekanaje umeme ukapita wananchi kwenda sehemu nyingine? Jambo hili tunapata fedheha. Vile vile maeneo kama Kasanga kwa mfano, Serikali imekubali tutakuwa na bandari, sasa bandari itaanza wakati hakuna umeme. Mizigo itapakuliwa mchana tu? *(Makofi)*

Kwa hiyo, naomba nalo hilo litazamwe. Vile vile kutoka Sumbawanga kwenda Mpwina na Laela, ni miji mikubwa sana hii, lakini kwao ukizungumza umeme ni kama ndoto. Kwa hiyo, nataka niseme, tunakokwenda tunatakiwa kila wakati *infrastructure* itangulie kukaribisha maendeleo na umeme ni kichocheo cha kuleta maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba niseme mambo ya Kitaifa. Haya mimi nitayasema kwa misingi miwili. Kwanza, sikusudii kunung'unika na yaliyopita, kwa sababu binadamu kazi yake ni kusonga mbele. Ingawa ni kweli katika vita, wanasema ukiona unazidiwa unarudi kidogo hatua mbili nyuma ili uende zaidi. Kwa hiyo, mimi nataka niseme tulipofika hivi sasa tulipo na tunakokwenda na nitalisema hili kwa imani, wote Wabunge tumesema kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne imeanza vizuri. Mimi nimemsikiliza Rais wetu, anasema yeye atafurahi sana kwamba, baada ya miaka yake mitano, wananchi waseme na yeye afurahi kusema kwamba, niliwakuta Watanzania hapa nimewafikisha hapa. Hiyo, ndiyo azma yake na mimi namtakia kila la kheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini ishara zinazoonekana wazi ni dhamira yake na wanaomsaidia. Kwa mfano, mambo mengi anayosema Waziri Mkuu na wanayafanya, nina hakika ni kero za muda mrefu, ambazo amekuwa akiziona na kuzijua tangu akiwa Mbunge na tangu akiwa Serikalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mambo mimi nitakayoyasema, naomba niyaseme kwa misingi kwamba, Serikali tuelekee huko na isionekane kwamba mimi nakosoa, hapana. Mambo haya sisi tumesema na katika Katiba tumesema, Sura ya kwanza inasema, Tanzania itakuwa ni nchi ya Ujamaa na Kujitegemea. Hiyo tumesema ndani ya Katiba. Sasa ninachotaka, Serikali yetu ianze kujiuliza, je, hivi isemavyo Katiba ndivyo tunavyokwenda? Maana katika rasilimali tuliyonayo na katika uwekezaji tulionao, tunaweza tukaja kugundua kwamba, nchi hii imebakia mikononi mwa matajiri wachache, tena mbaya zaidi wanaotoka nje. Kwa hiyo, naomba niseme Wabunge wengi wamesema kuhusu mambo ya mikataba, mimi nataka nipendekeze na nasema kwako kwamba tuweke ndani ya Kanuni kwamba, mikataba yote yenye maslahi na nchi, inayohusu uchumi, iletwe katika Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hii ni kuondoa kuweka Tume za kuchunguzana, maana mambo haya yatakuwa yamekwisha kuja Bungeni, hakuna wa kumlaumu. Sisi kazi yetu itakuwa ni kusimamia na nitasoma ili kuweka uzito wa maneno haya, naomba ninukuu kwa ruksa yako, Katiba yenyewe ya nchi inasema nini.

Mheshimiwa Spika, Katiba ya nchi ile sehemu ya kwanza, ibara ya 4(1) inasema hivi, nanukuu: "Shughuli zote za mamlaka ya nchi katika Jamhuri ya Muungano, zitatekelezwa na kudhibitiwa na vyombo viwili vyenye mamlaka ya utendaji, vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki na pia vyombo viwili vyenye mamlaka ya kutunga sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma."

Sasa mikataba ya migodi ni shughuli za umma. Hatuwezi tukaacha watu wachache wakafanya, halafu baadaye tukaanza kulaumiana. Kama ni kufa tufe wote, kwa maana ya kujua, maana haiwezekani watu wanafanya mkataba kwa *Air Port* ya Kilimanjaro wakiambiwa wanasema ni siri. Mkataba wa nchi utakuwaje ni siri!

Kwa hiyo, nasema la pili, ibara hiyo hiyo ya (4) kifungu cha (2) kinasema hivi: "Vyombo vyenye mamlaka ya utendaji, vitakuwa ni Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, vyombo vyenye mamlaka ya kutekeleza utoaji haki, vitakuwa ni Mahakama ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Mahakama ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na vyombo vyenye mamlaka ya kutunga Sheria na kusimamia utekelezaji wa shughuli za umma, itakuwa ni Bunge na Baraza la Wawakilishi." *(Makofi)*

Kwa hiyo, Wabunge tukitaka mikataba iletwe hapa, ndio kazi inayosemwa katika Katiba, mimi naomba tusilie wakati tuna haki, Katiba yenyewe inatupa haki, hilo la msingi la kwanza.

Pili, tunayo Sera ya Taifa, kwangu mimi nasema nataka tuseme yetu tunakotaka kwenda, sitaki kusema huku tulikotoka, naanzia hapa tulipo. Hii Sera ndio tuliyoinadi kwa wananchi, sasa uwezeshaji. Katika Ilani ya Uchaguzi ukiacha huduma za jamii, kitu ambacho tumesema kipewe kipaumbele nambari mbili, ni uwezeshaji wa wananchi wa Tanzania. Sasa ishara za uwezeshaji zimeanza kuonekana, kwa mfano, shilingi bilioni hamsini zilizowekwa, ambazo zitatolewa kwa mikoa shilingi milioni 50,000, napendekeza ziwe ni *seed money* kwa benki. Mabenki yaitwe nayo yachangie, *NMB* wana hela, *CRDB* wanazo hela, waitwe hawa watoe nao mchango katika fungu hili la Serikali. Kwa sababu hatuwezi kusema miaka yote, Serikali ndio itaweka fedha, shilingi bilioni kumi iwe *seed money,* kuwaambia Mabenki na nyie changieni tufike hata shilingi bilioni 60, ili kila mkoa uongezewe. Napendekeza fedha hizi isitolewe misaada, Watanzania waanze kuzoea kukopa na kulipa, hapa kupeleka misaada, Serikali itakuwa imewadhamini.

Sasa uwezeshaji inasemaje, nitasoma kwa ruhusa yako, nataka mimi niseme ya msingi tu ili tuelewane. Nasema hivyo kwa sababu hata wanaotekeleza hizi sera, wameweka kwenye makabati, wakija humu Wabunge wakiwabana ni kana kwamba hawajui, lakini mbona tunazo. Nitatoa mifano miwili ili kudhihirisha hayo, Wabunge walipokuwa wakizungumza maliasili na hasa uwindaji wa kitalii. Mimi nikashangaa Waziri hakusimama akaeleza hapa kwa sababu Waziri wa Maliasili na Utalii alichagua Kamati ya kusaidia Serikali kupendekeza namna ya kuendesha uwindaji wa kitalii. Alitoa hadidu za rejea nzuri sana, mimi na Mheshimiwa Job Y. Ndugai, tulikuwa Wajumbe wa Kamati aliyoiteuwa Waziri, tumeisaidia sana Serikali kuleta mapendekezo na tulimpa ayapate kabla ya Bunge.

Sasa angewaeleza yale tuliyoyapendekeza wala asingebanwa na mimi sikushangaa kwa sababu vilevile Serikali hii pia iliyotangulia, Waziri Mkuu, aliweka Tume ya kumsaidia namna ya kupendekeza Sera ya Sekta ya Madini. Hiyo nayo ipo nzuri kweli, haya yote tunayopiga kelele yamo kwenye kile kitabu cha mapendekezo ya Kamati ya Dr. Kipokola.

Sasa nayo ipo huku tunagombana kazi ilishafanyika. *Tanzanite*, Mheshimiwa Waziri Mkuu, wewe ni shahidi, Waziri Edgar D. Maokola-Majogo, aliweka Kamati ya Jenerali Mboma, wakaenda kuchunguza mambo ya *Tanzanite*, mapendekezo mazuri yako ndani ya kabati. Sasa ndio mimi nasema nataka na leo tuanzie hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema katika uwezeshaji, kwa mfano, sera imetafsiri, inawalenga ni wananchi, inasema walengwa wa sera ni wananchi na wananchi hao wamefafanuliwa kwamba ni makampuni ya Watanzania, ambayo yameundwa Tanzania na yana hisa zaidi ya asilimia 51. Ndio tafsiri ya makampuni ya uwezeshaji, sasa hawa wanaokuja kuwekezesha wageni wote wanaachiwa mia kwa mia, Serikali haimo na Watanzania hawamo. Kwa hiyo, hapo ndio mimi naomba tuanze kurekebisha.

Mheshimiwa Spika, sasa ili twende vizuri, samahani ukurasa unaofuata imezungumzia vilevile inatoa tahadhari kwamba, ukichunguza hali ilivyo sasa, hali halisi ni kwamba, matajiri ni wachache hivi sasa. Uwezeshaji unataka kututoa kwa matajiri wachache tuwe na matajiri wengi, wananchi wawezeshwe walio wengi kwa hisa zao na kadha wa kadha. Hivi sasa kwa utafiti nilioufanya, baada ya miaka kumi kama hatukuangalia, Tanzania itakuwa na matajiri kumi na utajiri wao utakuwa unatokana na bajeti ya Serikali, maana duniani kote hakuna mtu tajiri, tajiri ni Serikali, ndio wanaopewa *tender*, ndio kila kitu. Waziri Mkuu, nataka nikupongeze na Waziri wa Fedha, hapa ingetokea *scandal* juzi hapa kwa sababu kuna watu walikuja kufanya kampeni kwa Wabunge, ambao wanatumiwa kutetea matajiri humu Bungeni, lakini Waziri wa Fedha na Waziri Mkuu wakaweka jiwe, wakasema kufa na kupona, walitaka tufute kodi ya mafuta, turudishe kodi ya mafuta tuiondoe irudi kuwanufaisha wanyonyaji watatu tu wa mafuta. Waziri Mkuu alisimama imara na Waziri wa Fedha, hongereni sana Mungu awabariki. *(Makofi)*

Hatuwezi kuuza nchi, kwa hiyo, ninachosema kwa kumalizia mapendekezo yangu, la kwanza napendekeza kwamba, ile sheria ya kutekeleza sera ya nchi ya uwezeshaji? Vilevile napendekeza kwa Serikali, mambo muhimu yatakayotekelezwa, yaani kila Wizara ilete mambo muhimu yatakayotekelezwa kwa kuzingatia Sera na Ilani ya Uchaguzi. Kwa sababu *speed* ya Rais, lazima ifanane na Mawaziri wake na Wabunge. *(Makofi)*

Pili, nataka tutazame sura yetu kama Katiba yetu inavyotuelekeza, kwenye ujamaa inalingana na matamshi yetu. Wachina kwa mfano, wamebakia na Sera ya Ukomonisti, lakini ukifika sio Ukomonisti wa wakati ule. Ni Ukomonisti unaodhibiti nidhamu ya nchi na mambo kwenda sawa na sisi jamani tubaki na ujamaa lakini wenye manufaa kwa watu

wote, sio kwa watu wachache, watu wote wale sio watu wachache kula wengine wanalala njaa, hauwezi kuwa ujamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu vilevile napendekeza kwamba, sheria ya madini itazamwe upya, ina kasoro nyingi sana na katika sheria hiyo jambo litakalozingatiwa ni kwamba, maeneo yote yenye rasilimali ya madini yawe ni mali ya Taifa, watu waombe kwa Serikali. Sio kila mtu kuachiwa anakwenda anakotaka, maeneo yote yaliyotambuliwa yana madini kutokana na ramani ya nchi, yawe ni mali ya Serikali. Anayekuja anaambiwa nenda pale na Watanzania hawa, ubiya. Lakini sio kuachia tu watu wajiingilie wenyewe, hakuna mtu anayekubali mambo hayo. Kwa mfano, wa-*South Africa* watakuwa wakoloni baadaye wa nchi zote za hapa, mimi nilisafiri juzi kwa ndege, tulitoka na ndege kwenda Botswana, tulipita *South Africa,* tulipotaka kwenda Zimbabwe, tulirudi tena *South Africa. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii, niweze kuchangia kidogo katika Wizara hii muhimu. Lakini kabla sijaanza kuchangia, naomba nirekebishe jina langu ni Abubakar Khamis Bakary.

**SPIKA:** Wala sikujua kama ni wewe, kumbe walikuwa na maana ya Abubakar, wakaandika Bakary hapa, samahani sana.

**MHE. ABUBAKAR KHAMIS BAKARY:** Mheshimiwa Spika, madini ninavyofahamu mimi na nishati, ni vitu muhimu ambavyo naweza kusema kwamba ni *backbone* ya uchumi wa nchi. Lakini bahati nzuri, Mwenyezi Mungu ametujalia, Tanzania ina madini mengi sana na hii ni zawadi kwa Mwenyezi Mungu. Lakini bado nahisi kwamba, sisi Watanzania hatujawa *serious* katika suala hili na kulegea kwetu, ndiko kunako tufanya tuwe maskini kabisa kabisa.

Kwa sababu mimi siamini kwamba, haya makampuni ya nje, ambayo yanakuja kuchimba madini kwamba, kweli yana nia njema na Tanzania na kwa maana hiyo, naishauri Serikali kwamba, hebu tutazame upya mikataba, tutazame sheria hii ya madini, vyote vina matatizo. Waheshimiwa Wabunge wote hapa, wanapozungumza wanazungumzia suala la mikataba, suala la sheria, sasa mimi nafikiri tungelitazama, kwa sababu katika mikataba ziko *clauses* mbalimbali, yaani *performance clauses* zile ambazo tunaweza tukazizungumza na tukajua hasa ni kitu gani ambacho kinatuletea matatizo haya. Kwa hiyo, huo ni ushauri wangu wa mwanzo.

Lakini la pili, ambalo napenda kulizungumzia ni suala la umeme, ambao unatoka Rasi Kilomoni kwenda Rasi Fumba Zanzibar, pale kuna *sub-marine cable,* ambayo nafikiri iliwekwa kuanzia mwaka 1978 au 1979. Sasa ninavyofahamu ni kwamba, *life span* ya *sub-marine cable* kama ile ni miaka 20, sasa leo imeshazidi miaka 20, kwa hiyo, *cable* ile ipo katika matatizo, Je, Wizara au Serikali kwa ujumla, inalishughulikia vipi suala hili?

Lingine ni kwamba, katika *sub-marine cable* hii, ninavyokumbuka ni kwamba, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitoa fedha kulaza *sub-marine cable* hii na Serikali ya

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikapeleka umeme kutoka Rasi Kilomoni kwenda Zanzibar. Kwa hiyo, ninavyofahamu mimi ni kama mfano wa *joint venture* kwamba, mmoja ametoa kimoja na wapili ametoa cha pili. Sasa katika mapato yanayopatikana kwa kuuza umeme Zanzibar, yanafanywa vipi, yanagawiwa vipi na haya madeni ambayo yapo, yanashugulikiwa namna gani? Hilo ni suala la pili ambalo ningelipenda nipate majibu.

La tatu, ningelipenda nizungumzie kauli ya Serikali, ambayo ilitolewa juzi na Mheshimiwa Waziri wa Madini, nasema ni kauli ya Serikali, kwa sababu Waziri anapozungumza katika Bunge lako hili Tukufu, basi hiyo huwa ni kauli ya Serikali. Sasa juzi Mheshimiwa Waziri, nakumbuka aliulizwa kwamba, hii gesi ambayo inatoka Songosongo na ambayo imekuwa katika soko na taarifa tulizonazo ni kwamba, ni kiasi cha shilingi za Kitanzania bilioni 60, ambazo zimeshapatikana. Je, Zanzibar inafaidika vipi? Sasa kauli ya Serikali iliyozungumzwa hapa na Mheshimiwa Waziri alisema kwamba, kwa sababu Ubungo pana gridi pale ya Taifa, ambayo itakwenda Zanzibar na kwa sababu Tanga kuna azma ya kuwa ya gridi ambayo itapeleka umeme Pemba kwa kutumia gesi, kwa hiyo, ni faida kubwa ambayo Zanzibar itafaidika nayo.

Mheshimiwa Spika, sasa nahisi kwamba, kauli hii ya Serikali ikiwa kweli ndio kauli ya Serikali basi itakuwa wamekosea, kwa sababu moja kubwa kwamba, kwa mujibu wa Katiba, katika ibara ya 4(3) katika nyongeza ya kwanza ni kwamba, gesi ni masuala ya Muungano. Sasa unaposema au inapotoka kauli kusema kwamba, kwa sababu tu kuna gridi ambazo zitaunganisha umeme huu wa kutumia gesi kwenda Zanzibar. Kwa hiyo, hiyo ndio itakuwa imeshamalizika faida ya Zanzibar, nahisi hilo ni koseo na naomba Serikali ilirekebishe. Kwa sababu moja kubwa, ni sawa sawa na kusema kwamba, mimi na mwenzangu tuna ng'ombe ambao tunachunga pamoja, sasa ng'ombe wale kama wakizaa halafu maziwa ambayo yanatokana na ng'ombe wale ambao ni wetu pamoja, ikawa mimi nanunua maziwa yale ukasema kwamba, sina *share* nyingine tena kwa sababu tu nanunua maziwa. Mimi nahisi hilo litakuwa ni kosa.

Sasa mimi ninachosema ni kwamba, kwa sababu gesi hii ni ya Muungano, hata kama Serikali inapeleka gridi Zanzibar na Pemba, basi lazima kuna *share* ya Muungano, ambayo lazima ijulikane. Sasa *share* hiyo ya Muungano ya Zanzibar, katika gesi hii ambayo imepatikana na katika fedha hizi ambazo zimepatikana, iko vipi? Ndio hilo ambalo tungalipenda Serikali itoe jibu au itoe maelezo, sio maelezo aliyotoa Mheshimiwa Waziri ya kusema tu kwa sababu gridi ya Ubungo inakwenda Zanzibar na kwa sababu gridi ya Tanga itakwenda Pemba, hilo halitoshelezi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba tupate ufafanuzi katika suala hili.

Tatizo lingine ambalo nahisi lina matatizo katika Wizara hii ni suala zima ambalo mara nyingi nilikuwa nalisoma kwenye magazeti, nasikiliza kwenye redio, ni suala la kusikitisha kidogo. Kuna mtindo wa mafuta ya *transformer* kuibiwa kwa wingi sana. Sasa mafuta haya ya *transformer* yanayoibiwa yanasababisha hasara kwa Serikali. Nilikuwa najiuliza, *transformer* siku zote zinakuwepo juu au zinakuwepo mahali ambapo ni pa hatari sana, mimi ambaye sina uzoefu wa mambo ya umeme na mwingine yeyote, hawezi kwenda kufungua koki ya *transformer* akatoa mafuta kwa kujiamini; kwa hiyo

suala ni nini? Suala ni kwamba, lazima itakuwa ama ni wafanyakazi wenyewe wa umeme au ni watu ambao wameshastaafu na wanashirikiana na wenzao kuiba mafuta hayo. Sasa je, Serikali au Wizara, ina mpango gani wa kukomesha matatizo hayo? Nafikiri hiki kiwanda cha *ABB TANALEC,* Serikali ingelizungumza nao, wakaweza kuweka kitu ambacho itakuwa ni vigumu kukifungua, kwa wale wezi ambao wanakwenda wanaiba mafuta ya *transformer*. Sasa tukifanya hivyo *at least* tunaweza tukaokoa fedha nyingi sana ambazo zinapotea kutona na wizi huu.

Mheshimiwa Spika, gesi ambayo inapatikana na inatumiwa hivi sasa, bahati nzuri imeanza kutumika katika viwanda, sasa viwanda hivi kwa mfano, *Wazo Hill, Kioo, ALAF* na vinginevyo, madhumuni ya kutumia gesi ni kupunguza gharama za uzalishaji. Sasa ukitazama kwa mfano, *Wazo Hill,* kuanzia Julai, 2004 mpaka Juni, 2006, nafikiri habari nilizonazo ni kwamba, wameokoa kiasi cha *18.25 billion*, lakini ukitazama saruji yao bado inakwenda bei ya juu. Sasa mimi najiuliza, lengo ni nini; ni kuwasaidia viwanda wapate faida kubwa au kuwasaidia Watanzania? Ikiwa ni kuwasaidia Watanzania basi hatujafanya kitu, kwa sababu wao wameokoa kiasi cha *18.25 billion,* lakini bei ya mauzo ya saruji ni kubwa sana. Sasa kuna kitu gani hapo. Mimi Mheshimiwa Waziri, naomba hili ulitazame sana kwa faida ya Watanzania.

Jambo lingine ambalo ningelipenda kuzungumzia kidogo ni kwamba, Mheshimiwa Waziri alizungumza hapa juzi alipoulizwa kwamba, kutakuwa na gridi ya Taifa inayotoka Pangani kwenda Pemba, ni jambo zuri na tunamwombea afanikiwe na Mradi huu. Lakini navyofahamu mimi ni kwamba, Miradi kama hii inawekwa katika hotuba, inawekwa katika bajeti na inawekwa ili iweze kuchangiwa fedha ya kuendeleza katika Miradi hiyo. Sasa bahati mbaya, sikuona chochote katika hotuba, sikuona chochote katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri, je, Mradi huu utaanza katika mwaka huu wa 2006/2007 au utaanza miaka mingine inayofuata? Ningelipenda nipate maelezo kuhusu suala hili.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, ninakushuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia. Ahsante sana. *(Makofi*)

**MHE. FRED M. TUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Kwanza kabisa, kwa dhati, naomba niwapongeze Meshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, pamoja na watendaji wote ambao wameshiriki kwa pamoja, kuandaa hotuba ya bajeti ambayo inajadiliwa na Bunge lako Tukufu katika siku ya leo.

Mheshimiwa Spika, kutokana na taarifa mbalimbali ambazo zipo, Tanzania ina hazina kubwa ya madini ya aina mbalimbali. Tanzania ni tajiri kwa rasilimali lakini ni maskini kwa uchumi na maisha wanayoishi wananchi wake ni duni. Tangu mwaka 1926, Tanzania imekuwa inazalisha kwa kiasi kidogo, madini ya aina mbalimbali mfano dhahabu na almasi. Kama tulivyoelezwa na Wizara ya Nishati na Madini, wakati wa semina ya Wabunge kwamba, zipo hisia kubwa kwa wananchi ya kwamba, madini

tuliyonayo hayajatunufaisha ipasavyo. Hizo hisia zipo na Wizara iliweza kutueleza hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali ya Awamu ya Pili, hatua kadhaa zimechukuliwa kuendeleza sekta ya madini hapa nchini. Kulikuwa na wakati benki ziliweza kununua dhahabu, lakini Serikali ya Awamu ya Tatu, iliweza kukamilisha Sera ya Madini ya mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya mwaka 1998. Kutokana na kutekeleza Sera hii ya mwaka 1997 na Sheria ya Madini ya mwaka 1998, mafanikio katika Sekta ya Madini yalianza kuonekana. Kwa mfano, mchango wa Sekta ya Madini mwaka 1995 ulikuwa asilimia 1.4 na mwaka 2004 uliongezeka hadi kufikia 3.2 na mwaka 2005 ulifikia asilimi 3.5. Ni dhahiri kwamba, kuna haja ya kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tatu kwa hatua ambazo ilichukua, kuimarisha hii Sekta ya Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lengo la mchango wa Sekta ya Madini katika Pato la Taifa inatakiwa kufikia asilimi kumi ifikapo mwaka 2025. Hivyo, katika kufikia lengo hilo, hatua mbalimbali zinatakiwa zichukuliwe hasa na Serikali ya Awamu ya Nne.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie maoni yangu kuhusu hatua ambazo zinatakiwa zichukuliwe na hii Serikali ya Awamu ya Nne ili tuweze kuboresha Sekta ya Madini na iweze kufikia asilimia kumi kuchangia kwenye Pato la Taifa, ambayo tumeweka kwenye lengo letu. Lakini naomba nikiri kwamba, maoni yangu yanaegemea katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, ambacho naomba nichangie ni kuhusu fidia inayotolewa kwa wananchi wanaotakiwa kuhama kupisha utafiti au uchimbaji madini. Katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2005, ukurasa wa 43, kipengele cha (v), imeeleza bayana kwamba, utaratibu utawekwa, unaoleweka zaidi kuhusu fidia ambayo wanatakiwa wapewe wananchi wanaotakiwa kuhama, kupisha utafiti au uchimbaji madini. Kwa hiyo, inaonesha kwamba, kuna haja ya kurejea na kuipitia Sera ya Madini ya mwaka 1997, kama Ilani ilivyosema na ni jukumu la Serikali ya Awamu ya Nne kutekeleza hii Ilani ya Uchaguzi, ambayo iliwafanya wananchi kukichagua Chama cha Mapinduzi. Fidia inayotolewa kwa sasa, kwa kweli ni ndogo na hailingani na utajiri unaochukuliwa mahali pale na hauwezi kutosha hata kuwapa wananchi kuanza kujenga makazi mapya. *(Makofi)*

Chama cha Mapinduzi pekee, ndicho kilichotoa ahadi hii ambayo wananchi wengi waliikubali na wakakichagua Chama cha Mapinduzi. Kwa hiyo, maoni yangu ni kuiomba Serikali ya Awamu ya Nne itekeleze ahadi hii kwa wananchi. Jimbo la Kishapu kuna wananchi wa Buchambi, Songwa, Utemini, Konokelo na Idukilo, walipisha utafiti na uchimbaji wa almasi katika maeneo yao. Walipewa fidia kwa utaratibu wa sasa, nilioelezwa na viongozi wa Wizara ya Madini ni kwamba, wananchi wanaweza wakajadiliana na mwekezaji, wakishindwa kuelewana watalipwa fidia kufuatana na Sheria ya Ardhi, ambapo ndipo tatizo la wananchi na mimi naona ni tatizo. *(Makofi)*

Mwanachi anayeishi katika eneo lenye madini, kwa mfano, almasi imeanza kuchimbwa pale mwaka 1940, inajulikana kuna almasi pale. Mwananchi akipisha

kufuatana na Sheria ya Ardhi, atafidiwa kutokana na alivyoiendeleza ardhi pale na kwa kuwa wananchi wa kule ni maskini, hawawezi kuendeleza wakaja wakalipwa kiasi kinachowawezesha kuweza kuandaa makazi mapya na fidia ikatosha wakaweza kwenda kuishi mahali pengine, kupisha huo utafiti au uchimbaji wa madini. Kwa hiyo, wananchi wa Buchambi wamelipwa fidia lakini haikutosha kuwawezesha kwenda kutafuta makazi mapya. Naiomba Serikali ya Awamu ya Nne izingatie suala hilo la fidia.

Mheshimiwa Spika, la pili ni kuhusu huduma zinazotolewa na migodi katika maeneo yanayozunguka. Ilani ya Uchaguzi ukurusa wa 42(4), inazungumza bayana kwamba, utaratibu utawekwa ili maeneo yanayozunguka migodi yaweze kunufaika, kwa sasa huduma za jamii zinazotolewa na migodi hazitoshi, ni ndogo ukilinganisha na mapato yanayopatikana mahali pale. Huduma hizi zinatolewa kwa hiari ya wawekezaji, hawabanwi na sheria yoyote, wala hakuna mikataba ambayo inaweza ikawabana kwamba, watoe kiasi fulani, wanatoa kwa hiari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninachoiomba Serikali, itekeleze hii Ilani ya Uchaguzi kwa wananchi wanaoishi katika maeneo yanayozunguka migodi, hususan wananchi wanaoishi katika migodi ya almasi pale Mwadui, waweze kunufaika na uchimbaji wa madini hayo. Nashukuru kwamba, wawekezaji wa maeneo hayo, wanatoa misaada hata wakati wa njaa. Mwadui wametoa chakula Kijiji cha Magalata, *El-hilal Company* wametoa tani 60 kwa ajili ya vijiji vinavyozunguka. Lakini hiyo ni kwa hiari yake na tunashukuru kwa kufanya hivyo, ni uungwana mkubwa sana. Tunachoomba ni kwamba, kuwe na utaratibu maalum uliowekwa wa kuwezesha vijiji vya wananchi wanaoishi karibu na madini au karibu na migodi, waweze kunufaika ipasavyo, kulingana na utajiri unaotoka mahali pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kingine ni kuhusu kuwasaidia wachimbaji wadogo wadogo, taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri, inaonesha kwamba, kuna wachimbaji wadogo wadogo karibu milioni moja. Katika Ilani ya Uchaguzi imesema bayana kwamba, wachimbaji wadogo wasaidiwe kiteknolojia, kutafuta masoko ili waweze kuboresha uchimbaji huu wa madini na kama tutafanya hivyo, tutaweza kuongeza Pato la Taifa, kwa sababu uchimbaji utaongezeka na madini yatapatikana kwa wingi zaidi, kuliko sasa ambapo hatuwasaidii wachimbaji wadogo na uhusiano wa wachimbaji wadogo na wa migodini uimarishwe.

Naomba ule utaratibu au mpango wa *Diamond Development Initiative,* ambao umesemwa au umeelezwa, utekelezwe mapema iwezekanavyo, naamini utawasaidia wachimbaji wadogo wadogo na mahusiano ya wachimbaji wakubwa na wadogo yakiboreshwa, itasaidia.

La mwisho ni kuhusu nishati, naipongeza Serikali kwa mpango wa kusambaza umeme vijijini, utasaidia sana hasa katika maeneo kame, ambayo yamekata miti sana kutokana na matatizo mbalimbali. Sasa umeme ukipelekwa katika maeneo hayo, utasaidia kuboresha mazingira, kwani hawatakata tena miti kwa wingi.

Kwa hiyo, naomba vijiji vya Mwigumbi, Mipa na Bubiki, vilivyoko karibu na Mgodi wa Mwadui, Serikali ishawishi wawekezaji wa migodi hiyo, wasaidie kutoa umeme katika vijiji hivyo nilivyovitaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja, ahsate sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mbunge wa Simanjiro, Mheshimiwa Christopher O. Ole-Sendeka, atafuatiwa na Mheshimiwa Suleiman O. Kumchaya, aliyebadilishana na Mheshimiwa Gaudence C. Kayombo na wakati huo huo Mheshimiwa William M. Ngeleja, ajiandae.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Spika, naomba kwanza, nichukue nafasi hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi nyingine ya kuchangia katika Bunge hili na hasa kwa siku ya leo, kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. *(Makofi)*

Nachukua nafasi hii pia kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Simanjiro, kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Lawrence K. Masha na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati na Madini, kwa mambo makubwa mawili. La kwanza, kwa kuteuliwa na Rais kushika nyadhifa hizo za kuongoza Wizara hii muhimu sana, lakini la pili, kwa hotuba yao nzuri, ambayo wameiwasilisha leo asubuhi mbele ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nichukue nafasi hii, kwa niaba ya Wananchi wa Wilaya ya Simanjiro tena, kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete na Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Lowassa na Baraza la Mawaziri, kwa kutekeleza kwa dhati, dhamira ya Rais wetu ya kulitumikia Taifa letu, kwa moyo wake wote. Hili wamelifanya kwa vitendo na wamekwisha jipambanua na sisi Makada wa Chama hicho, kwa kweli tunatembea kifua mbele, kuona kwamba, sasa Serikali yetu inafanya yale ambayo tuliwaahidi wananchi wakati wa kuomba kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, sasa naomba nijielekeze kuchangia hotuba hii ya Waziri wa Nishati na Madini, Wizara ambayo inanigusa mimi na Wilaya yangu kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Spika, nimempongeza Rais, kwa dhamira hiyo ambayo ameionesha kwa vitendo, lakini kwa hoja ya leo, Wizara ya Nishati na Madini wote tutakumbuka kwamba, Rais wetu alielekeza kutazamwa au kupitiwa upya kwa mikataba ya madini. Kwa kuwa Wilaya yangu ya Simanjiro, sehemu kubwa kama mnavyojua, ina madini mengi ya vito ikiwemo *Tanzanite, Rubby, Green Garnet* na madini mengine. Lakini kipekee leo nitajielekeza sana kwenye madini ya *Tanzanite,* ambayo ni madini ya aina yake, ambayo kwa kweli kama mnavyojua, yanapatikana Wilaya ya Simanjiro tu au Tanzania na hayapatikani mahali pengine popte duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaunga mkono mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Uwekezaji na Biashara ya kuundwa kwa Kamati ya Bunge, itakayopitia mikataba hii ya

madini ili kuendelea kuweka uwazi na kujenga ushirikiano au ushirikishwaji wa wananchi kupitia kwa wawakilishi wao. Kwa kweli tukifanya hivi, wananchi wataona kwamba, wamewakilishwa vema na hata sisi Wabunge wao, tutaweza kutetea mikataba hiyo maana tutakuwa tunajua undani wa mikataba yenyewe. Kwa sasa hivi, tuko gizani na hatuna la kuweza kwenda kusema mbele ya wananchi, kwa sababu mikataba yenyewe wanaijua watendaji walioweka saini na makampuni ambayo wametiliana saini. Kwa hiyo na mimi naunga mkono hoja au pendekezo la Kamati na la Wabunge wenzangu, la kuundwa kwa Kamati ya kushughulikia au kuona mikataba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibu Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, alifanya ziara katika Jimbo langu, kufuatia maelekezo ya Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa nia ya kushughulikia baadhi ya kero za wananchi katika Jimbo hilo la Simanjiro na hususan katika maeneo ya Machimbo ya *Tanzanite* pale Mererani. Kwa kweli napenda kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza, kwa kweli kwa kufanya kazi moja nzuri ya kuweka bayana baadhi ya mambo ya msingi, ambayo yalikuwa yanaleta utata miongoni mwa wachimbaji wakubwa na wachimbaji wadogo. Lakini bado nasema kilio cha wachimbaji wa madini ya *Tanzanite* pale Mererani bado ni kikubwa.

Mheshimiwa Spika, wananchi walimwomba Waziri aweke bayana *report* ya Tume zilizoundwa na wale Mawaziri waliomtangulia, ikiwemo Ripoti ya Jenerali Mstaafu Mboma, Kamati ambayo iliundwa na Waziri wa wakati ule Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo na kama si yeye ni Mheshimiwa Daniel N. Yona.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo.

**MHE. CHRISTOPHER O. OLE-SENDEKA:** Mheshimiwa Edgar D. Maokola-Majogo. Sasa wananchi wa Mererani wamenituma niendelee kumwomba Waziri kwamba, Ripoti za Tume zilizokuja kushughulikia kero za Mererani, ziwekwe wazi ikiwemo hiyo ya Jenerali Mstaafu Mboma.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, aliwaaahidi wananchi kwamba, ataweka wazi Ripoti hiyo na kwamba, ningependa pia alieleze Bunge hili baadaye kwamba, ni lini Ripoti hizo zitakuwa hadharani ili kiu hiyo ya wananchi iweze kwisha.

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo langu la Simanjiro, wanakiri na kuthamini sana ziara hiyo ya Waziri, lakini zipo ahadi nyingine ambazo Waziri alizitoa katika kulinda mazingira. Waziri aliwaondoa wachimbaji wadogo waliokuwa wakichekecha maeneo ya madini, yanayozunguka vitalu vilivyokuwa vimepimwa kwa nia ya kunusuru mazingira, lakini Waziri pia aliwaahidi wachimbaji wadogo wale kwamba, atawatafutia eneo.

Mheshimiwa Spika, ni imani yangu kwamba, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, Waziri wetu wa Nishati na Madini, leo tena au kesho atatoa kauli ya kuwaeleza wale wananchi wa Mererani kwamba, lini atawapa maeneo yale kama alivyowaahidi,

baada ya miezi miwili atatekeleza. Najua haijaisha, lakini ndiyo inakaribia karibia ili wale waendelee kufarijika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, madini ya *Tanzanite* ni *unique* na hapa ndipo mahali ambapo ningependa sana kuchangia kama nilivyosema, ni *unique* kwa sababu hayapatikani mahali pengine popote duniani, yanapatikana Simanjiro tu ndani ya dunia hii yote mnayoijua. Ni *unique* kwa sababu hata mwamba wake, umekaa mshazari, yaani inakwenda *horizontally* ikitoka Kusini Magharibi kuelekea Kaskazini Mashariki kulenga Mlima Kilimanjaro. Kwa maana hiyo, kwa sababu inakwenda *horizontally,* Sheria ya sasa ya Madini, ambayo inaweka mipaka *vertically* na kwa kuwa wachimbaji wadogo wale wanapewa maeneo mafupi ya mita 50 kwa 50, anapoweka shafti ya kuteremka chini akianza kwenda kutambaa *horizontally,* anajikuta ameshavuka ile mita 50 na ameingia katika eneo la mtu mwingine kwa mujibu wa sheria ya sasa ya madini.

Mheshimiwa Spika, ombi la wachimbaji wadogo ni kutazamwa upya au kuwekwa kwa kanuni ya uchimbaji wa madini ya *Tanzanite,* ambayo itakuwa ni tofauti na uchimbaji wa madini mengine ya vito, ili kuepusha mgogoro wa sasa au mitafaruku ya sasa inayotokea kati ya wachimbaji wadogo na wachimbaji wakubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa faida ya Bunge lako Tukufu, nimependa tu kueleza kwamba, wachimbaji wadogo wamepewa maeneo ya mita 50 kwa 50, lakini makampuni makubwa yana maeneo makubwa, ambayo wanaweza kuogelea kwa kadri wanavyoweza kwenda mita 1,000 au zaidi. Kwa hiyo, unakuta kwamba, wachimbaji wale wadogo ambao wamekwisha wekeza nguvu zao nyingi, kwa sheria ya sasa ya madini, kwa kweli haiwapi fursa ya kuweza kurejesha nguvu walizoziwekeza katika uchimbaji wa majini. Ni kwa maana hiyo, kutokana na umuhimu na kipekee wa uchimbaji wa madini ya *Tanzanite*, naomba kupendekeza kwa niaba ya wananchi wa Simanjiro kwamba, sasa Serikali iitazame upya Sheria hiyo ya Madini au iweke kanuni itakayobainisha au itakayodhibiti uchimbaji wa madini ya *Tanzanite,* tofauti na madini mengine.

Mheshimiwa Spika, ningependa pia kuchukua nafasi hii, kuwasilisha ombi lingine la wachimbaji wadogo wa Mererani wa machimbo ya *Tanzanite* mbele ya Bunge lako Tukufu la kupewa soko la madini ya vito katika eneo lile la Mererani. Kama mnavyojua, Uwanja wa Kimataifa wa *KIA* upo kilomita 20 kutoka kwenye machimbo yetu na kwa maana hiyo, iwapo soko lile litawekwa Mererani, basi ni dhahiri kwamba, wanunuzi wa madini na wale wanaouza, wataweza kutumia Uwanja wa Kimataifa kuja Mererani. Wakati huohuo wale wenye madini, wataweza kuuza kwa urahisi. Kwa hiyo, napendekeza soko lile kama ambavyo limependekezwa na Kamati ya Uwekezaji na Biashara, liwekwe katika maeneo hayo ya madini ya *Tanzanite* pale Mererani.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila, kama nisipotumia nafasi hii, kuishukuru Serikali ya Awamu ya Nne, chini ya Mheshimiwa Rais Jakaya Mrisho Kikwete, kwa kutuahidi na leo Waziri wa Nishati na Madini, amesoma kabisa hapa kwamba, sasa umeme utapelekwa Makao Makuu ya Wilaya ya Simanjiro Orkesmet. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaishukuru Serikali ya Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, kwa sababu Rais alituahidi mambo makubwa matatu. Alituahidi kwamba, umeme utakwenda Orkesmet; alituahidi kwamba, atahakikisha kuwa tunapata barabara ya lami kutoka *KIA* kwenda Mererani; na alituahidi pia kwamba, atashughulikia matatizo ya wachimbaji wadogo na katika kulishughulikia hili la umeme, tayari tumeshaelezwa. Katika kushughulikia matatizo ya wachimbaji wadogo, Waziri wa Nishati na Madini, amekwishafika na ninamshukuru kwa hilo, ila tu nataka kumwambia kwamba, yale mengine ambayo hayajapatiwa ufumbuzi, sasa ajielekeze huko.

Jambo lingine ambalo ningependa kuiomba Serikali sasa ni Waziri ashughulikie kupatikana kwa Kamishna wa Madini, kwa sababu hilo nalo limekuwa ni tatizo, kwani mwenye mamlaka ya kutoa *Primary Mining Licence* na *Master Dealers Licence*, nafikiri ni Kamishna. Kama hivyo ndivyo, basi ni muhimu sana kupatikana kwa Kamishna haraka ili leseni hizo ziweze kutolewa kwa wakati unaostahili.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo Wilaya nyingine zinapata kodi kwenye Halmashauri zao, dola 200,000 kwa upande wa Simanjiro, ambapo madini ya *Tanzanite* yanapatikana, nitaomba ushirikiano mkubwa sana wa Wizara ya Nishati na Madini kwa sababu *Dealers* wote kama watasafirisha madini kupitia Dar es Salaam, Arusha au mahali pengine. Lakini ni lazima wataainisha kwamba, ni madini ya *Tanzanite*, basi asilimia ile ambayo inapaswa kulipwa kwa Halmashauri husika na kwa sababu sina wa kugombana naye kuhusu *Tanzanite,* basi Wizara inisaidie ili Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro iweze kupata kodi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Serikali itafanya hivyo, itakuwa imeweza kutusaidia sisi wananchi wa Wilaya ya Simanjiro.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kwa heshima na taadhima, niunge mkono hoja kwa moyo wangu wote na kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SULEIMAN O. KUMCHAYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa, nagependa kukushukuru wewe, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Nishati na Madini.

Pili, napenda niipongeze Wizara hii inayoongozwa na Waziri mzoefu, Ndugu yangu, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, kwa hotuba nzuri, yenye kuleta matumaini ya kupatikana kwa umeme katika nchi yetu, akisaidiwa na kijana wetu mchapakazi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Lawrence K. Masha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ningependa tukumbushe tu nishati na maendeleo ya nchi au Dunia kwa ujumla na hapa ningependa kutoa mifano hai, nasema tunakumbushana, hakuna geni hapa. Mwaka 1917, Urusi ama wakati ule *Union of Soviet Socialist Republic,* ilikuwa nchi ya kwanza kabisa, kujenga ujamaa katika dunia na kipindi kile kulikuwa na ubepari wanasema ubepari usiokuwa na huruma, ulikuwa unavamia kila eneo la uchumi popote pale katika dunia hii. Lakini Urusi ilisimama kidete chini ya

Mwanafalsafa, Vladmir Elich Lenin, aliyetafsiri kwa vitendo dhana ya *Marxism*, iliyoundwa na Marx aliyefia London.

Kitu cha kwanza kabisa, baada ya mapinduzi hayo ni kusambaza umeme katika nchi nzima na wengi hapa tumesoma Urusi, ni nchi kubwa katika dunia huku *Sunset* na huku *Sunrise,* lakini waliweza kuifanya kazi hiyo ya *electrification*. Matokeo ya kazi hii katika vita vya pili mwaka 1945, Warusi waliweza kumpiga Mjerumani, pengine kwa taarifa tu ndiyo waliompiga Mjerumani katika dunia katika vita vya pili. Waliweza kuhamisha viwanda vyao, wakavipeleka katika maeneo ambayo vita havijafika, lakini kwa sababu tu waliweza kusambaza umeme katika nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, utaona uzito wa umeme katika kuleta maendeleo, wasingefanya vile, Warusi wangepigwa na Wajerumani. Viwanda vingeteketea, watu wangeteketea na wasingeweza kuimarisha siasa yao ya ujamaa na sisi wengine tukaiga. Si Urusi tu, ndugu zetu China, wao walifanya Mapinduzi Oktoba, 1949, baadhi yetu tulikuwa bado hatujazaliwa hapa, wakaiga mfano huu huu wa kueneza umeme katika nchi yao, walipoamua kuleta *Economic Reform,* kilichowasaidia ni umeme katika nchi nzima. Matokeo yake, *Economic Growth Rate,* ilikwenda juu kwelikweli kwa sababu kulikuwa na uzalishaji wa nchi nzima, kwa sababu walikuwa na umeme. *(Makofi)*

Kama walivyozungumza wenzangu waliotangulia, mwaka 1960, Tanzania na Uchina hatukuwa mbali sana, lakini baadaye wakagundua kwamba, kumbe wana umeme, wakaanza kwenda kwa kasi katika kujiletea maendeleo katika nchi yao na kwa sababu hiyo, waliweza kutusaidia sisi. Miaka 20 tu ya Uhuru wao, wamekuja kujenga Mradi mkubwa katika Afrika, Reli ya *TAZARA,* kwa sababu ya umeme katika nchi yao.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimetoa mifano yote hii ili kuonesha jinsi gani umeme ni muhimu katika maendeleo ya nchi yoyote ile, pamoja na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, sisi hatukuanza na hili, tulisema kupanga ni kuchagua lakini nasema hatujachelewa sana, ingawa tumechelewa. Kwa maana hiyo basi, kwa dhana hii ya Ari Mpya, Nguvu Mpya na Kasi Mpya, kuna haja ya kubeba uzito huu wa umeme katika nchi na kuimarisha vyombo vyetu, ambavyo vimepewa majukumu ya kuleta umeme katika nchi yetu. Nimeona hapa jinsi Wizara ilivyojizatiti katika kuleta umeme katika nchi yetu kwa kutumia *REA* na *REF,* sasa ninaomba kwamba, haya yatekelezeke hata kwa kuongeza kuomba misaada kutoka kwa wenzetu wengine ili usambazaji huu wa umeme vijijini uwezekane. Kupeleka umeme vijijini, kusiwe ni mahaba, kusiwe ni mapenzi, kusiwe ni huba, bali upelekwe kwa kujua kwamba, tunatengeneza maendeleo ya nchi yetu ili na sisi tuwe kama nchi nyingine.

Mheshimiwa Spika, ningependa kuchukua nafasi hii, kumpongeza sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, kwa kufanya ziara na kwenda Mtwara katika Mkoa wangu na kufika *Mnazi Bay,* akajionea hali halisi ya Mradi ule na akatoa maelekezo palepale *(guidance on the spot)*, ninampongeza sana. *(Makofi)*

Kwa maana hiyo basi, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha, kwa kumpeleka Waziri Mkuu pale, maana yalikuwa yanazungumzwa mengi tu ya kukatisha tamaa ili Mradi ule usiwezekane. Lakini Waziri Mkuu amekwenda, ameona na ninaambiwa ametoa maelekezo palepale. Maelekezo ambayo yameleta matumaini makubwa kwa watu wa Mikoa ya Kusini, yaani Mtwara na Lindi, ili na sisi Lindi na Mtwara kupambazuke, umeme uwe wa uhakika.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo, kama si hili la *Mnazi Bay,* pengine leo ningekuwa na lugha nyingine ya kuzungumza katika Wizara hii katika vijiji vyetu vinavyotaka umeme katika maeneo yetu. Kulikuwa na maombi katika Jimbo langu Kijiji cha Mbuyuni, Luwatala, Nanjota na Mnavira ambao walikubali kuchangia ili umeme ufike katika maeneo yao, maana na wao wana mwamko wa kupenda maendeleo ili na ninyi mpende kuja Kusini.

Mheshimiwa Spika, sasa Ndugu yangu, Mheshimiwa Dr. Ibrahim S. Msabaha leo ni kukupongeza tu kwa hili, lakini naomba usirudi nyuma, ule Mradi wa *Mnazi Bay* ukianza tu, basi vijiji hivi na vijiji vingine vya Mikoa ya Mtwara na Lindi, viweze kupata umeme. Mimi nawaambieni, mkipeleka umeme katika mikoa ile, barabara za Dar es Salaam zitaanza kukosa Wamachinga, maana wataamua kurudi nyumbani, wakashiriki katika maendeleo kwa sababu umeme upo katika viwanda vidigo vidogo na maeneo mengine ambayo yanahitaji umeme.

Mheshimiwa Spika, ninaanza kupata uzoefu Bungeni hapa, nisingependa nipigiwe kengele, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Suleiman Kumchaya. Namwita sasa Mheshimiwa William M. Ngeleja, ilikuwa afuatiwe na Mhehimiwa Kilontsi M. Mporogomyi, lakini naona wasemaji wangu wanaanza kugwaya, sijui kwa nini lakini sijui Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi, unaweza kuchukua nafasi? Kama inawezekana basi ni vizuri, kwa hiyo, akishamaliza Mheshimiwa William M. Ngeleja, atafutiwa na Mbunge wa Kigamboni, Mheshimiwa Mwinchoum A. Msomi.

**MHE. WILLIAM M. NGELEJA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kuwashukuru sana, Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri wake, Mheshimiwa Dr. Lawrence K. Masha, Katibu Mkuu katika Wizara hii, pamoja na timu nzima ya Watendaji katika Wizara. *(Makofi)*

Naungana na wenzangu kuwapongeza kwa kazi ambayo mmeifanya na hasa hotuba ambayo tumeipata ambayo tunaijadili leo. Hotuba iliyotolewa asubuhi na ambayo kitabu chake tunacho, ilikuwa nzuri sana, imejaa matarajio na matumaini. Lakini kama ilivyo kawaida, katika kitu chochote kilicho chema, hakikosi kasoro ama pengine kilicho kizuri huwa hakikosi nafasi ya kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, naomba nichangie mambo ambayo nadhani kwamba, kwa kuunganisha na yale ambayo wenzangu wameyasema, pengine yanaweza kuboresha zaidi mipango ambayo tunayo kuendeleza nishati na madini.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla ya kufika huko, naomba nitoe shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Rais, mchango wangu wa kwanza katika hili, naanzia katika suala la kupitia upya Mikataba ya Madini, pamoja na kuboresha Sera na Sheria ya Madini, pale ukurasa wa 23 na 24.

Ni wazi kwamba, tumekuwa tukiongea kwa muda mrefu sana, masuala haya na mojawapo ya masuala ambayo yamekuwa yakiongelewa kwa uchungu sana na Waheshimiwa Wabunge, lakini na wananchi kwa ujumla, ni kuhusu mikataba na mojawapo ya mikataba ambayo imekuwa ikilalamikiwa ni Mikataba ya Madini.

Mheshimiwa Spika, tunafarijika sana kuona kwamba, mjadala huu wa kupitia Mikataba ya Madini, kwa dhati kabisa umeanzishwa na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne.

Inatupa matumaini na kwa sababu tumekuwa tukisema siku zote kwamba, kazi kubwa kabisa ya hizi nguzo kuu tatu za dola, ni kusaidiana basi tunaamini kwamba ni wakati muafaka Bunge hili Tukufu, kusaidiana na Serikali, kuipitia hii mikataba kwa maslahi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi niongelee suala la *Corporate Tax*, tumekuwa tukisema siku nyingi kwamba, kweli ukiangalia hali halisi ilivyo, rasilimali tuliyonayo na kile ambacho tunakipata, nadhani imekuwa ni dhahiri kwamba, tunachokipata kwa kweli kimekuwa hakitoshi na tunadhani tunastahili kiasi kikubwa kuliko.

Haya ndiyo yanajidhihirisha sasa hivi, inaonekana sasa nadhani pande zote zinaanza kuimba wimbo mmoja, ni jambo zuri sana.

Mheshimiwa Spika, niiombe au niishauri Serikali, pamoja na kwamba tunafanya haya mambo, tunajadili sasa na Serikali, Sera na nia njema iliyopo ya kubadilisha Sheria, nisisitize kwamba, kwa kweli jambo hili linahitaji kufanyika kwa haraka zaidi.

Wawekezaji ni wenzetu, tumekuwa nao kwa muda mrefu na tutaendelea kuwa nao kwa sababu tunawahitaji na kwa sababu tunawahitaji, hatuwezi kufanya kazi za maendeleo bila kuwa na ushiriki wa wenzetu, wanaotoka nje ya nchi ama wa ndani.

Lakini kwa hili, kwa kweli tunahitaji kulichukulia kidharura tupate hii kodi tunachokipata kwa sasa hivi ni kidogo sana na ni vema tukalifanya hili, Serikali ifanye haraka kuleta Muswada ambao utabadilisha sheria ili *Corporate Tax* ianze kulipwa mara moja.

Mheshimiwa Spika, lakini pia nitumie nafasi hii, kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa kuweza kufanya majadiliano, ambayo yamefikia muafaka na wawekezaji.

Sasa tunaambiwa na tumeshuhudia hivi karibuni kwamba, dola 200,000 zimelipwa na wawekezaji wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini katika Halmashauri mbalimbali hapa nchini. Hii ni hatua mojawapo, ambayo inalenga kuboresha maslahi ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, lakini siamini kama inatosha na ninadhani wenzangu wamekuwa wakilisema hili, dola 200,000 hazitoshi. Nilikuwa nashauri kwa sababu tumeelezwa kwamba, kilichokuwa kimekwamisha kwa maeneo ambayo kumekuwa na mikataba hii ya maendeleo, ambayo makampuni hayo ya wawekezaji yalipaswa yalipe hizo dola 200,000 tangu walipoanza kuchimba au tangu walipoanza uzalishaji wa madini katika maeneo husika ni utata wa tafsiri ya kisheria kati ya Mikataba hiyo, lakini pia na sheria zinazotawala Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa sababu muafaka umefikiwa na kama walivyosema wenzangu basi malipo haya ama hizo dola 200,000 zianze kulipwa kipindi ambacho hao wawekezaji walianza kuzalisha.

Mheshimiwa Spika, ukiangalia hii hotuba katika ukurasa wa 24 kilichokuwa kimekwamisha si kwamba hapakuwa na vifungu vya namna hii, hivi vilikuwepo, lakini kulikuwa na utata katika tafsiri, ndiyo maana nasisitiza kwamba wawekezaji kama wale walioko Nzega pale *Resolute* nadhani ni sahihi walipe *arrears.* Lakini pia katika sehemu zingine ambako kumekuwa na hii mikataba, *Development Agreement* ambayo imekuwa iki-*specify* kuchangia hiki kiwango cha fedha ambacho ni dola 200,000 kwa Halmashauri ambazo hizi shughuli za uchimbaji zinafanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naungana na wenzangu kwamba suala la kulipa *arrears* ni sahihi na linastahili kwa hizi Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo nilitaka kusisitiza sheria yetu ifanyiwe marekebisho na mojawapo ya mambo ambayo tunatakiwa kufanyia marekebisho nadhani ni haya mamlaka ambayo anakuwa nayo Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana katika Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, kuna kifungu pale kinasema; "Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ana mamlaka kwa hiari yake, ana *discretionary powers* za kuweza kuingia mikataba kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mambo mbalimbali likiwemo suala la mazingira. Lakini pia kwenye kuchangia shughuli mbalimbali za maendeleo na pia kusuluhisha migogoro."

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kwa jinsi lilivyo ni suala la busara yake Mheshimiwa mwenye dhamana atakayekuwepo wakati huo. Sasa nadhani ni wakati wa kurekebisha hizi sheria. Naishauri Serikali kwa sababu lilikuwa linatumika neno *may,* sasa tutumie neno *shall* kwa maana kwamba lile ni jukumu la msingi katika utekelezaji

wa masuala ya madini. Liwe ni suala la lazima kwamba popote pale ambapo kunafanyika uchimbaji wa madini hasa uchimbaji mkubwa basi wawekezaji wawajibike kulipa hicho kiwango na kwa kufanya hivyo, itaendana tu na maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Fred Tungu Mpendazoe, amesoma hili katika ukurasa wa 42, ile Ibara ya 39 kipengele cha 4 kinasema: "Kupitia upya sera ya madini kwa lengo la kuboresha katika maeneo mbali mbali yakiwemo yafuatavyo." Kipengele cha nne kinasema; "Utaratibu tutakaoweza kuweka kwa makusudi kwa lengo la kuyawezesha maeneo yanayozunguka migodi kufaidika zaidi na harakati za migodi hasa katika kurekebisha athari za kijamii na kimazingira zinazotokana na uchimbaji wa madini."

Mheshimiwa Spika, mimi naamini kama tutarekebisha hicho kifungu kisiwe hiari au busara ya Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana wa kipindi hicho ikawa ni jambo la lazima. Nadhani tutakuwa tumefanikiwa kutimiza maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niongelee jambo lingine. Tunaongelea uboreshaji wa sera nzima ya madini, lakini pia na sheria zinazotawala shughuli za madini. Lakini tuna tatizo kidogo mimi naliona katika hili na pengine ni changamoto niseme kwa sasa kwa hali ambayo inatuzunguka. Tumekuwa hatuna Kamishna wa Madini kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa. Nina imani kwamba hili ni tatizo, yawezekana kutokuwepo kwake si kukwamisha shughuli. Lakini ukiangalia ile mantiki kwa nini sheria inasema kwamba lazima awepo mtu wa namna hiyo Kamishna wa Madini, jibu rahisi kibusara litakuelekeza kwamba majukumu aliyonayo ni msingi katika Maendeleo ya Sekta yetu ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, mimi naishauri Serikali ifanye haraka kukamilisha uteuzi wa Kamishna kwa sababu tunajua kwa kutokuwepo kwa Kamishna wa Madini sasa hivi kuna migogoro mingi sana na hasa kwa jinsi sheria ilivyo. Mtu anaweza kukwambia kwamba kutokuwepo kwake Kamishna wa Madini kama nilivyosema hapo awali si tatizo, lakini ni tatizo. Kwa sababu sheria ilivyosimama inasema kuna mambo ambayo hayawezi kufanywa na mtu zaidi ya Kamishna na mojawapo ni matatizo ya migogoro ambayo inatokana na utafiti na uchimbaji wa madini.

Mheshimiwa Spika, sasa jambo hili kwa kweli tunaweza kusema tu lilishawaumiza wananchi wengi, wawekezaji wa nje na wa ndani, lakini pia na wananchi ambao kwa kutumia haki waliyonayo kisheria wameshafungua tayari mashauri mbalimbali katika Wizara hii ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye hima na ifanye haraka migogoro hii imekuwa ya muda mrefu na tunafahamu kisheria kwamba haki iliyochelewa ni sawa sawa na haki iliyodhulumiwa. Kwa hiyo, ninaamini kwamba pengine sasa kupitia Bunge hili Tukufu wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana

atatuambia ni lini uteuzi wa Kamishna mhusika utakamilika ili shughuli zingine ziendelee kufanyika. Nafahamu mambo mengi sasa hivi hayajafanyika.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ambalo nataka niongelee ni usambazaji wa nishati na hasa umeme vijijini. Kwa taarifa nilizonazo mimi kama mwakilishi wa Jimbo la Sengerema, Sengerema ni kati ya Wilaya ambazo zimebahatika kuwepo katika Mpango Maalum wa Usambazaji Umeme Vijijini hasa huu unaoitwa *Energy Rural Transformation (ERT)* awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Spika, taarifa nilizonazo ni kwamba mwaka jana, wataalam kutoka Benki ya Dunia walikwenda kule Sengerema wakafanya utafiti katika maeneo mbalimbali ambapo mradi huu ungeweza kufaidisha wananchi. Lakini pia taarifa nilizonazo ni kwamba mwanzoni mwa mwaka huu wataalam kutoka *TANESCO* Makao Makuu na hasa Kitengo cha Umeme Vijijini walifika Sengerema kuweza kuona maendeleo kwa jinsi gani mradi huu utawafaidisha wananchi wa vijiji mbalimbali. Nafahamu kuna vijiji ambavyo vimetengwa pale ikiwemo Nyamililo, Igalagalilo, nafahamu kuna Katunguru na Chifunfu, Kamang na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba wakati wa majumuisho Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya Nishati na Madini anisaidie na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Sengerema na Wilaya ya Sengerema kwa ujumla kwa sababu mradi huu ni wa Wilaya nzima kutueleza hatua zilizofikiwa na nini kinachosubiriwa sasa hivi katika kutekeleza mradi huu ambao utawafaidisha wananchi na itakuwa ni changamoto kubwa sana kuharakisha maendeleo ya wananchi wa Jimbo la Sengerema na kwa kufanya vile tutakuwa tunalisukuma gurudumu la maendeleo ya wananchi wa Tanzania.

La mwisho, ni ombi, naiomba sana Serikali iweze kuona ni kwa jinsi gani inaweza kusaidiana na wananchi tusambaze umeme kwa sehemu ambazo ni vyanzo vya uzalishaji kwa ajili ya kujipatia fedha kama Taifa. Naongelea vinu vya kuchambua pamba popote vinapopatikana vikiwemo vilivyoko katika Mkoa wa Mwanza. Nadhani nilishawahi kuongelea huko nyuma, lakini naishauri Serikali ione uwezekano wa kufanikisha hili kwa faida ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narudia tena kusema ninawapongeza sana Mheshimiwa Waziri hasa kwa jinsi ninavyomfahamu yeye ni *nationalist.* Nakumbuka kuna siku ambayo yeye alipewa taarifa iliyokuwa imeandikwa Kiingereza lakini aliikataa akasema iandikwe kwa Kiswahili. Hii ni ishara kuonyesha ni jinsi gani ana uchungu wa maendeleo ya nchi yetu. Lakini nampongeza sana Mheshimiwa Lawrence Masha, kwa jinsi ambavyo amekuwa mwepesi kutatua matatizo ambayo sisi kama wawakilishi wa wananchi tumekuwa tukienda katika ofisi yao kuweza kusukuma gurudumu la maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. MWINCHOUM A. MSOMI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Awali ya yote nachukua fursa hii kuipongeza Wizara ya Nishati na Madini kwa jinsi ilivyoandaa hotuba yao ambayo kwa kweli ina matumaini kwa wananchi wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pili, nampongeza kipekee Mheshimiwa Waziri kwa jinsi anavyojituma. Kwa hakika Watanzania wanamwona jinsi anavyohangaika katika nchi yetu kuwatafutia wananchi huduma ambazo kwa kweli wanastahili kupewa kama Serikali ilivyopanga katika mipango yake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuanza kuchangia kuhusu suala la gesi. Ninavyokumbuka katika miaka ya 1982 na mwaka 1983 kulifanyika uchunguzi wa kuchimba mafuta eneo la Kimbiji katika Tarafa ya Kigamboni. Kwa bahati nzuri kwenye taarifa ya *TPDC* wenyewe wamesema *with gas shows* miaka yote miwili. Kwa maana hiyo, kuna dalili ya kupatikana kwa gesi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba kutoa wito kwa Wizara hii wakati umefika sasa kujikita kutafuta nishati mbadala ya kutumia umeme ambayo kwa kweli inatusumbua kwa miaka mingi *hydro power* Naomba tujikite katika kutafuta gesi na dalili zipo. Katika mipango yake Wizara itazame Kimbiji kule vimechimbwa visima vitatu, kimoja baharini, ufukweni na kingine nchi kavu.

Mheshimiwa Spika, wataalam wamesema kwamba dalili ya gesi ipo. Naomba tuliangalie hili katika mipango yetu ya baadaye kama mwaka huu haiwezekani. Kwanza, tuangalie mfano wa ndugu zetu wa China wamepiga hatua sana kwenye matumizi ya gesi majumbani, kwenye matumizi ya magari na viwandani. Kwa hiyo, itatoa msukumo kwa wananchi vile vile kupunguza gharama za maisha katika matumizi ya petroli.

Mheshimiwa Spika, mchango wangu wa pili, tuna tatizo katika Kata moja pale inaitwa Kibada. Kwa muda mrefu wananchi wa Kata ya Kibada wamekuwa wakiomba umeme na kwa bahati nzuri umeme upo wanauchungulia pale kwa muda mrefu uliopita. Lakini kila wanapopeleka maombi yao kwa bahati mbaya huduma hiyo hawajafikiriwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kutumia nafasi hii ili wananchi hao waweze kufikiriwa wana Kibada kupata umeme ambao tayari uko karibu na wao. Ulipelekwa umeme kwa ajili ya kisima cha *TIPPER.* Sasa kwa mantiki hiyo hakuna sababu ambayo kwa kweli naona wasiweze kupatiwa huduma hiyo ambayo ni muhimu kwao. Nakuomba Mheshimiwa Waziri uliangalie hili.

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Mkoa wetu wa Dar es Salaam uko katika hatua ya kuendelezwa kimipango miji. Nahisi Wizara ya Nishati na Madini kwamba wakati sasa umefika kufikiria kutanguliza huduma katika mipango miji yetu kwa sababu umeme ni nyenzo kubwa katika maisha ya mwanadamu. Naiomba Wizara katika mipango yake ya baadaye ifikirie na kujikita hasa katika kutanguliza huduma katika mipango miji yetu, ukiacha Mkoa wa Dar es Salaam na Tanzania nzima kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, imekuwa kidogo moyo wangu ukinisuta kuna tatizo la uchimbaji mafuta Zanzibar. Mimi sioni kigugumizi kiko wapi? Sisi Tanzania Bara tuna migodi ya dhahabu na tuna madini ya kila aina almasi na kadhalika. Wenzetu Mwenyezi Mungu amewabariki wana dalili ya kupata mafuta kama tafiti zilivyosema mwaka 1956. Sisi tuna migodi na uchumi wetu umekua, tunaringia migodi hii. Sasa kwa nini wenzetu wa Zanzibar wana dalili ya kupata nafasi ya kujiinua kiuchumi tunashindwa kuwasaidia jamani?

Mheshimiwa Spika, pamoja na suala hilo lipo katika mazungumzo ya masuala ya Muungano, lakini kwa heshima na taadhima naiomba Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iangalie hili kwa ajili ya kuinua uchumi wa Zanzibar kama Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete alivyoahidi kuisaidia Serikali ya Zanzibar basi hapa ndipo pa kuanzia.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo katika Jimbo la Kigamboni katika Kata moja inaitwa Mjimwema. Nimewahi kuongea na Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, nimeongea na Waziri wa Maji na nimeongea na Waziri wa Utumishi, kuna kisima pale kililetwa miaka ya 1970 kwa heshima ya Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi. Kisima hicho ameendelea kukitumia Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi mpaka Idara Kuu ya Utumishi ilivyoweza kumchimbia kisima chake. Pamoja na kuchimbiwa kisima chake bado Mheshimiwa Aboud Jumbe, alikuwa anatumia kisima hicho. Wananchi walikuwa hawepewi maji mpaka atosheke yeye na ajaze maji ndiyo baadaye yanafunguliwa sehemu nyingine wanapewa wananchi. Lakini baada ya kufuatilia kote huko Wizara ya Maji, nimewafuatilia Wizara ya Nishati na Madini na Wizara ya Utumishi, kila mmoja anasema suala hili si lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimechanganyikiwa, wananchi wananifuata Mbunge tunataka huduma ya maji. Kwa bahati mbaya mashine pale ni nzima, kuna tatizo la bili ya umeme ya muda mrefu, *TANESCO* wamekata umeme. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri anisaidie kutatua tatizo hili. Bili ya maji ilikuwa inakwenda kwa Mhandisi wa Maji wa Mkoa kwa heshima ya Mheshimiwa Aboud Jumbe Mwinyi, maana yake ni Serikali. Sasa baada ya kuchimbiwa kisima chake pale wananchi wameachwa wakihangaika. Huduma ya maji hawana kwa muda wa mwaka mmoja na nusu sasa hawana maji. Kulikuwa na mlipuko mkubwa pale wa kipindupindu Mjimwema kutokana na ukosefu kwa upatikanaji maji safi. Maji yapo lakini taratibu za Serikali zinawatesa.

Mheshimiwa Spika, naomba hili liangaliwe, Mheshimiwa Waziri azungumze na *TANESCO* ili wafunge bili iliyopo ya Mhandisi wa Maji Mkoa ipelekwe Serikalini. Tuko tayari sisi kufungua akaunti mpya kwa jina la Mwenyekiti wa Mtaa wa Mjimwema. Naomba Wizara iliangalie hili ili kuwanusuru wana Mjimwema na vile vile ni moja ya kuenzi heshima ya kiongozi wetu ambaye kisima kile kililetwa kwa heshima yake.

Mheshimiwa Spika, tuna tatizo la upatikanaji wa LUKU Mkoani Dar es Salaam. Katika kipindi cha Maswali na Majibu Mheshimiwa Mussa Zungu, alilizungumzia hili tumejibiwa. Lakini naomba Wizara ilitazame kwa mtazamo mpya, wananchi wameelewa umuhimu wa LUKU. Waheshimiwa Wabunge ofisi zetu kila siku zinapata kelele za

LUKU. Sasa naomba katika mipango madhubuti ya kuleta LUKU waitazame Dar es Salaam kwa macho mia mia.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. HERBERT J. MNTANGI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasa hii ili niweze kuchangia katika hoja hii ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, pamoja na viongozi wote na watendaji kwa kazi nzuri na kwa hotuba nzuri na mwelekeo mzuri na bila shaka sasa Wizara hii itakuwa inatekeleza majukumu na matarajio ya wananchi wengi hasa katika kuwapatia umeme.

Mheshimiwa Spika, ukitazama idadi ya miradi ambayo imeorodheshwa na Wizara hii kwa utekelezaji katika mwaka 2006/2007 utaona ni miradi mingi zaidi kuliko miradi ambayo imewahi kutokea katika bajeti zilizopita. Hii peke yake inaonyesha dhamira ya kweli na nia ya kweli ya kuongeza kasi katika utekelezaji wa miradi ya umeme na nia hasa ya usambazaji umeme katika maeneo mengi hususan maeneo ya Vijijini.

Mheshimiwa Spika, kama tutaendelea na kasi hii, nina hakika kilio cha wananchi wengi cha kukosa umeme kitaendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Haiwezekani yote ikakamilika kwa mwaka mmoja. Lakini nina uhakika matatizo yataendelea kupungua kwa kiwango kikubwa kama tutaendelea na kasi hii.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na maamuzi aliyoyafanya kuwekeza katika Mradi ule wa *Mnazi Bay* ili umeme uweze kupatikana na ndugu zetu wa Kusini waweze kupata umeme. Ni maamuzi ya kishujaa kabisa yenye lengo la kuondoa tatizo la umeme kwa Mikoa Kusini na Mikoa ambayo tumekuwa tukiisikia ikilalamika na kulia sana ndani ya Bunge hili kwa miaka nenda rudi. Sasa tunataka kuona kwamba umeme unapatikana na yale yote yaliyokuwa yakizungumzwa kwa miaka mingi yanabaki kuwa historia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niwashukuru sana watu wa *TPDC* ambao wanafanya maonyesho yao hapo, ni maonyesho mazuri ya kisayansi. Ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge ambao hawajapata nafasi ni vyema wakaenda pale wakaona. Kivutio kikubwa ni mpango ambao mmeusikia hivi karibuni wa kuweza kutumia gesi katika kuendeshea magari yetu. Huo mpango upo na naomba nirudie niliyoyasema siku chache zilizopita kwamba tujitahidi kuhakikisha kwamba mpango huu unatekelezwa ili tuweke historia katika Bara la Afrika kwamba Tanzania itakuwa miongoni mwa nchi chache za kwanza kabisa zitakazoweza kutumia gesi kwa kuendeshea magari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mpango huu na mradi huo gari lako litaendelea kuwa na uwezo wa kutumia dizeli na petroli kama unataka hivyo. Lakini litafungwa vifaa vipya vya kukuwezesha au kuliwezesha gari lako kutumia gesi. Utakuwa na hiari kwa wakati

wowote kwamba ukitaka kutumia gesi, unatumia gesi, kama unataka kutumia petroli na dizeli unatumia, lakini gari lako litabaki pale pale na utaweza kutumia dizeli na petroli, una *switch on* kwenye gesi na unaweza ukarudi uka *switch on* kwenye petroli na dizeli.

Mheshimiwa Spika, nawapongeza tena zaidi *TPDC.* Ukitazama mikataba yao ya uchimbaji wa mafuta ya petroli iko wazi kabisa na kama Wizara nyingine na wenzetu wengine wanaotengeneza mikabata wangeangalia mifano ya mikataba ya Shirika hili la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* wala migogoro mikubwa isingekuwa inatokea. Inaeleza wazi namna mwekezaji kama atafanikiwa kuvumbua mafuta atakapopata fursa za kurejesha fedha zake alizotumia kwa uwekezaji wa mpango ambapo wakati anarejesha fedha zake na wakati huo huo Serikali inaendelea kupata kodi zake kwa mpango mzuri wa uhakika. Naomba ndugu zangu mkipata nafasi tuangalie mambo makubwa na umuhimu yaliyopo ndani ya mikataba hiyo katika maonyesho yanayoendeshwa hapo na Shirika hilo la *TPDC.*

Mheshimiwa Spika, ushiriki wa *TPDC* katika miradi, hizi ni fursa ambazo kwa kweli ni muhimu sana na hivyo tunaiomba Serikali ione hilo kwamba ni vizuri wakaiwezesha *TPDC* ikashiriki katika fursa hizi za uwekezaji. Kama katika mradi wa Songo Songo na *Mnazi Bay, TPDC* wanayo nafasi kimkataba ya kushiriki kuwekeza kwa asilimia 20. Tusipoteze nafasi hii, ni muhimu sana kwetu hasa kwa kuiwezesha Serikali kupata mapato zaidi.

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi sana tumekuwa tukidhani njia rahisi ya kukusanya kodi na kuwezesha Taifa kupata fedha ni kuweka kodi kubwa katika mafuta ya petroli, dizeli na mafuta ya taa. Sasa tumefika mahali tumegonga mwamba, tumekwenda kwa kasi kubwa ya kukusanya kodi katika maeneo hayo na sasa ni vigumu kuendelea kwa kasi kubwa kuweka kodi katika petroli na dizeli, tumeshafika mahali tumegonga mwamba. Hivyo, ni vyema Serikali ikaangalia fursa kama hizi ambazo zinawezesha Taifa kupata kodi kutokana na uwekezaji maana yake bila kuwekeza usidhani kweli utapata, lazima twende kisayansi kama Taifa, wekeza ili uweze kupata na tena utapata kwa faida kubwa.

Mheshimiwa Spika, sasa juzi nilisema itakuwa vigumu sana kuwa na matarajio makubwa ya kushuka kwa bei ya petroli na dizeli katika vituo vya mafuta hapa nchini. Wote tumeshuhudia hilo bado haliwezekani. Kwa hiyo, tutumie fursa hizi za uwekezaji kuliwezesha Taifa kupata fedha zitakazotusaidia katika utekelezaji wa miradi yetu mikubwa badala ya kungojea kodi kwenye petroli na dizeli kiasi ambacho imefika mahali haiwezi kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, ningeomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kuangalia uwezo wa *TANESCO* kwa hivi sasa. Katika kipindi kilichopita *TANESCO* katika Mikoa yetu na Wilaya zetu walituandikia barua kwamba baadhi ya miradi itaweza kutekelezwa katika kipindi hiki cha mwaka huu 2006/2007 nini uwezo wa *TANESCO?* Miaka michache iliyopita Wizara ilikuwa inaomba fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi, lakini *TANESCO* kama *TANESCO* walikuwa nao wanatekeleza miradi yao kutokana na mapato yao *(own sources).*

Katika kipindi hiki cha mwaka huu *TANESCO* wana fedha kiasi gani watakazoweza kutumia katika utekelezaji wa miradi kutokana na mapato yao wao wenyewe. Nina wasiwasi kwamba *TANESCO* haitakuwa na uwezo mkubwa. Tumewafikisha mahali pabaya.

Mheshimiwa Spika, la mwisho, ningependa tuangalie kwa makini mkataba wa *IPTL.* Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilikwenda *IPTL* na tulionana na Meneja anaitwa Pasban nadhani, mambo aliyotueleza yanatisha, kwa sababu kuna *fixed capacity* kwenye Mkataba. Sasa ukitazama mashine zimenunuliwa miaka mitatu iliyopita, lakini gharama za *fixed capacity* zinaendelea hivyo hivyo kwa miaka yote 25. Hivi hatujui jamani kuna *depreciation.* Lazima tungefikiria kwamba kiwango hiki cha *fixed capacity* kingekuwa kinapungua mwaka hadi mwaka kwa sababu mashine zile zinaendelea kuchakaa. Lakini hilo halikuangaliwa, tunalipa hivyo na tutaendelea kulipa kwa miaka mitano. Wasomi wetu walioshiriki kitaaluma kuchambua mikataba hapo hawakuliona kwamba hilo ni tatizo? Lakini linatuumiza sana.

Mheshimiwa Spika, ni vizuri tukaangalia upya. Nilipowauliza mafuta wanayotumia pale kuendesha zile *turbines*, *fuel oil* wanainunua kwa kiasi gani, wakaniambia dola 390 kwa tani, hii bei ni kubwa sana. Ukitazama bei za mafuta katika soko la dunia dola 700. Kwa nini *fuel oil* iuzwe kwenye soko la dunia kwa dola 390.

Mheshimiwa Spika, mimi nimekuwa nikiagiza mafuta hayo kutoka nje. Nafahamu tofauti kati ya bei ya mafuta ya petroli na *fuel oil*. *Fuel oil* inakwenda kwa wastani wa theluthi moja ya bei ya mafuta ya petroli kwenye soko la dunia. Sasa kwa dola 390 wakati petroli inauzwa dola 700 unashindwa kuelewa. Hakuna mtu anayefuatilia na kufanya tathmini ya gharama halisi. *TANESCO* wanaandikiwa tu bili wanalipa, ili mradi Mkataba unasema gharama zote za kuendesha mashine zile *turbines* pamoja na *fuel oil* wanalipa *TANESCO.* Mmeona wapi mambo haya! Wewe unakodisha gari mafuta uweke wewe, *spare part* za gari hilo uweke wewe na bado gharama uendelee kuzilipa kama mwenye gari anavyotaka wapi na wapi mikataba ile. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tuangalie tumejiingiza mahali pabaya. Ni jambo moja ambalo tuliangalie kwa makini mikataba hii ilikuwa inaenda mpaka miaka 25. Sasa tunasikia kuna hila hila zinataka kufanywa, watu wanataka ku-*extend* mkataba wa miaka 25 kabla miaka 25 yenyewe haijakwisha, wana nia gani hawa? Wanaona wanapata faida kubwa sana, sasa wanataka kutufunika waongeze muda badala ya miaka 25 iwe miaka 30. Sasa wana-*renew* mikataba na kufanya *extension* kabla ya muda ule haujakwisha.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwanza kwa kunipa nafasi hii kwa sababu nafahamu nilikuwa mbali kwenye orodha. Lakini nadhani kwa hili niwashukuru wale ambao walikuwa wameomba halafu

wamesema hawatachangia leo. Tunawapongeza sana waendelee na mpango huo ili wengine tulio mbali kwenye orodha hiyo tupate nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hilo naomba kwanza nianze kwa kusema kwamba naungana na wale wote ambao kwa kweli wamechangia hasa kwenye ngazi ya Kitaifa. Kwa yale yote ambayo kwa kweli wamesema ni mambo muhimu sana.

Kwa hiyo, naungana na wenzangu kwa yale yote yaliyosemwa ili na mimi nisirudie sasa kwa sababu muda ni mfupi mimi nitajielekeza zaidi kwenye jimbo langu.

Mheshimiwa Spika, kwenye kitabu hiki cha njano ambacho kimeandikwa taarifa ya jumla kuhusu Sekta ya Nishati na Madini naomba kwanza sahihisho lifanywe kwamba kwenye ukurasa wa 17 vijiji vilivyoandikwa pale haviko kwenye jimbo langu. Kwa hiyo, sina hata kijiji kimoja isije ikaeleweka kwamba nina kijiji ambacho kimepata umeme mwaka jana, hakuna hata kimoja. Kwa hiyo, havipo kwenye jimbo langu. Naomba kwanza taarifa hiyo iwekwe sawa.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili ambalo ningependa nichangie kuhusu jimbo langu, la kwanza niseme Mkoa wa Manyara ulipata bahati ya kupata Ofisi ya *TANESCO* Mkoa mwaka jana tu. Kwa hiyo, mwaka jana ndiyo tumepata Ofisi ya Mkoa na Babati pale ni Makao Makuu ya Mkoa wa Manyara. Taarifa iliyotolewa pale na Mtendaji wa Mkoa Babati pale tuna kituo cha umeme wa gridi ya Taifa. Kituo kile kina uwezo wa *megawatts* 32. Lakini taarifa inaonesha kwamba matumizi mpaka mwaka jana mwezi Agosti ni *megawatts* 5.6 tu kati ya *megawatts* 32 na hayo ni matumizi ya Mkoa mzima wa Manyara. Hiyo ina maana kwamba tuna kituo kikubwa sana na wateja ni kama 5,872 tu mpaka wakati huo. Hii ina maana kuna tatizo kubwa la usambazaji wa umeme kwenye maeneo mbalimbali. Mimi naamini hali iko hivyo katika baadhi ya Wilaya kwamba usambazaji wa umeme ndio tatizo kubwa.

Mheshimiwa Spika, tumeambiwa hapa na wasemaji wengi wamesema kwamba umeme ndio silaha ya maendeleo na hakuna nchi yoyote ambayo inaweza kuendelea bila kuweka umeme sehemu zote katika nchi nzima, haiwezekani, huwezi kupata maendeleo. Tukiangalia vijiji ambavyo tayari vimepatiwa umeme sehemu mbalimbali utakuta maendeleo yao ni tofauti na vile ambavyo kwa kweli havina umeme. Huo ndio ukweli.

Kwa hiyo, kuna umuhimu sana wa kuhakikisha kwamba tunaweka kipaumbele kwenye umeme na hasa umeme vijijini. Sasa kwenye jimbo langu la Babati Mjini kwanza niseme kwamba mji wenyewe wa Babati bado baadhi ya mitaa yake ni giza na tuna kituo kikubwa kama nilivyosema, kwa hiyo tatizo ni usambazaji. Mitaa mingi haina umeme. Sasa naomba niombe tu kwamba kwa kweli basi *TANESCO* wapewe uwezo wa kusambaza umeme kwenye mitaa yote ya mji wa Babati.

Mheshimiwa Spika, lakini kubwa zaidi kuna mji mdogo unaoitwa Bonga na hili nadhani Mheshimiwa Waziri atakuwa shahidi. Wiki iliyopita Mheshimiwa Waziri alikwenda Babati kwa ajili ya ziara ya Mheshimiwa Rais kule Minjingu na nina hakika alipita njia ya Kondoa kuja Babati. Nina hakika Mheshimiwa Waziri ulipofika kwenye

mteremko wa milima ya Bonga uliona mandhari mazuri sana na ukateremka ukaukuta mji mdogo unaoitwa Bonga. Pale Bonga ule mji una huduma ambazo kwa kweli kama umeme ukipatikana nina hakika ule mji utaendelea vizuri sana. Kwanza tuna Shule ya Sekondari, pili sasa hivi kituo cha afya cha Bonga Serikali inapeleka ukarabati mkubwa kwa kituo kile kwa shilingi milioni karibu 52. Vile vile tuna taasisi za dini, vile vile wakulima wa eneo hilo la Bonga na Haraa ni wakulima wa zao la kahawa.

Mheshimiwa Spika, kahawa ndiyo inayotuletea fedha za kigeni na kwa maana hiyo ndiyo inayosaidia katika kujenga miundombinu katika nchi yetu. Kwa hiyo basi, na sisi wa Babati kule Bonga tupate basi na sehemu ndogo kwamba umeme utoke Babati kuja Bonga. Kwa kweli sio kilometa nyingi tu ni kama 15 tu kutoka kwenye kituo hicho kikubwa ambacho kina uwezo wa *megawatts* 32 kama nilivyosema na matumizi ni kidogo sana kwa sasa. Umbali kutoka Babati mpaka Bonga mpaka maeneo ya Haraa sidhani kama unazidi zaidi ya kilometa 20 kwenye kilometa 10 au 15 na umeme unaweza ukachukuliwa kutoka kijiji cha Singe ambapo kilomita zitakuwa zimepungua. Zaidi ya hapo unapokwenda Bonga unakuta vijiji vya Managa, Himiti halafu ndio unafika Bonga kwenyewe halafu unakwenda Haraa.

Kama nilivyosema pale tunalima mazao mengi, taasisi ziko nyingi na vile vile ni kituo kizuri Bonga kwa ajili ya magulio. Watu wengi wanakwenda pale na eneo hili la Bonga lipo kwenye barabara kuu ya Kaskazini *(The Great North Road)* inayotoka Babati kuja Dodoma. Vile vile Mheshimiwa Waziri ameeleza kwenye kitabu chake hapa kwamba vijiji vitakavyopewa ni vile ambavyo viko kandokando ya njia kuu ya umeme. Sasa Bonga ndiyo imefika basi iko hapo njiani na vijiji vyote nilivyovitaja hivi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba kwa kweli hili ndio ombi langu kubwa kwamba Bonga ipatiwe umeme na vijiji vyake vya Haraa, Himiti na vile vile Managa kwenye Kata ya Singe.

Mheshimiwa Spika, vile vile ningependa kwamba umeme usambazwe kwenye kijiji cha Halla uko umeme ambao unakwenda mji mdogo wa Gallapo ambao sasa baada ya kupata umeme kwa kweli maendeleo yake ni makubwa sana. Kijiji kimoja hicho cha Gallapo peke yake kina trekta 51. Kwa hiyo ni maendeleo makubwa sana ndiko kwenye kilimo kule. Sasa kijiji cha Halla kipo karibu na Gallapo umeme ulipita ukapelekwa Gallapo sasa hapo nyuma katikati pamerukwa na Halla vile vile ni wazalishaji wa kahawa na mazao mengine ya ndizi na mazao ya kawaida na maharage kwa wingi katika eneo lile, kwa hiyo, ni eneo la wazalishaji kwa kweli. Nilikuwa naomba vile vile basi na umeme mwingine uteremshwe pale Hara ili na wale wananchi kwa kweli waweze kufaidika.

Mheshimiwa Spika, vile vile katika Kata ya Nangara kuna mitaa ya Aari, Balowa pamoja na Maweni. Pale kuna watu wenye uwezo wa kutosha kuweza kuunganisha umeme kwenye nyumba zao. Lakini umeme haujasambazwa mpaka eneo lile. Lakini inaonekana pengine labda *TANESCO* ndio hawana uwezo sasa wote tulipitisha hapa Mfuko wa Umeme Vijijini Mheshimiwa Waziri amesema hapa mfuko huo utaanza kazi baada ya Mkurugenzi Mkuu kuteuliwa na watendaji wake. Sasa sina hakika kama mfuko ndio utaweza kusaidia kusambaza umeme katika maeneo hayo, lakini kama sivyo basi

Serikali ihakikishe kwamba inatoa fungu la kutosha kwa *TANESCO* ili vijiji vipatiwe umeme.

Mheshimiwa Spika, katika Sera ya Uwezeshaji, mimi nilidhani ni vizuri sasa mpango huu vile vile uwahusu watu wanaotaka kuunganisha umeme. Gharama ya kuunganisha umeme ni kubwa kwa watu wa kawaida lakini katika mpango wa uwezeshaji hawa watu wangeweza kukopeshwa na wakalipa taratibu kwa njia hiyo tungeweza kupata maendeleo kwa haraka zaidi. Kwa hiyo, nilikuwa nadhani kwamba ni vizuri ebu tuone Serikali mkae chini muangalie ni namna gani mnaweza mkaharakisha maendeleo katika sekta hii. Kama nilivyosema hii ndiyo silaha pekee ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, naona niseme hayo tu yanatosha na niunge mkono hoja nikiwa na matumaini kwamba Mheshimiwa Waziri baada ya kupita hayo maeneo basi atahakikisha kwamba eneo hilo la Bonga na Haraa na maeneo niliyoyataja yatapatiwa umeme. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda uliosalia hautoshi kuendelea na mjadala huu badala yake tutaendelea kesho. Lakini kwa kumbukumbu tu ningependa kuyasoma majina ya wale ambao nadhani wataweza kuongea asubuhi. Tutaanza na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi, atafuatia Mheshimiwa Raynald Mrope, halafu Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Richard Nyaulawa, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Salum Hemed Khamis, Mheshimiwa Ezekiel Maige na pengine tutamfikia Mheshimiwa Bujiku Philip Sakila kabla ya saa 7.00 mchana. Hao ndio wajiandae kwa kesho asubuhi.

Sasa kwa kuwa muda hautoshi na nimekumbushwa kwamba kwa mujibu wa mazoea na utamaduni wetu ninayo madaraka ya kuahirisha Bunge kabla ya wakati wake. Kwa hiyo, sasa naliahirisha Bunge kabla ya wakati wake hadi kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.40 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumanne,*
*Tarehe 18 Julai, 2006 saa tatu asubuhi)*